



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

HOTUBA YA WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO, MHE. UMMY A. MWALIMU (MB), KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2017/18



Madaktari bingwa wa upasuaji wa Moyo na Mishipa ya damu katika Taasisi ya Jakaya Kikwete (JKCI) wakimfanyia mgojwa upasuaji wa moyo kwa jina la kitaalam Coronary Artery Bypass Graft

HOTUBA YA WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO, MHE. UMMY A. MWALIMU (MB), KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2017/18

I. UTANGULIZI

- 1. Mheshimiwa Spika**, kufuatia taarifa iliyowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii ndani ya Bunge lako Tukufu, ambayo imechambua Bajeti ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Kazi za Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa mwaka 2016/17 na Vipaumbele vya Wizara kwa mwaka 2017/18. Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Kawaida na Mpango wa Maendeleo ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa mwaka 2017/18.
- 2. Mheshimiwa Spika**, baada ya kumshukuru Mwenyenzi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa, napenda kuchukua fursa hii kwa heshima na unyenyekevu mkubwa kumshukuru kwa dhati **Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake imara kwa nchi yetu na maelekezo yake ambayo yamekuwa dira sahihi katika utendaji wangu na katika kuimarisha huduma za Afya na ustawi ya jamii nchini. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuweka chachu katika kudhibiti matumizi ya madawa ya kulevyo nchini ikiwa ni katika jitihada zake za kulinda afya za Watanzania hasa vijana ambao ndiyo nguvu kazi ya Taifa letu. Kwa jinsi hiyo, Wizara itaendelea kuelimisha na kuhimiza umma wa Watanzania kuhusu madhara yatokanayo na matumizi ya madawa ya kulevyo sambamba na kuzingatia mfumo bora wa maisha.
- 3. Mheshimiwa Spika**, napenda kutoa shukrani za dhati kwa **Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan**, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa miongozo na ushauri

wake wa dhati hasa katika kuboresha huduma za afya ya mama na mtoto na masuala ya kuwawezesha wanawake kiuchumi. Wizara yangu itaendelea kutumia taswira, ushawishi na uzoefu wake ili kujenga jamii ya watanzania inayowajali, kuwaheshimu na kuwaendeleza wanawake na wasichana kwa ajili ya kuwa na maendeleo ya kweli na endelevu katika nchi yetu

4. **Mheshimiwa Spika**, naomba kuchukua fursa hii kumshukuru **Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa (Mb)**, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake ambao umesaidia kuongeza ufanisi katika utendaji na kuimarisha huduma zinazotolewa na Wizara yangu. Aidha, naomba nimpongeze kwa hotuba yake aliyoiwasilisha kwenye Bunge hili ambayo imetoa dira ya jinsi Serikali itakavyotekeleza majukumu yake katika mwaka 2017/18.
5. **Mheshimiwa Spika**, napenda kukupongeza wewe binafsi, kwa kuendelea kutekeleza majukumu yako kwa weledi katika kuliongoza Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, nampongeza **Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson (Mb.)** kwa ushirikiano wake kwako, katika kutekeleza majukumu yako. Vilevile, nichukue fursa hii kuwapongeza Wenyeviti wa Bunge kwa kusimamia vyema mijadala ndani ya Bunge.
6. **Mheshimiwa Spika**, napenda nimshukuru **Mheshimiwa George Boniface Simbachawene (Mb)** Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa ushirikiano wake uliowezesha kusimamia na kuboresha utoaji wa huduma za afya nchini hasa afya ya msingi. Pia, nawashukuru Mawaziri wa Wizara nyingine zote ambazo ushirikiano wao na Wizara yangu umechangia katika utoaji wa huduma za afya na maendeleo ya jamii.
7. **Mheshimiwa Spika**, kipekee napenda kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, chini ya Mwenyekiti wake **Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba (Mb)**, na Makamu Mwenyekiti, **Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu (Mb)**

kwa ushauri na maelekezo waliyoyatoa wakati wa maandalizi ya Bajeti hii. Aidha nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushirikiano mzuri wanaonipatia ikiwemo kutoa ushauri na maoni mbalimbali yenye lengo la kuboresha huduma za afya na ustawi wa jamii nchini. Ninawashukuru sana! Ninawaahidi kwamba, Wizara yangu itazingatia ushauri wao na kuendelea kuwapa ushirikiano katika kutekeleza majukumu na kazi zetu za kuwatumikia wananchi ndani na nje ya Bunge.

8. **Mheshimiwa Spika**, napenda kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Abdallah Majura Bulembo (Mb), Mheshimiwa Anna Kilango Malecela (Mb), Mheshimiwa Prof. Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi (Mb), Mheshimiwa Juma Ali Juma (Mb), Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete (Mb) na Mheshimiwa Getrude Pangalile Rwakatare (Mb) kwa kuwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha nampongeza Prof. Kabudi kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Katiba na Sheria. Ninawaahidi kuwapa ushirikiano ili tuendee kuwatumikia wananchi kwa pamoja.
9. **Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa pole kwako, Bunge lako Tukufu, kwa familia na wananchi wa Jimbo la Dimani kwa kifo cha **Mheshimiwa Hafidh Ally Tahir** na **Dkt. Ely Marko Macha** aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum, CHADEMA. Aidha, natoa pole kwako na watanzania wote, ndugu, jamaa na marafiki waliopoteza ndugu na jamaa zao kutokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na magonjwa, ajali na majanga. Pia, natoa pole kwa wagonjwa na majeruhi wa ajali waliopo hospitalini na majumbani pamoja na wahanga wa vitendo vya ukatili na unyanyasaji wa kijinsia. Namuomba Mwenyezi Mungu awaponye haraka ili waweze kuendelea na ujenzi wa Taifa.
10. **Mheshimiwa Spika**, Baada ya kusema hayo, ninapenda sasa kutoa maelezo kuhusu utekelezaji wa shughuli za Wizara kwa mwaka 2016/17, Vipambebele vya Wizara kwa mwaka 2017/18 pamoja na maombi ya fedha ambazo zitaiwezesha Wizara yangu kutekeleza majukumu yetu.

II. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI NA MPANGO WA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2016/17

11. **Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza majukumu yake, Wizara imeendelea kuzingatia Sera, Mipango na Mikakati mbalimbali ya kitaifa na kimataifa ikiwa ni pamoja na Malengo ya Maendeleo Endelevu (2030), Dira ya Taifa ya Maendeleo (2025), Mpango wa II wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17 – 2020/21), Sera ya Afya (2007), Mpango Mkakati wa IV wa Sekta ya Afya (2016 - 2020) na Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM 2007 – 2017). Aidha tumezingatia Sera ya Taifa ya Wazee (2003), Sera ya Maendeleo ya Jamii (1996), Sera ya Maendeleo ya Mtoto (2008), Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia (2000), Sera ya Taifa ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (2001). Vilevile, Wizara imeendelea kutekeleza malengo yaliyoainishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2015-2020.

Mapato na Matumizi ya Fedha - Fungu 52 (Afya)

12. **Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu kupitia Fungu 52 (Afya) hukusanya mapato yake kupitia Bodi na Mabaraza mbalimbali, ada za uchangiaji wa gharama za mafunzo, marejesho ya masurufu, malipo ya ununuzi wa vitabu vya maombi ya zabuni, pamoja na makusanyo yatokanayo na utoaji wa huduma katika Taasisi na Mashirika yaliyo chini ya Wizara. Hadi kufikia mwezi Machi 2017, Wizara imekusanya jumla ya Shilingi **118,701,870,697.00** ikilinganishwa na makadirio ya Shilingi **157,786,384,366.00** yaliyoidhinishwa kwa mwaka 2016/17. Makusanyo haya ni sawa na asilimia **75** ya makadirio ya makusanyo ambapo usimamizi thabiti pamoja na matumizi ya mifumo ya Kielektroniki vimechangia kwa kiasi kikubwa kupatikana kwa ufanisi huu.
13. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/17, jumla ya **Shilingi 796,115,856,780.00** ziliidhinishwa kwa ajili ya utekelezaji wa

majukumu ya Wizara. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 277,629,895,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 518,511,683,780.00** ikiwa ni kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia mwezi Machi, 2017, jumla ya **Shilingi 339,194,232,240.85** zilipokelewa ikiwa ni **asilimia 43** ya fedha zilizoidhinishwa. Kati ya fedha zilizopokelewa **Shilingi 205,321,959,485.85 sawa na asilimia 74** ni fedha za Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 133,872,272,755.00 sawa na asilimia 26** ni fedha za Miradi ya Maendeleo (Vyanzo vya Ndani: Asilimia 37; Vyanzo vya Nje: Asilimia 8 kwa mfumo wa *Exchequer*). Aidha, tumepokea vifaa, vifaa tiba na dawa vyenye thamani ya **Shilingi 256,238,088,964.00** kutoka Mfuko wa Dunia wa Kupambana na UKIMWI, Malaria na Kifua Kikuu ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa bajeti ya miradi ya maendeleo.

Fungu 53 - Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto

14. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/17, Wizara kupitia Fungu 53, ilitarajia kukusanya jumla ya **Shilingi 2,382,679,000**. Vyanzo vya mapato ikiwa ni ada za wanafunzi katika Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na ada za Mashirika Yasio ya Kiserikali. Hadi kufikia mwezi Machi, 2017, makusanyo yalifikia **Shilingi 930,281,152** sawa na **asilimia 39.0**.
15. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/17, jumla ya **Shilingi 49,857,955,920** ziliidhinishwa kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya Wizara kupitia Fungu hili. Kati ya hizo, Matumizi ya Kawaida ni **Shilingi 41,009,372,644** yakijumuisha **Shilingi 18,669,129,000** kwa ajili ya mishahara na **Shilingi 22,340,243,644** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Bajeti ya matumizi ya Miradi ya Maendeleo iliyoidhinishwa ilikuwa **Shilingi 8,848,583,276** kati ya fedha hizo, **Shilingi 5,365,400,000** ni fedha za ndani na **Shilingi 3,483,183,276** ni fedha za nje. Hadi kufikia mwezi Machi, fedha za Matumizi Mengineyo **Shilingi 4,950,097,864** zilipokelewa sawa na **asilimia 28.4** ya bajeti iliyoidhinishwa na **Shilingi 7,866,426,933** za Mishahara zilipokelewa sawa na **asilimia 42.1** ya bajeti iliyoidhinishwa. Vilevile, katika bajeti ya miradi ya Maendeleo,

Shilingi 497,718,250 zilipokelewa ambapo **Shilingi 204,217,000** (3.8%) ni fedha za ndani na **Shilingi 293,501,250** (8.4%) ni fedha za nje.

16. **Mheshimiwa Spika**, ifuatayo ni taarifa kuhusu majukumu yaliyotekelezwa na Wizara katika kipindi cha Julai 2016 hadi Machi 2017;

UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA SEKTA YA AFYA

HUDUMA ZA KINGA

Udhibiti wa Magonjwa ya Kuambukiza na Yasiyo ya kuambukiza

17. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kutoa huduma za kinga nchini ambazo zinajumuisha udhibiti wa magonjwa ya kuambukiza, magonjwa yasiyo ya kuambukiza, huduma za uzazi na mtoto, lishe pamoja na utoaji wa elimu ya afya kwa umma. Katika kipindi cha 2016/17 Wizara ilitokeleza afua mbalimbali za huduma za kinga ikiwa ni pamoja na;

Huduma za Chanjo

18. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kutoa huduma za Chanjo kulingana na Sera na Miongozo. Aidha, Wizara kupitia Mpango wa Taifa wa Chanjo, imehakikisha kuwepo kwa chanjo za kutosha kwa ajili ya **huduma za chanjo kwa watoto** na makundi mengine kwa kununua na kusambaza chanjo katika Mikoa na Halmashauri zote nchini. Serikali ilitumia jumla ya **Shilingi bilioni 18 kununulia chanjo na vifaa vya kutolea chanjo**. Chanjo zilizonunuliwa kwa mwaka 2016/2017 zilikuwa **BCG** (chanjo ya kifua kikuu) dozi 6,000,000, **Polio** dozi 6,000,000, **Penta** (chanjo ya dondakoo, kifaduro, homa ya ini, Preumonia, homa ya uti wa mgongo na kichomi) dozi 5,975,500, **PCV** (chanjo ya homa ya nimonia na homa ya uti wa mgongo) dozi 5,082,200, **Rota** (chanjo dhidi ya ugonjwa wa kuharisha) dozi 3,303,400, **TT** (chanjo ya Pepo punda kwa wajawazito) dozi 2,480,000, **Surua Rubella** dozi 4,797,600 na

HPV (chanjo ya saratani ya mlango wa kizazi) dozi 67,100. Hii imeweza nchi yetu kuwa miongoni mwa nchi zilizofanya vizuri katika utoaji wa huduma za chanjo kwa mwaka 2016, ambapo tuliweza kuvuka lengo kwa kufikia kiwango cha chanjo cha asilimia 97.

19. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/2017, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa chanjo **imenunua magari 9** kwa ajili ya kuboresha huduma za usambazaji wa chanjo, usimamizi elekezi na ufuatiliaji wa magonjwa yanayozuilika kwa chanjo. Kati ya magari hayo, manne ni ya tani 3.5 na yana vyumba vya ubaridi. Aidha, Wizara ilinunua na **kusambaza majokofu 317 ya kutunzia chanjo** kwenye vituo vya huduma za afya ambapo majokofu 70 yanatumia mionzi ya jua na 247 yanatumia gesi. Vilevile Wizara **imeanzisha mfumo wa kukusanya taarifa za chanjo ikiwa** ni pamoja na ufuatiliaji wa chanjo kutoka ngazi ya Taifa hadi kwenye vituo vya kutolea chanjo (Vaccination Immunization Management System (VIMS)). Mfumo huu umeshapelekwa kwenye mikoa saba ambayo ni Dar es salaam, Lindi, Njombe, Arusha, Mtwara, Tabora na Mwanza.

Udhibiti wa Magonjwa ya Mlipuko

20. **Mheshimiwa Spika**, Wizara iliendelea kufuatilia mwenendo na viashiria vya magonjwa yanayotolewa taarifa kitaifa na kimataifa ikiwa ni pamoja na magonjwa ya milipuko. Katika mwaka 2016/17 nchi yetu ilikumbwa na **ugonjwa unaosababishwa na sumu kuvu (Aflatoxicosis)**. Hata hivyo Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ilidhibiti ugonjwa huo. Aidha, Wizara iliendesha mafunzo kwa watumishi wa afya mipakani, bandarini, viwanja vya ndege na bandari kavu kuhusu namna ya kukabiliana na magonjwa ya kuambukiza ikiwemo **Ebola**. Mafunzo haya yalishirikisha watumishi na wadau 110. Vilevile, Wizara imeandaa Mpango Mkakati wa Kitaifa wa Kukabiliana na Milipuko na Majanga ili kulinda usalama wa nchi kiafya (National Health Security Plan, 2017-2021). Utekelezaji wa Mpango huo umeshaanza.

21. **Mheshimiwa Spika**, ugonjwa wa kipindupindu uliendelea kutolewa taarifa na kudhibitiwa kwa kiasi kikubwa ambapo hadi Machi 2017, jumla ya wagonjwa 2,927 waliripotiwa na vifo 46 viliripotiwa. Wizara inaendelea kushirikiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI katika kupanga mikakati ya kudhibiti ugonjwa huo na magonjwa yote ya milipuko ambapo mafunzo yalitolewa kwa Mikoa na Halmashauri zilizoathiriwa na ugonjwa huo. Mafunzo hayo yalijielekeza zaidi katika matumizi ya maji safi na salama, usafi wa mazingira na usafi binafsi wa mwili. Aidha, jumla ya **tani 50 za dawa ya kutibu maji ya kunywa (Chlorine)** ilisambazwa katika mikoa ya Dar es Salaam, Lindi, Pwani, Morogoro, Iringa, Mwanza, Mara, Kagera, Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Dodoma, Mbeya, Rukwa, Singida, Kigoma na Manyara ambayo iliathiriwa zaidi na ugonjwa wa kipindupindu. Visima virefu 18 vya maji vilichimbwa katika Mikoa ya Mara na Mwanza kupitia msaada wa Shirika la Afya Ulimwenguni (WHO).
22. **Mheshimiwa Spika**, katika kuimarisha udhibiti wa **ugonjwa wa homa ya manjano**, Wizara imeendelea kuhamasisha wananchi wanaotegemea kusafiri nje ya nchi kuhusu umuhimu wa kupatiwa chanjo ya ugonjwa huo siku 14 kabla hawajasafiri ambapo kati ya Julai 2016 hadi Machi 2017 **wananchi 26,045 wamepatiwa chanjo** hiyo. Sambamba na uhamasishaji huo, Wizara imezindua **vyeti vipya vya Homa ya Manjano** vilivyoboreshwa vyenye alama maalum ya siri ambayo itazuia kughushi vyeti hivyo, ambapo kuanzia mwezi Agost 2016 mpaka sasa jumla ya **vyeti 34,000** vimebadilishwa kote nchini.

Usafi wa Mazingira

23. **Mheshimiwa Spika**, Wizara iliendelea kuratibu awamu ya pili ya Kampeni ya Kitaifa ya Usafi wa Mazingira (2016-2021) ambapo katika mwaka 2016/17, jumla ya kaya **391,937** zimejenga vyoo bora, kati ya hizi, kaya **320,894** zina sehemu maalum ya kunawa mikono mara baada ya kutoka chooni.

24. **Mheshimiwa Spika**, ili kuongeza chachu ya ushindani katika kutekeleza Kampeni ya Kitaifa ya Usafi wa Mazingira, Wizara iliendesha mashindano ya Afya na Usafi wa Mazingira na kutoa zawadi mbalimbali kwa Halmashauri zilizofanya vyema. Katika mashindano hayo, Halmashauri ya Wilaya ya Njombe iliibuka mshindi wa jumla kitaifa na kukabidhiwa zawadi ya gari jipya aina ya Toyota Hardtop 4WD. Zawadi nyingine zilizotolewa kwa washindi ni pamoja na pikipiki 17, vyeti na vikombe. Aidha, katika kujenga uwezo wa Halmashauri kusimamia na kufuatilia shughuli za afya mazingira, Wizara ilinunua na kugawa jumla ya pikipiki kwa Halmashauri 100 nchini hususani za vijijini (**Kiambatisho Na.1**)

Udhibiti wa Magonjwa Yaliyokuwa Hayapewi Kipaumbele

25. **Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Magonjwa yaliyokuwa hayapewi kipaumbele imeendelea kugawa dawa za kingatiba za matende, mabusha, usubi, trakoma, kichocho na minyoo ya tumbo katika Halmashauri zote zenye maambukizi haya. Katika kipindi cha Julai 2016 hadi Machi 2017, mpango umegawa dawa katika **Halmashauri 71 na kufikia watu milioni 14.3** katika mikoa ya Dar Es Salaam, Pwani, Ruvuma, Rukwa, Mbeya, Dodoma, Singida, Tanga, Tabora, Manyara, Mtwara, Lindi na Morogoro. Katika zoezi hilo serikali imesambaza **vidonge milioni 54.5** vya dawa ya Mectizan kwa ajili ya kuzuia maambukizi ya ugonjwa wa usubi na Matende, **vidonge milioni 23.8** vya albendazole kwa ajili kuzuia maambukizi ya ugonjwa waminyoo ya tumbo, **vidonge milioni 13.3** vya dawa ya Prazquantel kwa ajili kuzuia maambukizi ya ugonjwa wa kichocho na **dozi million 8.7 ya dawa ya Mectzan** kwa ajili kuzuia maambukizi ya ugonjwa wa trakoma.
26. **Mheshimiwa Spika**, Serikali imefanya **kambi za upasuaji kwa wagonjwa 805 wa matende na mabusha** bila malipo ambapo 705 ni katika Halmashauri ya Temeke na Ilala jijini Dar es salaam na 100 katika mkoa wa Mtwara. Wizara ilifanya tathmini ya kiwango cha maambukizi ya ugonjwa wa matende na mabusha

katika Halmashauri 27 za mikoa ya Dodoma, Katavi, Rukwa, Singida, Lindi, Mtwara, Ruvuma na Pwani. Matokeo ya tathmini hii yameonesha kushuka kwa kiwango cha maambukizi katika Halmashauri zote na hivyo hazihitaji tena ugawaji dawa wa kingatiba; isipokuwa katika Halmashauri ya Kondoa na Chemba.

Udhibiti wa Malaria

27. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea na juhudi za udhibiti wa malaria nchini, kwa kutekeleza afua mbalimbali zinazopendekezwa kimataifa, ili kuhakikisha kuwa wananchi wanapata kinga na matibabu pale wanapothibitika kuwa na vimelea vya malaria.
28. **Mheshimiwa Spika**, katika kuendelea na mapambano dhidi ya Malaria, Wizara imesambaza **dawa za kutibu malaria na vipimo vya kupima malaria (mRDT)** kwenye mikoa 26 ya Tanzania Bara. Katika kipindi cha Julai 2016 hadi Machi 2017, jumla ya **dozi za ALU 12,530,040 na Vitepe vya mRDT 15,511,500** vimenunuliwa na kusambazwa katika vituo vya huduma za afya nchini. Aidha, uhamasishaji wa jamii juu ya matumizi ya kipimo cha mRDT na matibabu sahihi ya malaria kupitia kampeni ya “SIO KILA HOMA NI MALARIA NENDA UKAPIME” umeendelea kufanyika katika mikoa yote nchini.
29. **Mheshimiwa Spika**, unyunyiziaji wa dawa ukoka umefanyika katika mikoa minne ya Kanda ya Ziwa ambayo ina maambukizi makubwa zaidi ya malaria hapa nchini ambayo ni (Kagera, Mwanza, Mara na Geita). Pia kampeni ya ugawaji wa vyandarua vyenye viuatilifu vya muda mrefu imetekelezwa katika Halmashauri ya Kilombero Mkoa wa Morogoro na Halmashauri zote za Mkoa wa DSM. **Jumla ya vyandarua 2,617,465** vilinunuliwa na kusambazwa katika Halmashauri hizo. Hivyo kukamilisha jumla ya Mikoa 23 ya Kigoma, Katavi, Rukwa, Songwe, Mbeya, Iringa, Njombe, Dodoma, Singida, Tabora, Shinyanga, Manyara, Tanga, Pwani, Dar es Salaam, Arusha, kilimanjaro, Mara, Simiyu, Mwanza, Geita, Kagera na Morogoro ambayo ilikuwa imelengwa na kampeni ambapo jumla ya vyandarua 27,189,572 vimesambazwa kwa kipindi cha mwaka 2015/2016 na 2016/2017.

Udhibiti wa Kifua Kikuu na Ukoma

30. Mheshimiwa Spika, huduma za kifua kikuu na Ukoma zimeendelea kuimarika nchini ambapo mafanikio makubwa yameendelea kupatikana. **Kwa hivi sasa kiwango cha wagonjwa wanaotibiwa na kupona ni asilimia 90 kati ya waliogunduliwa kuugua kifua kikuu.** Wizara imeendelea kuboresha huduma za vipimo kwa kuimarisha maabara 4 za Kanda ya Mbeya (Hospitali ya Rufaa Mbeya), Mwanza (Bugando Medical Centre), Dodoma (Hospitali ya Rufaa ya Mkoa) na Kilimanjaro (Hospitali ya Kibong'oto) ambazo zimeweza kufunguliwa na kuanza kutoa huduma za uchunguzi wa vimelea vya kifua kikuu. Hapo awali huduma hii ilikuwa inapatikana katika maabara moja tu iliyopo katika Hospitali ya Taifa Muhimbili.

31. Mheshimiwa Spika, huduma za uchunguzi na matibabu ya **kifua kikuu sugu** zimeimarishwa na kusogezwa karibu na wananchi. Awali huduma hizi zilikuwa zinatolewa katika hospitali ya Kibong'oto (Kilimanjaro) pekee, ambapo kuanzia Mwezi Desemba 2016 jumla ya vituo 18 vimeanza kutoa huduma hiyo. Vituo hivyo ni Tambuka reli, Bukombe, Mbogwe (Geita), Hospitali Amana, Ukonga, Rangi tatu na Sinza (Dar es salaam), Newala (Mtwara), Ifakara-Kibaoni (Morogoro), Bagamoyo (Pwani), Hospital ya Rufaa ya Kanda Mbeya, Ruanda, Mana (Mbeya), Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Kagera, Rubya, Kamachumu (Kagera), Tanga Mjini (Tanga) na Bariadi (Simiyu). Aidha, shughuli mbalimbali za uelimishaji na uhamasishaji jamii kuhusu Kifua Kikuu zilitekelezwa ikiwemo kuendesha Kampeni kupitia vyombo vya habari (TV, Radio) yenye lengo la kuibua wagonjwa wapya wa kifua kikuu kwa kuwa ni asilimia **39 tu** kati ya **wagonjwa 162,000** waliopo nchini ndio waliopo katika matibabu. Tunamshukuru Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mama Samia Suluhu Hassan kwa kuongoza mapambano dhidi ya kifua kikuu.

32. **Mheshimiwa Spika**, Wizara pia imeendesha Semina kwa Waheshimiwa Wabunge mwezi Novemba, 2016, ambayo iliwezesha kuanzishwa rasmi kwa **Umoja/Mtandao wa Wabunge wanaofuatilia masuala ya Kifua Kikuu**, (Tanzania Parliamentary TB Caucus) ikiwa ni utekelezaji wa maazimio ya kimataifa. Nitumie fursa hii kumpongeza Dkt. Faustine Ndugulile kwa kuwa Mwenyekiti wa kwanza wa Tanzania Parliamentary TB Caucus. Aidha, nawapongeza wabunge wote kwa kuwa chachu ya mapambano dhidi ya kifua kikuu. Napenda kutumia fursa hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Viongozi wa Dini, Madiwani na jamii kwa ujumla kuhimiza wananchi wote wenye dalili za ugonjwa wa kifua kikuu kupata tiba mara moja. Tusipofanya hivyo tunaiweka nchi katika hatari zaidi ya kuwa na wagonjwa wengi wa kifua kikuu kwa kuwa mtu mmoja anayeugua na hajanza tiba anauwezo wa kuambukiza hadi watu 20 kwa mwaka. Nisisitize kuwa **Kifua Kikuu Kinatibika na Huduma za Kupima na Matibabu hutolewa bila Malipo**.
33. **Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha tunaibua wagonjwa wapya wa kifua kikuu, Wizara kwa kushirikiana na Sekta Binafsi inatekeleza Mpango wa Taifa wa Kifua Kikuu na Ukoma wa 2015-2020 **wa kuibua wagonjwa wa kifua kikuu kupitia sekta binafsi**; ambapo mwaka 2016 jumla ya wagonjwa 7,090 kati ya 65,785 sawa na asilimia 11 waliibuliwa kupitia vituo vya afya vinavyomilikiwa na Sekta Binafsi. Aidha, Wizara ilishirikisha maduka ya dawa muhimu (ADDO) katika kuibua wagonjwa wa Kifua kikuu, jumla ya wauza dawa 300 kutoka mikoa 10 walipatiwa mafunzo ya mfumo wa utoaji wa rufaa za wahisiwa wa ugonjwa wa kifua kikuu. Vilevile, Wizara imeongeza wigo wa utoaji huduma za kifua kikuu katika vituo binafsi vya afya kutoka asilimia 10 mwaka 2014 hadi asilimia 15 mwaka 2016.
34. **Mheshimiwa Spika**, kuhusu jitiada za **kutokomeza ugonjwa wa ukoma**, Wizara imeendelea kufanya kampeni maalum ya utoaji elimu kwa jamii kuhusu dalili za ukoma na namna ya kutambua mapema wagonjwa katika hatua za awali za ugonjwa. Kampeni hiyo imetekelezwa katika wilaya za Kilombero, Liwale na

Nanyumbu ambapo jumla ya wagonjwa 61 waligunduliwa. Hii inaonesha kuwa bado kuna uwepo wa ugonjwa huu katika wilaya hizi.

Udhibiti wa UKIMWI

35. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka 2016/17, Wizara imeendelea na juhudi za kudhibiti UKIMWI kwa kutoa ushauri nasaha na kupima virusi vya UKIMWI (VVU). Kuanzia mwezi Januari hadi Desemba, 2016 jumla ya **wateja wapya 7,447,102 walipata ushauri nasaha na kupima VVU**. Aidha, Wizara imepanua wigo wa utoaji huduma za tiba na matunzo kwa watu wanaoishi na VVU. Hadi kufikia Desemba 2016, vituo **6,155** vilikuwa vinatoa huduma za tiba na matunzo kwa watu wanaoishi na VVU. Kati ya vituo hivyo vituo **5,690 (92%)** vinatoa huduma za maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto. Vilevile, Wizara **imeanzisha mfumo wa ufuatiliaji wa watoto wachanga waliozaliwa na mama wenye maambukizi ya VVU**. Programu hii imeweza kufanya majaribio ya mfumo mpya uitwao “Mother baby cohort monitoring system” katika mikoa 5 ya Iringa, Mbeya, Pwani, Tanga na Tabora ambapo tathmini yake imeonyesha kuwa mfumo huu unafaa kuanza kutumika katika mikoa yote nchini. Mpango huu utasaidia katika kubaini mapema watoto walioathirika na VVU.
36. **Mheshimiwa Spika**, kuanzia mwezi Oktoba 2016, Wizara ilianza **kutoa dawa za ARV** kwa watu wenye maambukizi ya Virusi vya VVU/UKIMWI (WAVIU) **bila kujali kiwango cha CD4** ambapo hadi Machi 2017 jumla ya WAVIU wanaotumia ART/ARV ni 849,594 ambayo ni sawa na asilimia 60 ya watu million 1.4 wanaokadiriwa kuwa na maambukizi ya VVU nchini. Kati ya hao watoto 55,670 wako kwenye matibabu ya ARV ambayo ni asilimia 50% ya lengo. Aidha, huduma mkoba za UKIMWI na Kifua kikuu zimeendelea kutolewa, na hadi Desemba 2016 asilimia **96** ya WAVIU wanaohudhuria kliniki za Tiba na matunzo wamepimwa hali zao za maambukizi ya kifua kikuu na dawa za **Isonizidi** ya kuzuia maambukizi ya Kifua kikuu kwa WAVIU inatolewa katika vituo **512** sawa na asilimia **30** ya vituo vya matunzo na Tiba kwa

WAVIU. Pia, Wizara imefungua mashine mpya **14** za kupima uwingi wa virusi vya UKIMWI {viral load} katika damu katika hospitali za rufaa za mikoa ya Mtwara, Dodoma, Tabora, Iringa, Morogoro, Arusha, Ruvuma, Kagera na Rukwa Hospitali za Rufaa za Kanda - Bugando, Mbeya, KCMC, Hospitali ya Taifa ya Muhimbili na Maabara ya Taifa ya Viwango na Ubora.

37. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kutekeleza afua ya **tohara kwa wanaume** kama mojawapo ya afua ya kupambana na maambukizi ya VVU. Kuanzia mwezi Januari hadi Desemba, 2016 jumla ya wanaume **374,411** kati ya lengo la wanaume **492,844** wenye umri wa kati ya miaka 10 hadi 49 wamepata huduma ya Tohara kutoka mikoa 14 ya kipaumbele (Mbeya, Songwe, Katavi, Rukwa, Ruvuma Njombe, Iringa, Tabora, Shinyanga, Mwanza, Geita, Simiyu, Mara (Wilaya ya Rorya) na Kagera na kufikisha jumla ya wanaume **2,203,230** waliokwisha kupata huduma hiyo tangu ilipozinduliwa nchini mwaka 2010. Idadi hiyo ni sawa na asilimia **79** ya wanaume **2,800,000** wanaopaswa kufikiwa ifikapo mwaka 2017.
38. **Mheshimiwa Spika**, Wizara kwa kushirikiana na wadau imebuni kifungashio kipya kwa kondom ya kiume ambayo imekuwa ikitolewa na serikali na kuipa jina la ZANA. **Kondom ya ZANA** ilizinduliwa kitaifa katika mkoa wa **Mbeya** na kutambulishwa kwa umma na hali kadhalika, uzinduzi ulifanyika pia katika mikoa ya **Mwanza, Arusha, Tanga, Dodoma, Mtwara, Kigoma na Morogoro**. Jumla ya kondom za **ZANA 21, 000,000** ziliagizwa na kusambazwa katika mikoa yote kupitia Bohari ya Dawa.

Udhibiti wa Magonjwa Yasiyo ya Kuambukiza Nchini

39. **Mheshimiwa Spika**, kutokana na ongezeko kubwa la Magonjwa yasiyo ya kuambukiza kama vile Kisukari, Shinikizo la Damu na Magonjwa ya Moyo, Wizara imeandaa Mkakati wa Kitaifa wa kupambana na magonjwa Yasiyo ya Kuambukiza wa 2016 – 2020 ambao ulizinduliwa Dodoma mwezi Novemba 2016. Hatua hiyo ilifuatiwa na kuanzishwa kwa Kampeni ya Kitaifa inayolenga katika

kuhamasisha wananchi kufanya mazoezi na kupima afya mara kwa mara na kuzingatia ulaji wa vyakula unaofaa. Kampeni hiyo ilizinduliwa na **Mhe. Makamu wa Rais Mama Samia Suluhu Hassan** mwezi Desemba 2016 jijini Dar es Salaam, ambapo pamoja na mambo mengine Mhe. Makamu wa Rais aliagiza kuwa kila Jumamosi ya Pili ya Mwezi iwe ni Siku ya Hamasa ya Kufanya Mazoezi.

40. **Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa agizo hilo umeanza mara moja ambapo Mikoa/Halmashauri mbalimbali inaandaa mazoezi ya pamoja angalau mara moja kwa mwezi lengo likiwa ni kujenga utamaduni kwa wananchi hasa wanaoishi mijini na wanaofanya kazi za ofisini kufanya mazoezi ya mwili mara kwa mara na hivyo kupunguza maradhi, ulemavu na vifo vitokanavyo na magonjwa yasiyo ya kuambukiza. Sambamba na kampeni ya mazoezi, Wizara imeendelea kuhamasisha wananchi kuzingatia mfumo bora wa maisha ikiwemo ulaji wa vyakula unaofaa, kupunguza unywaji wa pombe kupita kiasi, kujiepusha na matumizi ya sigara na bidhaa za tumbaku pamoja na kujenga utamaduni wa kupima afya mara kwa mara. Inategemewa kuwa, kutekelezwa kikamilifu kwa mikakati hii kutapunguza kwa kiasi kikubwa kasi ya kuongezeka kwa magonjwa haya nchini.

Udhibiti wa Matumizi ya Tumbaku na Kilevi

41. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea na utekelezaji wa afua mbalimbali zenye lengo la kuelimisha wananchi juu ya madhara ya Tumbaku, pamoja na kusimamia Sheria na Kanuni zinazohusu Uvutaji Sigara na matumizi ya mazao ya Tumbaku nchini kwa lengo la kulinda afya za wananchi. Katika kutekeleza hilo, Wizara imehakikisha kuwa Pakiti za Sigara zinazouzwa nchini hivi sasa zina maandishi ya onyo “Uvutaji wa Sigara una athari katika Afya” yanayoonekana kwa urahisi (yenye ukubwa wa asilimia 30). Aidha, kanuni za mwaka 2014 za kudhibiti matumizi ya tumbaku zilifanyiwa mapitio na kuongeza suala la udhibiti wa matumizi ya Shisha. Kanuni hizi zinatarajiwa kuanza kutumika rasmi kuanzia mwezi Julai 2017.

Huduma ya Afya ya Uzazi na Mtoto

42. **Mheshimiwa Spika**, Upatikanaji wa huduma inayofikiwa na wanawake wote, kabla ya ujauzito, wakati wa ujauzito, na wakati wa kujifungua hadi wiki sita baada ya kujifungua ni muhimili muhimu wa kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi. Hata hivyo, tatizo la vifo vitokanavyo na uzazi bado ni changamoto. Tafiti zilizofanyika hapa nchini mwaka 2015 zinaonyesha kwamba vifo vitokanavyo na uzazi havijapungua, ambapo takwimu zinaonesha idadi ya vifo ni 556 kwa kila vizazi hai 100,000. Katika kuimarisha huduma za Afya ya Uzazi na Mtoto nchini, Wizara imeandaa Mpango Mkakati unaotekelezwa kuanzia mwaka 2016 hadi 2020 unaolenga kuboresha afya ya uzazi, watoto na vijana pamoja na kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi kufikia 292 kwa kila vizazi hai 100,000 ifikapo mwaka 2020. Katika kutekeleza mkakati huo, Wizara imezingatia maeneo makuu matatu: ambayo ni: huduma ya uzazi wa mpango, huduma wakati wa ujauzito na huduma wakati wa kujifungua.
43. **Mheshimiwa Spika**, uzazi wa mpango ni eneo muhimu katika kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi na kuhakikisha afya nzuri kwa mama na mtoto. **Tafiti zinaonyesha kwamba uzazi wa mpango ukitumiwa kikamilifu, unaweza kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi kwa asilimia 30.** Hivyo, Wizara imekuwa ikitekeleza afua mbalimbali ili kuhakikisha kwamba huduma hii inapatikana kwa wote wanaohitaji. Katika kipindi cha Julai 2016 hadi Machi 2017, jumla ya **wateja 357,244** walifikiwa kupitia huduma za mkoba na **2,509,280** walifikiwa kupitia vituo vya kutolea huduma za afya. Wizara kwa kushirikiana na wadau imetoa mafunzo kwa watoa huduma **3,233** ili kuwajengea uwezo wa kutoa huduma za aina mbalimbali za uzazi wa mpango. Aidha, Wizara imenunua na kusambaza dawa za uzazi wa mpango ikiwa ni pamoja na **“Depo-provera” vichupa 4,973,811, “Microval” mizunguko (cycles) 743,615 na Kondomu za Kiume 13,096,916.** Utekelezaji wa afua hizo umewezesha kiwango cha kutumia uzazi wa mpango kupanda kutoka asilimia 27 mwaka 2010 hadi asilimia 32 mwaka 2015/16 (TDHS). Lengo ni kufikia asilimia 45 mwaka 2020.

44. **Mheshimiwa Spika**, kuhusu huduma wakati wa ujauzito imebainika kuwa matatizo mengi wakati wa ujauzito yanaweza kuzuilika, kugundulika na kutibiwa kama wanawake wajawazito watahudhuria kliniki ya wajawazito na kupimwa na wahudumu wenye ujuzi. Huduma zinazopaswa kutolewa katika kliniki za wajawazito ni pamoja na; chanjo ya pepopunda, kupimwa wingi wa damu, kupimwa protini kwenye mkojo, kupimwa kama kunauambukizo wa VVU na vimelea vya kaswende na kupewa matibabu. Huduma nyingine zinazotolewa ni kugundua dalili za hatari na kutoa matibabu mapema wakati wa ujauzito. Katika kipindi cha 2016/17, Wizara kwa kushirikiana na wadau iliendelea kuhakikisha huduma hizi zinapatikana sambamba na kuelimisha wajawazito kuhudhuria kliniki. **Kulingana na tafiti zilizofanyika mwaka 2015/16 asilimia 98 ya wajawazito wote walihudhuria kliniki angalau mara moja na asilimia 51 walihudhuria angalau mara 4** ambacho ni kiwango cha chini cha mahudhurio kinachopendekezwa. Lengo ni kufikisha asilimia 70 ya wanawake wajawazito kuhudhuria kliniki angalau mara 4 katika kipindi cha ujauzito ifikapo mwaka 2020. **Nitumie fursa hii kuwahimiza akinamama wajawazito kuhudhuria kliniki kama inavyoshauriwa.**

45. **Mheshimiwa Spika**, upatikanaji wa huduma wakati wa kujifungua ikiwemo huduma ya dharura wakati wa kujifungua hadi wiki sita baada ya kujifungua, ni muhimu sana ili kuepuka vifo vitokanavyo na uzazi. Huduma kwa matatizo haya hupatikana tu kwenye vituo vya kutolea huduma ya afya na mtoa huduma mwenye ujuzi. Katika mwaka 2016/17, Wizara kwa kushirikiana na wadau imeendelea kuhamasisha na kuhimiza wanawake wajawazito kujifungulia kwenye vituo vya kutolea huduma. Idadi ya akinamama wanaojifungulia katika vituo vya kutolea huduma imeongezeka kutoka **asilimia 51 mwaka 2010 hadi kufikia asilimia 64 mwaka 2015/16**. Napenda kutoa wito kwa wanawake wajawazito wote nchini wajifungulie kwenye vituo vya kutolea huduma ya afya ili kupunguza vifo na changamoto za uzazi kwa mama na mtoto. Aidha, Wizara imetoa mafunzo mbalimbali ya

uzazi salama na huduma za dharura wakati wa ujauzito na kujifungua kwa watoa huduma 1,300 nchini.

46. **Mheshimiwa Spika**, katika jitihada za kusogeza huduma karibu na wananchi, Wizara kwa kushirikiana na OR - TAMISEMI, imekamilisha **ukarabati wa vituo vya afya 8** katika Mikoa ya Mwanza, Geita, Simiyu na Mara ili viweze kutoa huduma za uzazi wa dharura ikiwemo upasuaji wa kutoa mtoto tumboni (CEmONC). Hadi sasa vituo vya Afya 171 vinatoa huduma za upasuaji na kati ya hivyo, 117 vinamilikiwa na Serikali ambapo ni sawa na asilimia 21 ya vituo vya afya **473** vinavyomilikiwa na Serikali. Aidha vituo vya afya 145 viko katika hatua mbalimbali za ukamilishaji ili kuweza kutoa huduma za dharura za uzazi ikiwemo upasuaji wa kutoa mtoto. Lengo la serikali ni kuhakikisha angalau asilimia 50 ya vituo vya afya nchini vinatoa huduma kamili za uzazi wa dharura ifikapo mwaka 2020.
47. **Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea kukabiliana na tatizo la uhaba wa damu hasa kwa wanawake wajawazito. Wizara kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI imeanzisha utaratibu wa kuwa na vituo vya benki za damu kwenye ngazi ya mikoa hapa ili visaidaine na benki za damu za kanda katika kuboresha upatikanaji wa damu salama. Hadi sasa Benki za damu za Mikoa **7** zimeanzishwa katika mikoa ya Dar es salaam, Lindi, Morogoro, Dodoma, Iringa, Kigoma na Shinyanga. Aidha, uanzishwaji wa benki hizo katika mikoa ya Mara na Kagera upo katika hatua za mwisho. Lengo ni kuhakikisha kila Mkoa una Benki ya Damu ikiwa ni jitihada za kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi.
48. **Mheshimiwa Spika**, Huduma za Rufaa kwa Wajawazito zimeendelea kuboreshwa ambapo Wizara imegawa **magari ya kubebea wagonjwa (Ambulance) 67** katika Halmashauri za Mikoa yote ya Kanda ya Ziwa na Kigoma na mikoa mingine hapa nchini. Aidha, Wizara imegawa **magari 8** kwa ajili ya kuratibu shughuli za afya ya mama na mtoto katika Kanda ya Ziwa, Kati, Magharibi, OR - TAMISEMI Dodoma, na magari 2 katika kitengo cha Afya ya mama na Mtoto Wizarani. Hatua hiyo itatoa msukumo

na kuimarisha juhudi za kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi katika mikoa hiyo ambayo takwimu zimeonesha kuwa wana vifo vingi zaidi kuliko mikoa mingine nchini.

49. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imechukua hatua kwa ajili ya **kuongeza uwajibikaji** kwa ngazi zote ili kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi kwa kutaka kila kifo cha mama na mtoto kinachotokana na matatizo ya uzazi kijadiliwe ndani ya saa 24 katika kituo/hospitali husika kwa lengo la kubaini chimbuko la kifo hicho na kuchukua hatua stahiki ikiwa ni pamoja na kuboreshwa zaidi kwa huduma zinazotolewa katika kituo husika. Miongozo imeandaliwa na mafunzo ya kujenga uwezo yamefanyika kwa mikoa yote nchini. Sambamba na hilo **Wizara kuanzia mwezi Oktoba 2016 imeanzisha utaratibu wa kutaka kila halmashauri na mikoa nchini kutoa taarifa ya vifo vitokanavyo na uzazi kila mwezi**. Taarifa hizi zinafanyiwa kazi na hatua stahiki zimekuwa zikichukuliwa na mrejesho kutolewa kwa Mikoa na Halmashauri husika.
50. **Mheshimiwa Spika**, kuhusu **vifo vya watoto**, kupitia Mpango Mkakati wa Afya ya Uzazi na Mtoto wa 2016-2020, Serikali imedhamiria kuwa ifikapo 2020 kupunguza vifo vya watoto wa chini ya mwezi mmoja kutoka 21 hadi 16 katika kila vizazi hai 1,000; vifo vya watoto wa chini ya umri wa mwaka mmoja kutoka 45 hadi 25 katika kila vizazi hai 1,000 na vifo vya watoto wa chini ya umri wa miaka mitano kutoka 54 hadi 40 katika kila vizazi hai. Katika mwaka 2016/17, Wizara imeendelea kuwajengea uwezo watoa huduma ya afya 241 katika wilaya tano za mkoa wa Iringa. Aidha katika kupunguza vifo vya watoto waliozaliwa na uzito pungufu, Wizara ilitoa mafunzo kwa watoa huduma 143 jinsi ya kumtunza mtoto mchanga kwa njia ya Kangaroo.
51. **Mheshimiwa Spika**, Jamii ni sehemu muhimu katika mikakati ya kuboresha afya ya uzazi na mtoto. Hivyo katika mwaka 2016/17 Wizara imetoa mafunzo ya afya ya uzazi na mtoto kwa wahudumu 1,649 wa afya kwa ngazi ya jamii (Community Health care Workers program) ambao wanatumika kuhamasisha na kuelimisha

jamii wanapoishi. Aidha Wizara imeanzisha mpango maalum wa kuwa na kada ya watoa huduma ngazi ya jamii watakaoajiriwa baada ya kupata mafunzo rasmi yaliyopitishwa na NACTE. Katika mwaka wa fedha 2016/17, jumla ya wahudumu 3,688 walihitimu mafunzo yao.

52. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea na juhudi za kudhibiti saratani za via vya uzazi (Reproductive cancers) ikiwemo saratani ya mlango ya kizazi, saratani ya matiti na saratani ya Tezidume. Katika kuhakikisha kuhakikisha upatianaji wa **huduma za kupima na matibabu ya Mabadiliko ya awali ya Saratani ya Mlango wa kizazi na saratani ya matiti** ambazo ndizo zinazoongoza nchini, vituo 360 vya kupima dalili za awali ya Saratani ya mlango wa kizazi vimeanzishwa na kutoa huduma hiyo katika mwaka wa fedha 2016/17. Aidha Taasisi za Serikali na mashirika yasiyo ya kiserikali yameendesha kampeni za kuelimisha jamii juu ya kudhibiti saratani za via vya uzazi sambamba na kuandaa kambi na huduma za kupima saratani za uzazi katika maeneo mbalimbali nchchi.

Huduma za Lishe

53. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/17, Wizara inaendelea kushirikiana na asasi mbalimbali za Serikali na zisizo za kiserikali kuhakikisha virutubishi muhimu kwa ukuaji wa mwili na akili vinaendelea kupatikana kote nchini. **Kwa sasa urutubishaji unaoendelea ni ule wa uongezaji wa virutubishi muhimu kwenye unga wa mahindi na unafanyika katika** mikoa ya Morogoro, Dodoma na Dar es Salaam wakati mikoa ya Iringa (Kilolo na Iringa vijijini), Njombe (Njombe mjini) na Arusha (Monduli, Karatu na Meru) inaendelea na mradi wa urutubishaji vijijini. Aidha usindikaji wa mafuta ya alizeti kwa kuongeza vitamini A unaendelea katika mikoa ya Singida na Manyara. Jumla ya mikoa 11 (Dodoma, Arusha, Morogoro, Dar es Salaam, Lindi, Iringa, Mbeya, Tabora, Rukwa, Mara na Simiyu) imefikwa kupitia mpango wa urutubishaji chakula kwa kutumia virutubishi nyongeza kwenye chakula cha kawaida kwa watoto wenye umri wa miezi 6 hadi 59 katika ngazi ya jamii (Home food Fortification). Kwa mujibu

wa takwimu za TDHS 2015/16 kaya zinazotumia chumvi yenye madinijoto kwa viwango vilivyowekwa kisheria zimeongezeka na kufikia asilimia 61 kutoka asilimia 47 mwaka 2010.

Elimu ya Afya kwa Umma

54. **Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2016/17, Wizara iliendelea kuelimisha na kuhamasisha jamii kutunza afya zao dhidi ya magonjwa na kufanya uchunguzi wa afya mara kwa mara. Wizara iliendelea kuelimisha jamii kujikinga na ugonjwa wa kipindupindu kupitia matangazo ya Radio, Runinga, simu za kiganjani kwa kupiga simu nambari 117 bila malipo. Aidha Wizara ilitayarisha na kusambaza kupitia mitandao ya kijamii elimu kuhusu magonjwa ya kuambukiza na yale yasiyo ya kuambukiza. Vilevile, Wizara ilihakiki matangazo na vielelezo mbalimbali vilivyotayarishwa na wadau, kuhusu ubora unaotakiwa ikiwa ni pamoja na kuzingatia Sera na Miongozo ya Wizara. Matangazo na Vielelezo hivyo vilihusu uzazi wa mpango, afya ya uzazi na mtoto, saratani ya mlango wa kizazi, lishe, chanjo, UKIMWI, kifua kikuu, afya ya mazingira, magonjwa yanayoambukiza na yasiyo ya kuambukiza, magonjwa yaliyokuwa hayapewi kipaumbele, malaria, afya ya kinywa na meno pamoja na macho. Wizara imekamilisha ujenzi wa studio ya radio na runinga ambazo zitaiwezesha Wizara kurekodi vipindi vya kuelimisha na kuhamasisha jamii.

HUDUMA ZA TIBA

Huduma za Damu Salama

55. **Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia Mpango wa Taifa wa Damu Salama imeendelea kutekeleza jukumu la ukusanyaji na usambazaji wa Damu Salama nchini, ambapo katika kipindi cha Julai 2016 hadi Machi, 2017 jumla ya chupa za damu **145,300** zilikusanywa, sawa na asilimia **63** ya lengo la kukusanya chupa **230,000** kwa mwaka. Chupa zote za damu zilizokusanywa ziliweza kupimwa kwa ufasaha magonjwa yote manne ambayo ni VVU, kaswende, homa ya ini aina B na C pamoja na kuangalia makundi ya damu, ambapo jumla ya chupa **130,408** sawa na asilimia **90**

zilionekana kutokuwa na maambukizi ya aina yoyote na hatimaye kusambazwa hospitalini kwa ajili ya kupewa wagonjwa wahitaji.

Huduma za Maabara za Uchunguzi wa Magonjwa

56. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/17, Wizara imeendelea kuboresha huduma za maabara ambapo hadi kufikia mwezi Machi 2017, jumla ya maabara **66** ambazo zipo katika ngazi za Mikoa, Wilaya na Vituo vya Afya, zilishiriki kwenye utaratibu wa Shirika la Afya Duniani wa kutoa Ithibati hatua kwa hatua, kwa kutoa nyota za viwango vya ubora wa huduma za maabara. Maabara **33** zilipata kati ya nyota moja **(1)** mpaka Tatu **(3)** za viwango vya ubora. Aidha, Maabara ya Taifa na zile za Kanda sita **(6)** zimepata ithibati ya SADCAS ya kiwango cha kimataifa yaani **ISO 15189:2012**. Maabara hizo ni Maabara ya Taifa ya Afya ya Jamii (NHLQATC), Hospitali ya Kanda Bugando (BMC), Hospitali ya Kanda Mbeya (MRH), Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) na Kilimanjaro Christian Medical Centre (KCMC). Pia, Wizara inaendelea na ujenzi wa maabara ya Taifa ya Afya ya Jamii katika eneo la Mabibo, Dar es salaam. Mradi huo hadi kukamilika unatarajiwa kutumia kiasi cha **Shilingi 7,493,193,434.97.00**.

Upatikanaji wa Dawa, Vifaa, Vifaa Tiba na Vitendanishi

57. **Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea kutoa kipaumbele katika kuboresha upatikanaji wa dawa kwa kununua, kutunza na kusambaza dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini. Katika mwaka 2016/17, Wizara ilitenga **Shilingi 251,500,000,000.00** kwa ajili ya kununua na kusambaza dawa, vifaa, vifaa tiba, na vitendanishi ikilinganishwa na kiasi cha **Shilingi 31,000,000,000.00** kilichotengwa mwaka 2015/16. Hadi kufikia Machi 2017, jumla ya **Shilingi 112,198,920,456** zilipokelewa ambazo ni sawa na **asilimia 45**. Hadi kufikia mwezi Machi 2017 mikoa/halmashauri/hospitali zimepokea zaidi ya asilimia 95 ya fedha za dawa. (**Kiambatisho Na.2**) Upatikanaji wa fedha hizi umeboresha upatikanaji wa dawa, vifaa na vifaa tiba nchini

ikilinganishwa na kipindi kilichopita. Nitumie furusa hii kuzitaka mamlaka za halmashauri na mikoa/hospitali kuhakikisha uwepo wa mifuko maalum ya dawa (drung revolving fund) katika maeneo yao ili kuhakikisha upatikanaji endelevu wa fedha za dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi.

58. **Mheshimiwa Spika**, Hadi kufikia Machi, 2017, asilimia **81 ya dawa muhimu zaidi (essential medical items) zinapatikana katika Bohari ya Dawa**. Ongezeko hili la upatikanaji wa dawa kutoka **asilimia 36** kipindi cha mwezi Juni 2016 na kufikia **asilimia 81** mwezi Machi, 2017 limetokana na uamuzi wa Serikali wa kuongeza bajeti ya dawa na kuhakikisha upatikanaji wa fedha kwa ajili ya dawa, vifaa, vifaa tiba, na vitendanishi. Aidha, katika kuboresha upatikanaji wa dawa, Wizara kupitia Bohari ya Dawa (MSD) imeanza kutekeleza mikakati mbalimbali ikiwemo **ununuzi wa dawa moja kwa moja kutoka kwa wazalishaji** kwa lengo la kupunguza gharama za dawa na kuongeza uwezo wa MSD kununua dawa nyingi zaidi ambapo Zabuni 6 za wazalishaji zimekamiliika. Kukamilika kwa zabuni hizi, kutawezesha upatikanaji wa dawa muhimu zaidi kutoka moja kwa moja kwa wazalishaji kwa asilimia 76. **Lengo la Wizara ni kuhakikisha hali ya upatikanaji wa dawa inafikia** asilimia 90 ifikapo mwishoni mwa mwaka wa fedha 2016/17.
59. **Mheshimiwa Spika**, kuimarika kwa hali ya upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba, na vitendanishi katika Bohari ya Dawa kumeongeza **upatikanaji wa dawa kwenye vituo vya umma vya kutolea huduma za Afya afya nchini**. Kwa mujibu wa takwimu zilizokusanywa kutoka katika Mikoa na Halmashauri mbalimbali nchini, hali ya upatikanaji wa dawa kwenye vituo inakadiriwa kuwa wastani wa **asilimia 83** kufikia mwishoni wa Machi 2017 (**Kiambatisho Na. 3**). Wizara itaendelea kukusanya taarifa za upatikanaji wa dawa kutoka Halmashauri na Mikoa kila mwezi ili kujiridhisha zaidi juu ya hali halisi ya upatikanaji wa dawa katika vituo vya kutolea huduma hasa ngazi ya zahanati na vituo vya afya. Hata hivyo, bado zipo changamoto mbalimbali katika upatikanaji wa dawa ikiwemo baadhi ya **Halmashauri /Hospitali**

kutowasilisha mahitaji yao ya dawa kwa wakati na hivyo kusababisha tatizo la upatikanaji wa dawa katika vituo. Vilevile, kuna usimamizi hafifu wa matumizi ya dawa, makusanyo na matumizi ya fedha zitokanazo na uchangiaji wa huduma za afya na matumizi ya mifumo na utunzaji taarifa za dawa na vifaa tiba. Wizara imejipanga kukabiliana na changamoto hizi kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI. Moja ya hatua tulizochukua ni kuamua kuwa kuanzia Julai 2017 fedha za dawa kupitia Mfuko wa Pamoja wa Afya (Health Basket Fund) zitapelekwa moja kwa moja kwenye vituo vya kutolea huduma. Nitumie fursa hii kuzitaka mamlaka za halmashauri na mikoa kuhakikisha wanasimamia fedha hizo ikiwemo makusanyo na matumizi ya fedha zitokanazo na uchangiaji wa huduma za afya sambamba na kutoa taarifa sahihi za hali ya upatikanaji wa dawa.

60. **Mheshimiwa Spika**, kwa kutambua changamoto zilizopo katika mfumo wa ugavi na usambazaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba, vitendanishi na chanjo nchini, Wizara imefanya mapitio ya mfumo (Holistic Supply Chain Review) kwa lengo la kuandaa mpango mkakati wa utekelezaji ili kuwa na mfumo madhubuti wenye kukidhi mahitaji ya nchi.
61. **Mheshimiwa Spika**, Wizara pia imetekeleza ahadi ya **Mhe. Rais Dkt. John Pombe Magufuli** ya kuhakikisha kila kituo cha kutolea huduma za afya cha umma kinakuwa na vifaa vya kutosha. Katika mwaka 2016/17, **Wizara imenunua na kuanza kusambaza kwa kila Halmashauri vitanda vya kawaida 20, vitanda vya kujifungulia 5, magodoro 25 na mashuka 50**. Uzinduzi wa zoezi hili umefanyika mwezi Aprili 2017 katika halmashauri ya Kongwa Dodoma. Jumla ya vitanda vya kawaida (Hospital beds) 3,680, vitanda vya kujifungulia (delivery beds) 920, magodoro 4,600 na mashuka 9,200 vimenunuliwa ambapo thamani yake ni **Shilingi 2,933,125,600.00**
62. **Mheshimiwa Spika**, **Usugu wa dawa** aina ya antibiotiki ni tatizo kubwa ambalo linaikabili dunia kwa sasa. Hali ya Dunia ya utumiaji wa dawa aina ya antibiotiki kwa mwaka 2015 inaonyesha kwamba

matumizi ya dawa hizo kwa ukuzaji wa kuku, ng'ombe na nguruwe, husababisha Usugu wa dawa kwa vimelea vya bakteria ambavyo vinaenea kwa binadamu. Aidha, utafiti uliofanyika hapa nchini umeonesha kuongezeka kwa usugu wa dawa za antibiotiki katika kutibu magonjwa ya kuambukiza kwa binadamu, wanyama na mazingira.

63. **Mheshimiwa Spika**, Katika kupambana na usugu wa dawa hizo, Serikali imeitikia tamko la Mkutano Mkuu wa 68 wa Shirika la Afya Duniani uliofanyika mwaka 2015 ambapo nchi Wanachama walikubaliana kufanya juhudi za dhati za kupambana na usugu wa dawa hizo. Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, Mifugo na uvuvi na Wadau wengine imeandaa mpango wa miaka mitano wa kupambana na usugu wa dawa hizo kwa binadamu, mifugo na kilimo. Mpango huu umekamilika na kuzinduliwa mwezi Aprili, 2017.
64. **Mheshimiwa Spika**, Mpango huo pamoja na mambo mengine umelenga kuhamasisha na kuelimisha wataalam wa afya na wananchi kwa ujumla juu ya madhara yatokanayo na utumiaji wa dawa za antibiotiki usio sahihi kwa binadamu, mifugo na kwenye kilimo na jinsi ya kutatua changamoto hizo. Aidha, Wizara itaendelea kusimamia utumiaji ulio sahihi wa dawa aina ya antibiotiki hasa kwa kufuata sheria na kanuni zilizowekwa na inapobidi kuandaa sheria mpya; Kuzuia maambukizi ya vimelea vya bakteria kwa kuzingatia usafi wa mazingira hasa sehemu za kutolea huduma na katika kukuza mifugo.

Uimarishaji wa Huduma za Matibabu ya kibingwa

65. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/17, moja ya jukumu la kipaumbele kwa Wizara ilikuwa ni kuendelea kuboresha na kuimarisha huduma za kibingwa zitolewazo nchini. Maboresho hayo, yanalenga katika kupunguza idadi ya wagonjwa wanaopewa rufaa ya Matibabu nje ya nchi ili kupunguza gharama kubwa ambazo serikali inaingia katika kupeleka wagonjwa nje ya nchi. Hadi kufikia Machi 2017, **idadi ya Wagonjwa waliopewa rufaa ya**

Matibabu nje ya nchi ilipungua kwa asilimia 35 kutoka wagonjwa **553** mwaka 2015/16 hadi Wagonjwa **357** mwaka **2016/17**. Mafanikio haya ni kutokana na maboresho yaliyofanyika katika Hospitali zilizo chini ya Wizara zinazotoa huduma za Kibingwa ambazo ni Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI), MOI na Ocean Road. Takwimu za mwaka 2016/17 zinaonyesha kuwa magonjwa yanayoongozwa kwa rufaa nje ya nchi ni Saratani (36%), Moyo (17%), Masikio, pua na koo (15%), mishipa ya fahamu (8%), mifupa (4%) na mengineyo (5%).

Hospitali ya Taifa Muhimbili

66. **Mheshimiwa Spika**, Kwa kipindi cha Julai 2016 hadi Machi 2017, **Hospitali ya Taifa Muhimbili** imewahudumia jumla ya wagonjwa wa nje 317,660 ikilinganishwa na wagonjwa 357,343 waliopatiwa huduma mwaka 2015/16. Aidha, hospitali ilihudumia jumla ya wagonjwa waliolazwa 39,418 ikilinganishwa na wagonjwa 51,698 mwaka 2015/16. Pia, ukusanyaji wa mapato ya Hospitali umeongezeka na kufikia kiasi cha **Shilingi 39,793,000,000** kwa kipindi cha Julai 2016 hadi Machi, 2017 ikilinganishwa na **Shilingi 30,145,000,000** zilizokusanywa katika kipindi kama hicho 2015/16 ikiwa ni sawa na ongezeko la **asilimia 32**.
67. **Mheshimiwa Spika**, Hospitali ya Taifa Muhimbili imeendelea kuchukua hatua mbalimbali zenye lengo la kuboresha utoaji wa huduma za kibingwa. Hatua hizo ni pamoja na kufanya ukarabati wa Wodi mbalimbali kwa lengo la kuongeza uwezo wa kuhudumia wagonjwa wengi, ambapo jumla ya wadi 5 za ICU zimefanyiwa ukarabati. **Ukarabati huo utaoongeza vitanda vya ICU kutoka 21 na kufikia 75**. Aidha, mashine **14** za upasuaji (Diathermy Machines), mashine kubwa mbili (**2**) za utakasishaji vifaa zenye thamani ya **Shilingi milioni 717.6** zimenunuliwa. Vilevile, Hospitali imenunua mashine ya **CT-Scan** mpya yenye uwezo wa "slice" **128**, ambayo imegharimu **Shilingi bilioni 3.9**. Pia Hospitali imefanya ukarabati wa mashine za *ventilators, monitors na*

anaesthesia kwa jumla ya **Shilingi milioni 213**. Hospitali imeanza kukarabati jengo kuu la upasuaji wa kina mama wajawazito na jengo la upasuaji wa watoto; ukarabati huo utaongeza vyumba vya upasuaji **6** na kufanya Hospitali iwe na jumla ya vyumba **19**. **Upanuzi wa jengo la kusafisha figo** unafanyika ambao utaongeza vitanda **27** na kufikia jumla ya vitanda **42** ambapo jumla ya **Shilingi bilioni 1.02** zitatumika. Aidha, Hospitali ya Taifa ya Muhimbili imepeleka jumla ya wataalamu saba (7) nchini India kwa ajili ya mafunzo ya upandikizaji wa vifaa vya kusaidia kusikia (Cochlear Implants) kwa wagonjwa wenye matatizo ya kusikia. Jumla ya **Shilingi milioni 75.8** zimetumika katika mafunzo haya. Vilevile katika kuhakikisha upatikanaji wa huduma za kubadilisha figo nchini, wataalamu ishirini (20) wakiwemo Madaktari, Wauguzi, Wataalamu wa Maabara wamepatiwa mafunzo nchini India kwa gharama ya **Shilingi milioni 700**.

68. *Mheshimiwa Spika*, Hospitali ya Taifa ya Muhimbil pia imepanua sehemu ya kutoa huduma za dharura ili kuendana na ongezeko la wagonjwa sambamba na kuwa na sehemu ya dharura kwa ajili ya watoto. Upanuzi huo umeshakamilika kwa asilimia **60** na utagharimu **Shilingi bilioni 1**. Aidha, Hospitali imekarabati Wadi ya Sewahaji namba 18 kwa ajili ya wagonjwa wa kulipia yenye vitanda 13 kwa kutumia **Shilingi milioni 250 ambazo zimetokana na** vyanzo vya ndani. Aidha, upatikanaji wa Dawa katika Hospitali ya Taifa Muhimbili umeongezeka na kufikia zaidi ya asilimia **95**. Vilevile Hospitali imeanzisha mfuko wa fedha za kununulia dawa (**Revolving Fund**) ambao sasa umefikia **Shilingi 1,000,000,000** inayolipwa kila mwezi ili kukabiliana na changamoto za upatikanaji wa dawa.

69. *Mheshimiwa Spika*, Hospitali kwa kushirikiana na Mpango wa Damu Salama ilianzisha huduma za kuchangia damu katika jamii zoezi ambalo limepunguza kwa kiasi kikubwa sana ukosefu wa damu Hospitalini. Hospitali imeanzisha mpango wa uchunguzi na tiba kwa ugonjwa sugu wa homa ya ini ambao utatoa fursa kwa wataanzania kupata huduma hiyo. Mpango huo utawezesha vituo vingine kujifunza na kuweza kutoa huduma hiyo.

Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI)

70. **Mheshimiwa Spika**, Kwa kipindi cha Julai 2016 hadi Machi 2017 **Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI)** imewahudumia jumla ya wagonjwa wa nje 119,580 ikilinganishwa na wagonjwa 79,927 waliopatiwa huduma mwaka 2015/2016. Aidha, hospitali ilihudumia jumla ya wagonjwa waliolazwa 6,830 ikilinganishwa na wagonjwa 8,355 mwaka 2015/2016. Pia, kutokana na matumizi ya mfumo wa kieletroniki (HMIS) ukusanyaji wa mapato, umeongezeka kwa asilimia 8.5 na **kufikia Shilingi 6,707,172,559.43 kwa kipindi cha Julai 2016 hadi Februari, 2017** ikilinganishwa na Shilingi **6,134,667,970.65** zilizokusanywa katika kipindi kama hicho 2015/16.
71. **Mheshimiwa Spika**, Taasisi ya MOI imeendelea na juhudi za kupanua wigo wa huduma za kibingwa ambapo katika kipindi cha Julai 2016 - Machi 2017, imeanza kutoa huduma ya upasuaji wa migongo ya watoto iliyopinda (paediatric scoliotic spine correction) ikishirikiana na *Centre of Disease Excellence in Orthopaedics (COEDN)* ya Marekani pamoja na kuanzisha mafunzo ya upasuaji huo. Aidha, Taasisi hiyo imetoa huduma za upasuaji mkubwa kwa wagonjwa 496, wakijumuisha wagonjwa 67 waliofanyiwa upasuaji wa nyonga, 62 mgongo, 55 Ubongo, 262 watoto wenye vichwa vikubwa na 50 watoto wenye mgongo wazi.
72. **Mheshimiwa Spika**, Taasisi ya MOI kwa kushirikiana na GSM Foundation imetoa huduma ya upasuaji wa vichwa vikubwa na mgongo wazi kwa watoto kupitia kambi Tiba katika mikoa 18 ya Tanzania Bara na hospitali ya Mnazi Mmoja – Zanzibar. Katika kipindi cha Julai 2016 hadi Machi 2017, jumla ya watoto **2,200 walifanyiwa uchunguzi na watoto 250 walifanyiwa upasuaji kwa mafanikio** na kutoa mafunzo kwa Madaktari wa upasuaji wa kawaida katika hospitali za rufaa za mikoa/kanda nchini. Kwa sasa Taasisi ipo kwenye mpango wa kuchukua madaktari wa upasuaji toka hospitali husika kuja Dar es Salaam kujifunza zaidi upasuaji huo. Aidha, Taasisi kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Weil

Cornel na California San Francisco vya Marekani, inafanya utafiti wa kuboresha matibabu kwa wagonjwa wa ajali ya Kichwa, mfupa wa paja na Ugoko.

Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI)

- 73. Mheshimiwa Spika**, kwa kipindi cha Julai 2016 hadi 2017, Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKC) imewahudumia jumla ya wagonjwa wa moyo wanaotibiwa na kurudi nyumbani **37,199** ikilinganishwa na wagonjwa **24,570** waliopatiwa huduma hiyo mwaka 2015/16. Taasisi ilifanya upasuaji wa moyo kwa wagonjwa **236** kwa gharama ya **Shilingi 1,555,500,000.00** ambapo kama upasuaji huo ungefanyika India ungegharimu takribani **Shilingi 5,307,000,000.00**, hivyo kuokoa kiasi cha **Shilingi 3,751,500,000.00**. Idadi hii ni sawa na **wastani wa wagonjwa 30 kwa mwezi**, ikiwa ni ongezeko la asilimia 100 ukilinganisha na **wastani wa wagonjwa 15 kwa mwezi** katika mwaka wa fedha 2015/16. Kati ya wagonjwa 236 waliofanyiwa upasuaji, watu wazima walikuwa 74 wakati watoto walikuwa 162. Asilimia 49 ya wagonjwa walifanyiwa upasuaji na madaktari wa JKCI na asilimia 51 walifanyiwa kwa kushirikiana na madaktari kutoka nje ya nchi kupitia kambi za upasuaji wa pamoja. Aidha jumla ya **wagonjwa 608** walipatiwa matibabu maalum kupitia **tundu dogo kwa kutumia mtambo wa kisasa - catheterization laboratory** (stents, percutaneous intervention, device closure, pacemaker). Idadi hii ni ongezeko la **asilimia 190** ukilinganisha na **wagonjwa 290 waliohudumiwa katika mwaka wa fedha 2015/16**. Kati ya wagonjwa hao, **asilimia 82.6** walikuwa watu wazima na **asilimia 17.4** walikuwa watoto. **Asilimia 89** ya huduma ya matibabu maalum ya moyo kwa kutumia mtambo wa kisasa – *catheterization laboratory* zimefanywa na madaktari wa Taasisi na **asilimia 11** zilifanywa kwa kushirikiana na wataalam kutoka nje ya nchi.
- 74. Mheshimiwa Spika**, Vilevile, JKCI ilifanya kambi 3 za upasuaji kwa kushirikiana na mataifa rafiki (Israel, Germany na Australia). Hatua hiyo imesaidia kujenga uwezo wa madaktari wazawa kwa kupata utaalum wa kupasua wagonjwa kutumia tundu dogo (hii

inasaidia wagonjwa kuona mapema na kuruhusiwa kurudi nyumbani ndani ya siku chache). Vilevile, **JKCI** kwa kushirikiana na Wizara imeweza kupeleka madaktari 9 kwenye masomo ya juu katika fani ya moyo (2 Afrika ya Kusini, 2 Israel, 1 India, 1 China na 3 MUHAS). Pia imeweza kuchapisha matokeo ya chunguzi zake kwenye majarida ya kimataifa machapisho 3 (3 peer reviewed publications).

Taasisi ya Saratani Ocean Road

75. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017, **Taasisi ya Saratani Ocean Road** iliendelea kutoa huduma za uchunguzi, matibabu, kinga, mafunzo na utafiti wa saratani. Katika kipindi hicho, Taasisi imehudumia jumla ya wagonjwa **19,244** ambapo **3,982** ni wagonjwa wapya wa Saratani, **13,109** ni wagonjwa wa marudio wa saratani, na **2,133** ni wagonjwa wasio wa saratani ikilinganishwa na wagonjwa 31,075 walipatiwa huduma na Taasisi katika mwaka 2015/16. Aidha, jumla ya wanawake **6,717** walifanyiwa uchunguzi wa awali wa saratani ya mlango wa kizazi na matiti na wanaume **534** walifanyiwa uchunguzi wa saratani ya tezi dume. Katika uchunguzi huo, jumla ya wanawake **451** waligunduliwa kuwa na dalili za awali za saratani ya mlango wa kizazi na **267** walikutwa na dalili za saratani ya matiti. Vilevile, wananchi **1,204** walifanyiwa uchunguzi wa saratani ya mlango wa kizazi, saratani ya matiti na saratani ya tezi dume katika kampeni ya mkoa wa Dar es Salaam iliyofanyika katika Viwanja vya Mnazi Mmoja pamoja iliyofanyika kwa Waheshimiwa wabunge, Dodoma mwezi Februari 2017.
76. **Mheshimiwa Spika**, Taasisi iliendelea kutoa huduma za mkoba katika mikoa mbalimbali ambapo jumla ya wagonjwa **3,215** walipatiwa matibabu na rufaa kufuatana na mwongozo wa huduma. Aidha, jumla ya wananchi **16,433** walifanyiwa upimaji wa saratani katika mashirika mbalimbali ya serikali na yasiyo ya kiserikali katika huduma ya elimu na upimaji. Vilevile, Taasisi kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi cha Muhimbili (MUHAS) iliendelea kutoa mafunzo kwa wanafunzi **43**

wa Shahada ya Kwanza ya Tiba ya Saratani kwa Mionzi na wanafunzi **17** wa Shahada ya Uzamili katika Sayansi ya Tiba ya Saratani. Wanafunzi **2** walihitimu Shahada ya Uzamili katika Sayansi ya Tiba ya Saratani na wanafunzi **3** Shahada ya Kwanza ya Tiba ya Saratani kwa Mionzi. Pia, Taasisi imeendelea kushirikiana na wadau wa ndani na nje katika utafiti wa Saratani na katika kipindi husika jumla ya machapisho **matatu (3)** yalichapishwa katika majarida ya kisayansi duniani (peer-reviewed journals).

- 77. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/17, **Taasisi ya Saratani Ocean Road** imekamilisha ukarabati wa jengo la kutolea tiba ya dawa (chemotherapy) pamoja na kununua vifaa na vitanda ambapo idadi ya wagonjwa wanaohudumiwa imeongezeka kutoka wastani wa wagonjwa **40** hadi kufikia wagonjwa **100** kwa wakati mmoja. Aidha, Taasisi **imeweza kupunguza muda wa kusubiri kuanza tiba za mionzi (radiotherapy) kutoka miezi 3 hadi wiki 6**; kwa kuhakikisha wagonjwa wanapata tiba mara mbili kwa wiki na kufanya matengenezo ya mashine kwa haraka. Lengo la Wiraza ni kupunguza muda huo uwe **chini ya wiki 2** pindi mashine mpya za LINAC zitakaposimikwa.
- 78. Mheshimiwa Spika**, upatikanajii wa dawa za saratani umeboreshwa kutoka **asilimia 4** mwaka 2015/16 hadi kufikia **asilimia 60** mwezi Machi, 2017; na kwa baadhi ya saratani kama ya mlango wa kizazi, saratani ya koo, tezi dume na dawa za dripu (chemotherapy) zinapatikana kwa **asilimia 100**. Aidha, upatikanajii wa dawa za mionzi hasa *radioactive iodine* kwa sasa zinapatikana kwa **asilimia 100** na ununuzi wa dawa hizo unafanywa kutoka kiwandani nchini Afrika Kusini kupitia MSD. Taasisi imeanzisha duka la dawa la jamii ambalo limeongeza wigo wa upatikanajii wa dawa kwa wagonjwa na hasa wale wa Bima na kuongeza mapato ya dawa kutoka **Milioni 30 kwa mwezi** hadi kufikia **Milioni 700 kwa mwezi**.
- 79. Mheshimiwa Spika**, **Taasisi ya Saratani Ocean Road** ilikamilisha ujenzi wa jengo la 'bunker' ambapo mashine za mionzi

za *LINAC* pamoja na *CT Simulator* zitasimikwa. Aidha, Taasisi inakamilisha taratibu za manunuzi ili kununua mashine hizo ambazo zinategemewa kusimikwa mwezi Juni 2017.

Hospitali ya Rufaa Benjamin Mkapa - DODOMA

- 80. *Mheshimiwa Spika***, kwa kipindi cha Julai 2016 hadi Machi 2017, **Hospitali ya Rufaa Benjamin Mkapa** ilihudumia jumla ya wagonjwa 21,662 ambapo wagonjwa wa nje walikuwa 20,812 na waliolazwa 850 ikilinganishwa na wagojwa 6,450 waliohudumiwa mwaka 2015/2016. Aidha, uchunguzi wa matibabu ya Macho kwa ushirikiano na timu ya wataalamu kutoka Marekani ulifanyika katika Hospitali kwa wagonjwa 3,500 na kati ya hao wagonjwa 500 walifanyiwa upasuaji na waliobaki walipata matibabu mengine ikiwemo utoaji wa miwani na ushuri mbalimbali. Vilevile, kulifanyika huduma za uchunguzi wa figo mwezi Machi 2017 ambapo wagonjwa 754 walichunguzwa na kupewa ushuri. Pia, Hospitali imekabidhiwa gari la kubebea wagonjwa na Wizara ili kukidhi mahitaji ya huduma kwa wagonjwa.
- 81. *Mheshimiwa Spika***, katika kuendeleza na kuboresha utoaji wa huduma za afya, Hospitali imefunga mitambo ya Uchunguzi wa magonjwa mbalimbali kama vile MRI, CT-Scan, Mammography, General Purpose X-ray, Fluoroscopy, Ultrasound na Dental Unit and Dental X-ray machine. Huduma zitaanza kutolewa baada ya Tume ya Taifa ya Mionzi kutoa leseni. Aidha, hospitali ipo katika hatua za mwisho za ukamilishwaji wa maabara ya kisasa *Cath-lab* kwa ajili ya matibabu ya moyo pamoja na Maabara yenye uwezo wa kuchunguza vinasaba ambapo hadi mwezi Machi 2017 baadhi ya vifaa vimenunuliwa ikiwemo DNA, Analyser, Dignator PCR na Conventional PCR. Vilevile, hospitali imeboresha na kuimarisha miundombinu ya kutolea huduma za afya katika Wodi za wagonjwa, jengo la huduma za kinywa na Meno, Vyumba vya upasuaji na Chumba cha Wagonjwa mahututi.

Hospitali ya Mirembe

82. **Mheshimiwa Spika**, Kwa kipindi cha Julai 2016 hadi Machi 2017 **Hospitali ya Mirembe** ilihudumia jumla ya wagonjwa wa akili 2,111 kati yao wanaume 1,511 na wanawake 600 na pia ilihudumia wagonjwa wa magonjwa ya kawaida 364. Aidha, hospitali ilihudumia wagonjwa wa akili wa kutibiwa na kuondoka 8,363 ambao kati yao wanaume walikua 3,023 na wanawake 5,340. Wagonjwa wa magonjwa mengine 12,633 walihudumiwa katika mwaka 2016/17; ikilinganishwa na wagonjwa 33,900 waliopewa huduma mwaka 2015/2016.
83. **Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai ya mwaka 2002 na Sheria ya Afya ya Akili ya mwaka 2008, **Hospitali** ilihudumia jumla ya wagonjwa wa akili wahalifu 374 waliopokelewa katika Taasisi ya Isanga ambapo wanaume walikuwa 297 na wanawake 77. Aidha, Hospitali iliandaa ripoti za kisheria kwa wagonjwa wa akili wahalifu 75 ambao walihisiwa kutenda makosa wakati wakiwa na ugonjwa wa akili, kati yao wanaume 66 na wanawake 9. Wagonjwa hao walichunguzwa na taarifa za kitaalamu zilitumwa katika Mahakama Kuu na Mahakama za Wilaya ili kuzisaidia katika kufikia maamuzi ya kisheria. Taasisi pia, ilipokea hati za ruhusa kwa wagonjwa 62 wa kundi maalum (Category C) wakiwemo wanaume 53 na wanawake 9. Wagonjwa hao ni wale waliopona na kumaliza muda wao wa matibabu wa miaka 3 kwa mujibu wa Sheria.

Hospitali Maalumu ya Kibong'oto

84. **Mheshimiwa Spika**, Kwa kipindi cha Julai 2016 hadi Machi 2017, **Hospitali** iliendelea kutoa huduma kwa wagonjwa **18,441** wa nje na kati ya hao wagonjwa wa Kifua Kikuu na UKIMWI ni **283**, Kifua Kikuu Sugu waliolazwa **112**, Kifua Kikuu cha kawaida **159** na wagonjwa 17,887 wa magonjwa mengine ikilinganishwa na wagojwa **22,348** kwa mwaka 2015/2016. Katika kufuatilia mwenendo wa magonjwa ya kuambukiza, Hospitali imeweza kupima sampuli za makohozi kwa wagonjwa 1,961 na kupata

wagonjwa 367 (asilimia 33.5) na kati yao wagonjwa 30 walikuwa na Kifua Kikuu Sugu. Aidha hospitali imepata mashine ya kupima usugu wa vimelea vya Kifua Kikuu kwa dawa daraja la pili (Secondline anti tuberculosis drug susceptibility testing) na kupunguza muda wa uchunguzi wa Kifua Kikuu Sugu Zaidi (Extensive drug Resistant TB) chini ya siku 90.

85. Mheshimiwa Spika, Hospitali pia iliendelea kutoa elimu kwa watoa huduma kutoka Hospitali mbalimbali nchini kwa lengo la kuwajengea uwezo wa kuanzisha matibabu ya Kifua Kikuu Sugu nchini. Vituo **19** katika Mikoa **14** wamejengewa uwezo wa kutibu wagonjwa na kuwafuatilia matibabu. **Kwa hivi sasa hospitali imeweza kufupisha muda wa kuanza Tiba kutoka siku 14 mpaka siku 3 tangu mgonjwa kugundulika kuwa na kifua Kikuu Sugu hivyo kupunguza maambukizi kwa jamii.** Aidha, Hospitali ilifanya tafiti mbalimbali za kusaidia kujua changamoto zinazoikabili sekta ya afya katika mfumo mzima wa ugunduzi na tiba ya Kifua Kikuu na UKIMWI kwa kushirikiana na taasisi za utafiti nchini na nchi za nje. Vilevile, Hospitali imechapisha machapisho matatu ya kisayansi kifua kikuu na kifua kikuu sugu.

86. Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa bajeti ya 2016/17, **Hospitali ya Kibong'oto** kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Nelson Mandela imeandaa andiko la kuanzisha mafunzo ya shahada za uzamili na uzamivu katika magonjwa ya kuambukiza ikiwa na lengo la kuongeza wataalam wabobezi wenye uwezo wa ugunduzi wa vipimo kwa magonjwa haya nchini. Kwa makubaliano hayo wafanyakazi wawili (Madaktari; 1 shahada ya uzamivu na 1 shahada ya uzamili) wamejiunga na Chuo cha Nelson Mandela kusomea Sayansi ya Magonjwa ya Kuambukiza.

Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini (Mbeya)

87. Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha Julai 2016 hadi Machi 2017 **Hospitali ya Rufaa ya Kanda - Mbeya** imewahudumia jumla ya wagonjwa wa nje **175,478** ikilinganishwa na wagonjwa 198,219

waliopatiwa huduma mwaka 2015/2016. Aidha, Hospitali ilihudumia jumla ya wagonjwa waliolazwa **24,927** ikilinganishwa na wagonjwa **29,162** mwaka 2015/2016.

- 88. Mheshimiwa Spika, Hospitali** imeendelea kuimarisha huduma za kibingwa, ambapo hadi kufikia Machi 2017, jumla ya wagonjwa 37 walifanyiwa upasuaji kwa kutumia tundu dogo. Aidha, Hospitali kwa kushirikiana na Taasisi ya Mifupa Muhimbili imefanya upasuaji kwa watoto wenye matatizo ya mgongo wazi na vichwa vikubwa. Jumla ya Wagonjwa 10 wamewekewa *Arteriovenous Fistula* kwa ajili ya kuchujia damu (*dialysis*).
- 89. Mheshimiwa Spika, Hospitali** imeendelea kuboresha na kupanua wigo wa huduma zinazotolewa kwa kukarabati jengo la daraja la kwanza na **kukamilisha ujenzi wa jengo la watoto**. Kukamilika kwa jengo jipya la Idara ya Watoto kutatoa nafasi kwa Idara ya upasuaji (mifupa na ajali, njia ya mkojo na tezi dume pamoja na upasuaji wa jumla) na hivyo kumaliza tatizo la wagonjwa kulala chini. Kukamilika kwa miradi hiyo miwili kutaongeza uwezo kwa hospitali kutoka **vitanda 477 vya sasa mpaka vitanda 605**.
- 90. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2016/17, Hospitali imeanzisha idara ya matibabu ya pua, koo na masikio (ENT)** na hivyo kuwaondolea wananchi mzigo wa kusafiri kufuata huduma hizo katika Hospitali ya Taifa Muhimbili. Hadi kufikia mwezi Machi 2017 wagonjwa 883 wenye matatizo ya pua, koo na masikio wamehudumiwa. Aidha, Idara ya Mifupa imeimarishwa baada ya kupata vifaa kama *sign nails sets* hivyo kupunguza sana muda wa wagonjwa walio vunjika kukaa wodini ambapo kwa sasa mgonjwa hukaa wodini kwa muda wa chini ya siku tatu ikilinganishwa na siku 42 ilivyokuwa hapo awali. Vilevile, Huduma ya kusafisha figo (*dialysis*) imeimarishwa kwa kununua vitanda vipya 3 na hivyo kufikisha idadi ya vitanda 6. Pia, hospitali imepata mashine za kisasa za maabara (*cobas machine*), *histopathology* na mashine ya kutolea dawa ya usingizi, vyote vikiwa na thamani ya **Shilingi milioni 340**, pamoja na kununua mashine ya vipimo vya damu (*Hematology*) kupitia fedha zake za ndani iliyogharimu kiasi cha

Shilingi milion 57. Aidha, ujenzi wa jengo la radiologia unaendelea ambapo tayari **Shilingi bilioni 1.5** zimepokelewa kutoka Hazina na mkandarasi atakayetekeleza kazi hiyo ameshapatikana.

Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Ziwa - Bugando

- 91. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai 2016 hadi Machi 2017, **Hospitali ya Bugando** iliwahudumia jumla ya wagonjwa 117,992 ambapo wagonjwa wa nje walikuwa 89,091 na waliolazwa walikuwa 28,901 ikilinganishwa na wagonjwa 327,080 mwaka 2015/2016. Hospitali pia imeendelea kutoa huduma za kifua na moyo ambapo jumla ya wagonjwa 1,347 walihudumiwa na 26 walifanyiwa upasuaji mkubwa. Aidha, **huduma za moyo kwa watoto zimeanza kutolewa kuanzia mwezi Januari 2017** na hadi sasa watoto 250 wamepata huduma hizo. Hospitali imetoa huduma kwa **akinamama 174 wenye fistula**. Vilevile, Hospitali imeendelea na ukarabati wa miundombinu ya kutolea huduma ikiwa ni pamoja na kliniki za wagonjwa wa nje, jengo la Saratani, na kukamilisha ujenzi wa kliniki za wanachama wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya.
- 92. Mheshimiwa Spika,** Hospitali imekamilisha ufungaji wa CT-Scan simulator ambayo hutumika kupanga matibabu ya mionzi ya saratani. Huduma zitaanza kutolewa baada ya Tume ya Mionzi ya Taifa (TAEC) kutoa leseni. Kukamilika kwa usimikaji wa mitambo hiyo na kuanza kutolewa kwa matibabu ya saratani kwa njia ya mionzi itakuwa ni ukombozi na faraja kubwa kwa wagonjwa wa saratani wa Kanda ya Ziwa ambao wamekuwa wakilazimika kusafiri hadi Dar es Salaam ili kupata huduma hiyo katika Taasisi ya Saratani Ocean Road. Hospitali ya Bugando pia imeweza **kuanzisha kituo cha kusafisha damu** (Haemodialysis Unit) ambacho kinaweza kutoa huduma kwa wagonjwa 10 kwa wakati mmoja. Kituo hiki ambacho kilianza mwezi Julai 2016 hadi sasa kimeweza kuhudumia wagonjwa 30 katika mizunguko (sessions) 2,107.

Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Kaskazini - KCMC

93. **Mheshimiwa Spika**, Kwa kipindi cha Julai 2016 hadi kufikia Machi 2017, **Hospitali ya KCMC** ilihudumia jumla ya wagonjwa 162,078 ikilinganishwa na wagonjwa 223,198 waliohudumiwa mwaka 2015/16. Hospitali kwa kushirikikiana na Taasisi za *Foundation for Cancer Care in Tanzania* (FCCT) na *Tanzania Cancer Care Foundation* (TCCF) ambao ni marafiki wa Shirika la Msamaria Mwema Tanzania imekamilisha ujenzi wa kituo cha tiba za saratani awamu ya kwanza kati ya nne. Awamu hiyo ilijumuisha ujenzi wa jengo la kliniki kwa ajili ya wagonjwa wa saratani na jengo la tiba ya dawa (Chemotherapy). Utoaji wa huduma katika kituo hiki umerahisisha upatikanaji wa matibabu ya saratani karibu na wananchi wa mikoa ya Tanga, Manyara, Singida, Arusha, na Kilimanjaro.
94. **Mheshimiwa Spika**, wagonjwa waliohudumiwa na kituo cha tiba za saratani ni 415, kati yao watu wazima walikuwa ni 367 (wanawake 189 na wanaume 178) na watoto ni 48. Watu wazima 160 na watoto 19 walikuwa wakiendelea na tiba ya dawa. Aidha Hospitali imekamilisha ujenzi wa Wodi mpya kwa ajili ya wagonjwa walioungua moto na kemikali. Wodi hizo zina uwezo wa kulaza wagonjwa 24 kwa wakati mmoja. Vilevile, **Kitengo cha ICU kwa ajili ya watoto kimefunguliwa tangu Oktoba 2016** ambapo hadi kufikia mwezi Machi 2017, jumla ya watoto 91 wamepata huduma. Hospitali pia imeanza kutoa **huduma za kusafisha figo tangu Desemba 2016** baada ya kufunga mashine nne za kusafisha figo. Kati ya Januari na Machi 2017, jumla ya wagonjwa 32 wameshapata huduma hii.

Usimamizi wa utoaji wa Huduma za Tiba Nchini

95. **Mheshimiwa Spika**, Wizara ikiwa na dhamana ya kusimamia utoaji wa huduma za afya nchini imeendelea kutoa miongozo na maelekezo yenye lengo la kuhakikisha utoaji wa huduma bora kwa wananchi unazingatiwa. Wizara kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI inaendelea kusisitiza kwa vituo vyote vya umma vya

kutolea huduma za afya nchini kuweka utaratibu mwepesi kwa wananchi kufikisha malalamiko yao pindi wanapoonna kwamba hawakupatiwa huduma za afya kwa kiwango stahiki. Aidha, Wizara imeendelea kupokea na kushughulikia malalamiko na kero za wananchi juu ya huduma zinazotolewa. Kwa kipindi cha Julai 2016 hadi Machi 2017 malalamiko kuhusu utoaji wa huduma kwa vituo binafsi na huduma kwa vituo vya Umma yalipokelewa na kupatiwa ufumbuzi. Vilevile **magari 10 ya wagonjwa** kutoka katika Serikali ya Qatar yalitolewa kwa hospitali mbalimbali nchini ili kuimarisha huduma za rufaa kwa wagonjwa.

96. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/17, Wizara pia imeendelea kuratibu utolewaji wa huduma ya matibabu bure kwa wazee. Katika kutekeleza azma hiyo, Halmashauri ziliendelea kuhimizwa kutenga fedha kwa ajili ya kulipia matibabu ya wazee kupitia Mfuko wa Afya ya Jamii na kuwanunulia dawa na vifaa tiba.

Huduma za Tiba Asili na Tiba Mbadala

97. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/17, Wizara imeendelea kutoa elimu kwa umma kupitia vyombo vya habari kuhusu Sheria ya Tiba Asili na Tiba Mbadala Na. 23 ya Mwaka 2002, kanuni zake na miongozo mbalimbali. Katika kutekeleza majukumu ya Kisheria, Wizara imeandaa na kuchapisha nakala 4,950 za mpango mkakati wa tiba asili na tiba mbadala **2016/17-2021/22**. Vitabu hivyo vitatoa msaada kwa waganga wakuu wa mikoa na Halmashauri kuweza kupanga mipango itakayo husu tiba asili na tiba mbadala katika maeneo yao. Aidha, Wizara inaendelea kuwakumbusha wamiliki wa vyombo vya habari kuzingatia Sheria ya Tiba Asili na Tiba Mbadala Na. 23 ya Mwaka 2002, kanuni zake katika utoaji wa matangazo ya Tiba Asili na Tiba Mbadala. Vilevile, Wizara iliratibu mafunzo kwa waganga 25 wa tiba asili yaliyofanyika mwezi Februari 2017 katika chuo kikuu cha MUHAS na wanachuo 44 katika Chuo Kikuu cha Kumbukumbu ya Sebastian Kolowa.

HUDUMA ZA UUGUZI NA UKUNGA

98. **Mheshimiwa Spika**, Katika kuhakikisha kuwa huduma za Uuguzi na Ukunga zinaimarika, Wizara imezindua Mpango Mkakati kwa ajili huduma za Uuguzi na Ukunga. Lengo la Mpango huo ni kutoa dira inayolenga katika kuboresha huduma za Uuguzi na Ukunga nchini. Aidha, Wizara imezindua mwongozo wa maabara ya mafunzo ya Uuguzi na Ukunga nchini, mwongozo huo unalenga katika kuboresha mafunzo ya vitendo yatolewayo katika vyuo vya uuguzi na ukunga, ili kuongeza weledi, maarifa, na stadi za kuhudumia wananchi kwa ubora zaidi. Katika kuimarisha umahiri kwa wauguzi na wakunga, Wizara imetayarisha na kuzindua mwongozo wa mafunzo sehemu za kazi kwa ajili ya kuwaongoza wakufunzi wa vitendo katika kusimamia mafunzo yatolewayo kwa wanafunzi sehemu za kazi. Vilevile, **Wizara imeendelea kuisitiza umuhimu wa kuzingatia maadili ya Uuguzi na Ukunga** kwa kutumia fursa mbalimbali ikiwa ni pamoja na kufanya usimamizi shirikishi, mikutano ya wauguzi na ile ya wasimamizi wao

UHAKIKI UBORA WA HUDUMA ZA AFYA

Uhakiki na Ukaguzi

99. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/17, Wizara imekamilisha zoezi la kufanya tathmini ya awali ya Vituo vya Kutolea Huduma za Afya ya msingi (Zahanati, Vituo vya Afya na Hospitali) katika Halmashauri zote za mikoa 6 iliyosalia ya Iringa, Njombe, Mbeya, Songwe, Kilimanjaro na Arusha. Vituo vilipewa hadhi ya nyota kulingana na ubora wa huduma zinazotolewa. Jumla ya vituo 1,665 vimefanyiwa tathmini, ambapo kati ya vituo hivyo, 446 (27%) vilipata nyota sifuri, 862 (52%) vilipata nyota moja, 272 (16.3%) vilipata nyota mbili, 63 (4%) vilipata nyota tatu na 2 (0.12%) vilipata nyota nne. Mipango ya Uimarishaji Ubora wa huduma za afya kwa kila Kituo iliandaliwa na utekelezaji unaendelea kwa kushirikiana na Timu za Uendeshaji Afya za Halmashauri. Aidha, katika utekelezaji na ufuatiliaji wa mipango ya uboreshaji wa

huduma za afya, Wizara ilitoa kiasi cha **3,040,000,000** katika mikoa 4 ambapo jumla ya vituo 304 (Dodoma 118, Kigoma 135, Singida 32 na Tanga 19) vilivyokuwa na nyota sifuri vilipatiwa Shilingi **10,000,000** kwa kila Kituo.

- 100. Mheshimiwa Spika**, Wizara ilifanya tathmini ya marudio kwa vituo 52 katika mkoa wa Shinyanga. Ukilinganisha matokeo ya awali na matokeo ya tathmini ya marudio, vituo vimeonyesha mabadiliko makubwa katika utekelezaji wa mipango ya uboreshaji wa huduma ambapo kati ya vituo 40 vilivyokuwa na nyota sifuri, ni vituo 3 tu (7.5%) ndivyo vimebaki katika hadhi ya nyota sifuri. Aidha, Wizara imefanya usimamizi shirikishi kwenye eneo la Kukinga na Kudhibiti Maambukizi (infectious, prevention and control) katika vituo vya kutolea huduma vya mikoa 21 (**Kiambatanisho Na.4**) ya Tanzania bara. Vilevile, Jitihada za Kukinga na Kudhibiti Maambukizi zimeimarishwa katika utoaji huduma za dharura na Maafa ili kuzuia kuenea kwa maambukizi wakati wa utoaji wa huduma hizo.

Dharura na Maafa

- 101. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/17, Wizara imetekeleza mikakati ya kujenga utayari wa kisekta wa kukabiliana na dharura kwa kuwapatia mafunzo ya kukabiliana na dharura na maafa timu za dharura katika mikoa 23 ya Dar es Salaam, Pwani, Morogoro, Dodoma, Singida, Manyara, Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Lindi, Mtwara, Mbeya, Iringa, Rukwa, Tabora, Kigoma, Kagera, Mwanza, Mara, Geita, Simiyu Shinyanga na Katavi ambapo jumla ya watoa huduma 120 walipata mafunzo hayo. Aidha, Wizara imeandaa na kuchapisha miongozo ya kutoa huduma za dharura pamoja na kufanya tathmini ya viashiria vya dharura “*Vulnerability Risk Assessment and Mapping*” kuhusu mlipuko wa ugonjwa wa kipindupindu nchini ili kusaidia kuimarisha mikakati ya kukabiliana na ugonjwa huo.
- 102. Mheshimiwa Spika**, Aidha, Wizara imeanza maandalizi ya kuanzisha huduma za dharura katika barabara kuu kutoka Dar es Salaam hadi mpaka wa Tanzania na Malawi, kwa kupitia mradi wa *South Africa Trade and Transport Facilitation (SATTF)*. Awamu ya

kwanza ya mradi huo utanzia Dar Es Salaam hadi mpakani mwa Morogoro na Iringa katika eneo la Ruaha Mbuyuni. Aidha, Wizara inashirikiana na wadau wa usalama barabarani kutekeleza mikakati ya kupunguza ajali za barabarani kwa kupitia Mradi wa “*Bloomberg Initiative for Road Safety (2015-2019)*”. Katika Mradi huo, Wizara inaratibu Wadau wa Usalama Barabarani, kuhamasisha uboreshaji wa sheria, utoaji wa taarifa za kuhamasisha masuala ya usalama barabarani na mafunzo ya kujenga uwezo kwa wanasheria na waandishi wa habari.

- 103. *Mheshimiwa Spika***, Wizara pia imeshiriki katika kukabiliana na dharura mbalimbali pamoja na kuratibu ushiriki wa wadau katika kukabiliana na dharura. Kwa kupitia kituo cha uratibu wa Operesheni za Dharura na Maafa, Wizara imeratibu utoaji wa huduma za afya katika dharura ikiwemo matukio ya tetemeko la ardhi mkoani Kagera, mlipuko wa magonjwa ya kipindupindu na sumu kuvu. Shughuli hizo zimefanyika kwa njia ya kutuma wataalamu, kupeleka dawa, vifaa na vifaa tiba na kuratibu mikutano ya wadau mbalimbali katika ngazi ya Taifa na Mkoa.

URATIBU, UFUATILIAJI NA UGHARAMIAJI HUDUMA ZA AFYA

Tathmini, Ufuatiliaji na Usimamizi wa huduma za Afya

- 104. *Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha ushirikishwaji wa wananchi na uwajibikaji katika kutekeleza vipaumbele vya Sekta ya Afya, Wizara imeendelea kufanya tathmini shirikishi kwa kutumia nyenzo ya kijamii (Community Score Card) ili kuongeza uwazi na uwajibikaji kwa lengo la kuboresha kiwango cha utoaji wa huduma za afya kwa wananchi. Tathmini hiyo imefanyika katika ngazi ya jamii inayohudumiwa na vituo vya afya 227 vya umma katika Halmashauri 14 (Mkoa wa Pwani halmashauri 8 na Kilimanjaro halmashauri 6). Matokeo ya tathmini hizo yametumika kuandaa mipango kabambe ya Halmashauri ya uboreshaji wa huduma za afya katika vituo vya kutolea huduma.

- 105. Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha dhana ya ushirikishwaji wa wananchi katika mipango na utawala bora katika sekta ya afya, Wizara kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI imefanya usimamizi shirikishi katika mikoa yote na kubaini uwepo wa Bodi za Usimamizi wa Huduma za Afya za Halmashauri katika Halmashauri 45 za mikoa ya Singida, Dodoma, Mbeya, Songwe, Tanga na Tabora ambazo hazifanyi kazi vizuri. Katika kuhakikisha Bodi hizo zinatekeleza majukumu yake ipasavyo, Wizara kupitia zoezi la usimamizi shirikishi ilitoa mafunzo elekezi, miongozo ya namna bora ya kutatua changamoto za usimamizi wa shughuli za afya za Halmashauri.
- 106. Mheshimiwa Spika,** Wizara pia imeendelea kuboresha upatikanaji wa takwimu za afya kutoka katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini. Uboreshaji huo unatokana na kuimarishwa kwa mfumo wa kielektroniki wa kutoa taarifa za vituo vya afya nchini yaani “Health Facility Registry” na uboreshaji wa mtandao wa kutoa taarifa za afya kupitia anuani ya hmisportal.moh.go.tz
- 107. Mheshimiwa Spika,** Wizara iliendelea kuimarisha mfumo wake wa Takwimu za kila siku katika kila kituo kinachotoa huduma za Afya unaoitwa “Mfumo wa Taarifa za Uendeshaji wa Huduma za Afya (MTUHA) na pia kusimamia mfumo wake wa kielektroniki unaoitwa “District Health Information System (DHIS2)”. Mfumo huu umezisaidia Halmashauri, Mikoa pamoja na ngazi ya Taifa katika kuchambua na kutumia taarifa hizo katika kuandaa mipango ya utoaji wa huduma za afya. Aidha, Wizara imeingiza Mafunzo ya MTUHA kwenye mitaala ya kufundishia katika Vyuo vya Mafunzo ya Afya Nchini.

TEKNOLOJIA YA HABARI NA MAWASILIANO

- 108. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuelekeza matumizi ya mifumo ya kielektroniki kwa taasisi zilizo chini yake ili kuondoa matumizi ya karatasi na kuimarisha taarifa za wagonjwa na mtoa huduma. Kupitia Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), Wizara imekamilisha kufunga mfumo wa kielektroniki wa hospitali

(paperless) ikiwa ni pamoja na kusimamia mapato katika Taasisi ya Mifupa Muhimbili, Hospitali za Mikoa za Singida na Tabora, usimikaji unaendelea katika Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete, Hospitali ya Kanda ya Rufaa ya Mbeya, Hospitali ya Taifa Muhimbili, Mirembe na Hospitali ya Kibong'oto.

109. *Mheshimiwa Spika*, Wizara kwa kushirikia na OR-TAMISEMI na wadau mbalimbali imetengeneza Mpango Mkakati wa uwekezaji katika mifumo ya TEHAMA (Investment Recommendation Plan), mpango huu umewezesha Serikali na Wadau kubaini maeneo ya uwekezaji. Pamoja na kuharakisha uunganishaji wa mifumo katika sekta ya Afya.

110. *Mheshimiwa Spika*, Katika mwaka 2016/17, Wizara imeendelea na utekelezaji wa Mkakati wa TEHAMA katika Sekta ya Afya (ehealth Strategy 2013-2018). Katika kipindi cha Julai 2016 hadi Machi 2017, Wizara imefanya tathmini ya mifumo ya kieletroniki iliyofungwa kwenye hospitali zote za rufaa katika ngazi ya Mkoa na hospitali za Wilaya ili kujua kama inakidhi miongozo na viwango vilivyotolewa na Wizara pamoja na Wakala ya Serikali Mtandao. Tathmini ilionyesha kuwa mifumo iliyopo inakidhi vigezo kwa kati ya asilimia 18 hadi 92. Kufuatia matokeo ya tathimini hiyo, Wizara ilielekeza kuwa, Mifumo ambayo haikufikia vigezo kwa asilimia 60 isitumike na ile iliyofikia zaidi ya asilimia 60 iboreshwe kufikia asilimia 100. Aidha, Wizara inakamilisha mfumo wa kupokea maoni ya wananchi juu ya ubora wa huduma zinazotolewa katika vituo vya Afya nchini, ambapo mgonjwa ataweza kutoa taarifa kupitia *code* namba *152*05#.

RASILIMALI WATU KATIKA SEKTA YA AFYA

111. *Mheshimiwa Spika*, Wizara imeendelea kusimamia na kuratibu uzalishaji wa wataalamu kutoka vyuoni ambao wameendelea kuwa nguzo muhimu ya utoaji huduma za afya nchini. Uzalishaji huu umeendelea kuimarika kutokana na ongezeko la wanafunzi watarajali wanaodahiliwa katika vyuo vya afya kutoka wanafunzi **13,002** mwaka 2015/16 hadi wanafunzi 13,632 mwaka 2016/17. **Serikali imevuka lengo la Mpango wa Maendeleo ya Afya ya**

Msingi (MMAM) la kudahili wanafunzi 10,000 waliotarajiwa kudahiliwa ifikapo mwaka 2017. Vilevile, kwa mwaka wa fedha 2016/17, Wizara inasimamia utoaji wa **mafunzo kwa vitendo (internship) kwa wahitimu 1,798** wa vyuo vikuu katika fani mbalimbali za afya ikiwemo madaktari (1,072), wafamasia (186), wauguzi (265), maafisa mazingira (46), Radiologia na Radiografia (9), na maabara (220). Wanafunzi hao wanatarajia kukamilisha mafunzo hayo mwezi Oktoba, 2017.

- 112. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea na jitihada za kupunguza uhaba wa wataalam wanaotoa huduma za kibingwa nchini kwa kutekeleza mpango wake wa **kugharamia masomo ya uzamili** kwa wataalamu 404 wa afya katika nyanja mbalimbali. Hadi Machi 2017, wanafunzi 387 walikuwa wanaendelea na masomo katika vyuo mbalimbali ndani ya nchi na wanafunzi 17 katika vyuo vya nje ya nchi.
- 113. Mheshimiwa Spika,** Aidha, Wizara inaendelea kuimarisha vyuo vyake vya Mafunzo kwa kuvifanyia ukarabati mkubwa pamoja na ujenzi wa majengo mapya. Katika mwaka 2016/17, vyuo **14** vimeboreshewa miundombinu yake kupitia ufadhili wa Mfuko wa Dunia (Global Fund) na kati ya hivyo vyuo 12 vimekamiliika na kukabidhiwa kwa watumiaji. Vyuo hivyo ni Lindi CATC, Songea CATC, Njombe NTC, PHI Iringa, Rukwa CATC, Mpanda CATC, Kigoma CATC, Musoma NTC, Nzega NTC, PHN Morogoro, Tanga NTC na Mtwara COTC. Vyuo viwili ambavyo havijakamilika ni Mirembe NTC na Mvumi TI ambavyo vinategemea kukamilika mwaka wa fedha 2017/18. Wizara pia imenunua vifaa vya Maabara za vitendo kwa ajili ya kufundishia kwa vyuo 10 vya utabibu, uuguzi na ukunga.
- 114. Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa kushirikiana na kituo cha kudhibiti magonjwa cha Marekani “Centre for Disease Control (CDC)” inatekeleza mpango wa uimarishaji mifumo ya huduma za Afya. Katika mwaka 2016/17, Wizara imejenga Kituo kipya cha Elimu kwa njia ya Masafa eneo la Mkundi Manispaa ya Morogoro kitakachoweza kutoa elimu kwa Kada za Afya. Kituo hicho

kitakuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi hadi 300 kwa wakati mmoja. Vilevile, Mpango huo wa uimarishaji mifumo ya huduma za Afya umewezesha kutoa ajira za mkataba kwa wauguzi (97) na Tabibu wasaidizi (95) ambao wamesambazwa kwenda kutoa huduma kwenye vituo vya Afya na Zahanati katika Halmashauri 40 hapa nchini.**(Kiambatisho Na. 5)**

115. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea na jitihada za kuajiri watumishi wa afya ambapo katika mwaka 2016/17, **kibali cha kuajiri madaktari 258 kimepatikana. Hatua hii itasaidia kupunguza pengo la watumishi hasa katika ngazi ya vituo, Hospitali za wilaya na mikoa.** Hata hivyo, Sekta ya afya bado inakabiliwa na upungufu wa watumishi wa afya, kwa takribani asilimia 49. Serikali inaendelea na jitihada mbalimbali za kuhakikisha upungufu huu unaisha ili kuhakikisha huduma bora za afya kwa wananchi wote zinapatikana hasa kwenye zahanati, vituo vya afya, Hospitali za Wilaya na Hospitali za Rufaa za Mikoa.

116. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2016/17, Wizara kwa kushirikiana na wadau wakiwemo Taasisi ya Benjamini Mkaipa imeendelea na awamu ya pili ya ujenzi wa nyumba **200** za watumishi katika Mikoa 9 ya Kigoma, Mwanza, Shinyanga, Geita, Kagera, Tanga, Manyara, Pwani na Simiyu. Chini ya udhamini wa Mfuko wa Dunia (Global Fund), Ujenzi wa nyumba **132** umekamilika na nyumba **68** ujenzi unaendelea. Kukamilika kwa nyumba hizo kutaongeza idadi ya nyumba za watumishi zilizojengwa kupitia mradi huu na kufika nyumba **480** katika maeneo yenye mazingira magumu.

UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO YA AFYA YA MSINGI

117. Mheshimiwa Spika, Serikali inakamilisha utekelezaji wa Mpango wa miaka kumi wa Maendeleo wa Afya ya Msingi unaokamilika mwaka 2017. Katika utekelezaji wa mpango huo, Vituo vya kutolea huduma vimeendelea kuongezeka kutoka jumla ya **vituo 5,172** mwaka 2005 na kufikia jumla ya vituo 7,232 mwaka 2016. Hii ni

ongezeko la **vituo 2,060** sawa na asilimia 40. Kati ya vituo vyote vilivyopo nchini, **vituo 5,414** sawa na asilimia 75 ni vya Serikali na 1,818 ni vya taasisi binafsi. Aidha kupitia MMAM, Serikali iliingia Mkataba na watoa huduma binafsi (Service Level Agreement) ili kupunguza ulazima wa Halmashauri kujenga vituo vipya vya huduma za afya sehemu ambazo kuna vituo binafsi. Katika makubaliano hayo jumla ya Halmashauri 39 zinatumiya hospitali teule.

- 118. Mheshimiwa Spika**, kutokana na kipindi cha utekelezaji wa MMAM kufikia ukingoni, Wizara imeanza maandalizi ya kufanya tathimini ya utekelezaji wa mpango huo ili kupima mafanikio na changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wake na kutoa mapendekezo ya namna bora ya kuandaa na kutekeleza mpango mwingine.

UGHARAMIAJI WA HUDUMA ZA AFYA NCHINI

- 119. Mheshimiwa Spika**, Utoaji wa huduma za afya nchini unasimamiwa na Sera ya Afya ya mwaka 2007. Sera hii ni ya muda mrefu hivyo katika mwaka 2016/17 Wizara ilifanya mapitio ya Sera na kubaini kuwa kuna maeneo mengi ya Sera ambayo yametekelezeka kwa ufanisi mkubwa na maeneo machache ambayo hayakutekelezeka kikamilifu. Kufuatia matokeo haya, Wizara imeanza maandalizi ya kutunga Sera mpya ya Afya itakayokidhi mabadiliko katika Sekta ya Afya. Maandalizi ya Sera hiyo yanatarajiwa kukamilika katika mwaka 2017/18. Maandalizi ya Sera hii yamekuwa shirikishi na nichukue fursa hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge na wadau wote kuendelea kutoa ushirikiano wa dhati kwa Wizara kwa kutoa maoni na ushauri katika ukamilishwaji wa Sera hiyo.
- 120. Mheshimiwa Spika**, Wizara pia ilikamilisha maandalizi ya Mkakati wa Ugharamiaji huduma za afya nchini. Lengo kuu la Mkakati huu ni kutafuta vyanzo mbalimbali vya uhakika vya kuongeza rasilimali fedha katika Sekta ya afya. Mkakati huo una maeneo mengi ya Kisera ambayo bado yanafanyiwa kazi na wadau kabla ya kuanza

kutekelezwa. Utekelezaji wa mkakati huu utasaidia kuimarisha upatikanaji wa Rasilimali Fedha katika Sekta ya Afya na kuwahakikishia wananchi upatikanaji wa huduma bora za Afya pindi wanapozihitaji hasa wananchi wasio na uwezo na wenye mahitaji maalum.

- 121. Mheshimiwa Spika**, kupitia Mfuko wa Bima ya Taifa ya Afya na kwa kushirikiana na Benki ya Ujerumani (KfW) inatekeleza Mpango wa NHIF/CHF kwa Wanawake Wajawazito na Watoto ujulikanao kama **Tumaini la Mama**. Mpango huo wenye lengo la kupunguza vifo vya akinamama na watoto ulianza kutekelezwa mwaka 2012 ambapo akina mama wajawazito hulipiwa kadi za NHIF/CHF ili kuwa na uhakika wa matibabu katika kipindi chote cha ujauzito na miezi sita baada ya kujifungua kwa mama na mtoto. Katika kipindi cha Julai 2016 hadi kufikia mwezi Machi 2017, wanawake **wajawazito 147,615 walijisajiliwa** na hivyo kufanya jumla ya wanufaika kufikia wanawake **572,576** katika mikoa ya **Mbeya, Tanga, Lindi, Mtwara na Songwe**.
- 122. Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI pamoja na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya imepanga kutekeleza mpango wa Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF) iliyoboreshwa ili kuhakikisha watanzania wanapata huduma bora na kwa urahisi kwa kuzingatia uwezo wa kifedha wa mwanachama. Kupitia mpango huo, mwanachama ataweza kupata huduma kutoka ngazi ya zahanati hadi ngazi ya mkoa bila kujali Kituo/Halmashauri alipojisajili tofauti na ilivyo sasa ambapo mwanachama wa CHF hupata huduma kutoka ngazi ya zahanati hadi ngazi ya Halmashauri aliyojisajili tu.
- 123. Mheshimiwa Spika**, ili kuongeza ufanisi, kupitia Mpango huu wa CHF iliyoboreshwa, Halmashauri zitabaki na jukumu la kutoa huduma (**service provider**) na Mfuko/NHIF utakuwa na jukumu la kuandikisha wanufaika, kukusanya fedha za wanachama na kulipa watoa huduma (**purchaser**). Aidha, katika kuimarisha ushirikishwaji wa wananchi, vikao vya kijiji vitapewa fursa ya kuteua maafisa watakaokuwa na jukumu la kusajili wanachama

na kuwahamasisha pamoja na kukusanya michango. Mpango huo utatekelezwa kwa kuanzia katika **halmashauri 50** za mikoa ya **Kagera, Mwanza, Singida, Mara, Tabora, Pwani, Ruvuma** na baadae utasambazwa katika mikoa yote nchini. Uzinduzi rasmi wa mpango huu unatarajiwa kufanyika katika mkoa wa Singida kabla ya mwisho wa fedha 2016/17. Nitoe rai kwa Waheshimiwa Wabunge, kwa nafasi zao na ushawishi mkubwa walionao katika jamii tunayoishi, kuendelea kuwaelimisha wananchi wote umuhimu wa kujiunga na bima ya afya ili waweze kupata huduma za tiba bila kikwazo cha fedha.

Uratibu wa Mfuko wa Pamoja wa Afya (Health Basket Fund)

- 124. Mheshimiwa Spika**, Wizara imekuwa na jukumu la kuratibu **Mfuko wa Pamoja wa Afya (Health Basket Fund)** ulioanzishwa mwaka 1996. Kupitia Sekretarieti ya Uratibu wa Mfuko, Vikao mbalimbali vya majadiliano kati ya Serikali na Wadau vimekuwa vikifanywa ikiwa ni pamoja na kutoa taarifa ya Serikali jinsi inavyotekeleza kazi zinazogharamiwa na fedha za Wadau. Kwa hivi sasa Mfuko huo unachangiwa na Wadau (7) ambao ni Denmark, Uswisi (SDC), Ireland, Canada, Benki ya Dunia, UNICEF na Korea Kusini. Wizara inaendelea na juhudi za kuwaleta pamoja wadau wengine zaidi ili wachangie katika Mfuko huo ili kuleta ufanisi na matokea makubwa katika utekelezaji wa miradi ya afya nchini.
- 125. Mheshimiwa Spika**, wanufaika wa Mfuko huu ni OR -TAMISEMI, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto (Idara kuu ya Afya), Mikoa na Halmashauri zote nchini. Fedha hizo hugawiwa kwa fomula kwa kuzingatia makubaliano kati ya Serikali na Wadau wanaochangia Mfuko. Asilimia 90 ya fedha zote hupelekwa katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa, asilimia 6 ya fedha hizo hutumika katika Wizara ya Afya kwa ajili ya masuala ya uratibu, usimamizi na ufuatiliaji wa utekelezaji wa masuala mbalimbali ya Kisera katika Sekta ya Afya. Aidha, asilimia 3 ya fedha hizo hupelekekwa katika Mikoa kwa ajili ya kugharamia ufuatiliaji katika ngazi za Mamlaka za Serikali za Mitaa na asilimia

1 ya fedha zote hupelekwa Makao Makuu ya OR– TAMISEMI kwa ajili ya kugharamia ufuatiliaji katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

- 126. Mheshimiwa Spika**, Hadi robo ya tatu ya mwaka wa fedha 2016/17, kiasi cha **Shilingi bilioni 88.8 kimepokelewa** kupitia Mfuko wa Pamoja wa Afya. Kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 5.6 zilipokelewa na Wizara ya Afya (Fungu 52), Shilingi milioni 865.1 zilipokelewa na OR-TAMISEMI, Shilingi bilioni 2.6 zilipokelewa na Mikoa na kiasi cha Shilingi bilioni 79.7 zilipokelewa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.** Fedha hizi hutumika kadiri ya Mkataba wa Makubaliano kati ya Serikali na Wadau wa Maendeleo, ambapo asilimia 33 ya fedha zinazopelekwa katika Halmashauri zinatakiwa kutumika kama nyongeza ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa dawa na asilimia 67 ni kwa ajili ya utekelezaji wa afua mbalimbali ambazo zinalenga kuboresha huduma za afya nchini ikiwa ni pamoja na kugharamia usambazaji na ufuatiliaji wa chanjo kwa kuimarisha mnyororo baridi (cold chain), uimarishaji wa huduma za dharura za mama na mtoto (CEmOC), udhibiti wa magonjwa yanayoambukiza na yasiyoambukiza pamoja na yale yasiyopewa kipaumbele na kuwajengea uwezo watoa huduma za afya.
- 127. Mheshimiwa Spika**, pamoja na kuzingatia vigezo vya usawa katika kugawanya fedha za Mfuko, muelekeo wa Wadau kwa sasa ni kutoa umuhimu kwa ufanisi katika utekelezaji wa kazi zilizokubaliwa ili kuongeza ufanisi katika kazi zinazokubaliwa. Na ili kuviwezesha vituo vya kutolea huduma za afya kupata fedha kwa wakati na kuweza kufanya maamuzi ya haraka ya kutumia fedha hizo kulingana na mahitaji ya kituo husika, Wizara imeandaa utaratibu wa kuwezesha fedha za Mfuko kutumwa moja kwa moja kwa vituo vya kutolea huduma za afya ili kuviwezesha vituo kununua dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi kulingana na mahitaji yao kwa haraka. Halmashauri zitabaki na jukumu la kusimamia na kufuatilia matumizi ya fedha hizo. Mheshimiwa Spika, ninapenda kutumia fursa hii kuwaomba waheshimiwa wabunge pia kufuatilia matumizi ya fedha hizi

UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO (FUNGU 53)

MAENDELEO YA JAMII

- 128. *Mheshimiwa Spika***, Sera ya Maendeleo ya Jamii ya 1996 inasisitiza ushiriki wa wananchi katika shughuli za maendeleo kwa kutumia rasilimali zinazowazunguka kuleta mabadiliko chanya katika jamii. Katika kutekeleza maelekezo hayo, Wizara katika kipindi cha 2016/17 iliendelea kuwezesha na kuratibu utekelezaji wa majukumu ya Maendeleo ya Jamii hususan katika kutoa hamasa kwa jamii kushiriki katika shughuli za maendeleo kupitia miongozo mbalimbali. Kazi zilizofanyika ni pamoja na kuandaa Mwongozo wa Ufuatiliaji na Tathmini wa shughuli za Maendeleo na Ustawi wa Jamii kwa ajili ya kuhakikisha shughuli za maendeleo na ustawi wa jamii zinatekelezwa kwa ufanisi na kuwanufaisha wananchi ipasavyo katika Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa na hivyo kuharakisha kufikiwa kwa malengo mbalimbali ya maendeleo. Kazi hii ilifanyika kwa kushirikiana na OR- TAMISEMI.
- 129. *Mheshimiwa Spika***, Wataalam wa Maendeleo ya Jamii ni muhimu wakatumika ipasavyo katika kufanikisha Malengo ya Sera mbalimbali za Maendeleo ya nchi yetu. Wataalamu hawa ni muhimu katika kuwanda wananchi kushiriki katika kupanga na kutekeleza programu za Kilimo, Elimu, Maji, Barabara, Afya, Mifugo na Hifadhi ya Mazingira. Wizara ina jukumu la kuandaa wataalam wa kada ya Maendeleo ya Jamii katika ngazi mbalimbali za elimu kupitia Vyuo 8 vya Mafunzo ya Taaluma ya Maendeleo ya Jamii na taasisi moja ambayo ni Taasisi ya Maendeleo Tengeru. Katika mwaka 2016/17, Wizara kupitia Vyuo hivi imeendelea kuzalisha wataalamu hao ambapo jumla ya wataalam 1,685 walihitimu na wanachuo 2,216 walidahiliwa katika ngazi za Astashahada, Stashahada, Shahada na Stashahada ya Uzamili.

Aidha, katika kuboresha utoaji wa mafunzo katika chuo cha Maendeleo ya Jamii Rungemba, Wizara imewezesha kukirejeshea

chuo eneo lenye ukubwa wa hekari 175 lililokuwa na mgogoro na wanakijiji wa Rungemba, ambapo jumla ya Shilingi milioni 193,384,000.00 zimelipwa kwa wananchi 39. Hatua hii inatoa fursa ya kuhifadhi eneo la chuo kwa ajili ya upanuzi.

MAENDELEO YA JINSIA

- 130. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/17, Wizara imeendelea kutekeleza afua mbalimbali kwa lengo la kufikia usawa wa jinsia na kuwawezesha wanawake nchini. Utekelezaji huo ulizingatia maeneo manne ya kipaumbele ambayo ni Uwezeshaji wanawake kiuchumi; Kuzuia na kutokomeza ukatili wa kijinsia ikiwemo Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto; Kuwawezesha wanawake kushiriki katika uongozi na ngazi za maamuzi; na uingizaji wa masuala ya jinsia katika sera, mikakati na mipango ya kisekta na kitaifa.

Uwezeshaji Wanawake kiuchumi

- 131. Mheshimiwa Spika**, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeendelea na jitihada za kuwawezesha wanawake kiuchumi kwa kuwapatia mikopo kupitia **Benki ya Wanawake Tanzania** na **Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake** ili waweze kushiriki na kunufaika na ukuaji wa pato la kaya na taifa sawa na wanaume.
- 132. Mheshimiwa Spika**, Kwa upande wa Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake, Wizara imeendelea kuratibu Mfuko huu kwa lengo la kuwawezesha wanawake wajasiriamali wadogo. Katika mwaka 2016/17, jumla ya **Shilingi milioni 156** zilikopeshwa kwa Halmashauri tano za Kisarawe, Busokelo, Gairo, Iringa Manispaa, Masasi na Mtwara vijijini kwa ajili ya kutoa mikopo kwa vikundi 61 vyenye wanawake wajasiriamali 658.
- 133. Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake unawafikia wanawake wengi, Wizara kwa kushirikiana na OR TAMISEMI imeendelea kuzihamasisha Halmashauri kuchangia asilimia tano (5%) ya mapato yao ya ndani katika Mfuko

huo. Katika kipindi cha Julai hadi Disemba 2016, jumla ya Halmashauri 147 zilichangia jumla ya **Shilingi 7,826,722,946**. Pamoja na kuongezeka kwa mwamko wa Halmashauri kuchangia katika Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake, Halmashauri 39 hazikuchangia. (**Kiambatisho Na. 6**) Napenda kutumia fursa hii kuzipongeza Halmashauri zote ambazo zimechangia katika Mfuko huu. Aidha, natoa wito kwa Halmashauri ambazo hazijachangia zichangie Mfuko huu ili kuharakisha kufikiwa kwa malengo ya maendeleo jumuishi ambayo nchi imejiwekea. Vilevile, natoa rai kwenu wabunge wenzangu kuhakikisha Halmashauri zetu zinachangia ipasavyo Mfuko huu.

134. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa **Benki ya Wanawake Tanzania**, mikopo kwa wajasiriamali 6,956 yenye thamani ya Shilingi bilioni 10,469,282,000 (wanawake 4,596 na wanaume 2,360) imetolewa. Hivyo, mikopo iliyotolewa na Benki imeongezeka kutoka Shilingi 112,473,600,000 mwaka 2015/16 hadi kufikia Shilingi 121,796,840,000 mwaka 2016/17. Aidha, idadi ya wajasiriamali walionufaika na mikopo inayotolewa na benki imeongezeka kutoka wajasiriamali 79,983 mwaka 2015/16 hadi kufikia wajasiriamali 86,939 mwaka 2016/17 ambapo asilimia 75 ya wanufaika ni wanawake.

135. Mheshimiwa Spika, Aidha, Benki imeongeza vituo vya kutolea mikopo na mafunzo kutoka vituo 184 mwaka 2015/16 hadi kufikia vituo 252 mwaka 2016/17. Aidha, Benki iliwezesha jumla ya wanawake 223 kati ya wanufaika 560 kumiliki ardhi katika mikoa ya Dar es Salaam na Pwani. Benki pia katika kumwezesha mwanamke wa kipato cha chini kupata huduma za mikopo yenye riba nafuu, Benki imeanzisha Akaunti ya Malaika ambayo ilizinduliwa na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan. Lengo la akaunti hiyo ni kutoa mikopo yenye riba nafuu isiyozidi asilimia 10.

136. Mheshimiwa Spika, vile vile, Wizara kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi pamoja na Ofisi ya Rais TAMISEMI iliratibu uanzishwaji na uzinduzi wa majukwaa ya

uwezesaji wanawake kiuchumi katika mikoa ya Kigoma na Singida. Uanzishwaji wa majukwaa haya unalenga kuendeleza jitahada za **Makamu wa Rais, Mhe. Samia Suluhu Hassan** ambaye alizindua Jukwaa la Uwezesaji Wanawake Kiuchumi Tanzania kwa ngazi ya taifa.

- 137. Mheshimiwa Spika**, Wizara pia imeratibu maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani yaliyofanyika mwezi Machi, 2017 ambapo hapa nchini yalifanyika katika ngazi ya mkoa kwa mikoa yote. Kaulimbiu ya maadhimisho hayo ilikuwa **‘Tanzania ya Viwanda: Wanawake ni Msingi wa Mabadiliko ya Kiuchumi’**. Maadhimisho hayo yametoa fursa kwa wadau kutafakari, kubadilishana uzoefu kuhusu mafanikio yaliyofikiwa na kuzitafutia ufumbuzi changamoto mbalimbali zinazowakabili wanawake katika kufikia ukombozi wa kiuchumi.

Jitihada za Kuzuia na Kutokomeza Ukatili wa Kijinsia

- 138. Mheshimiwa Spika**, katika kukabiliana na ukatili wa kijinsia na ukatili dhidi ya wanawake na watoto, Wizara kwa kushirikiana na wadau imendaa Mpango wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto (2017/18 – 2021/22) ambao uliozinduliwa mwezi Disemba, 2016. Uzinduzi huo ulishirikisha Mawaziri 10 kutoka katika wizara mbalimbali ambao waliahidi kuutekeleza Mpango huo kwa manufaa ya wanawake na Watoto wa Tanzania. Katika Aidha, yamefanyika maandalizi ya awali ya utekelezaji wa mpango huu ambayo yalikusisha: kutoa mafunzo kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii wa mikoa 25, Maafisa wa Madawati ya Jinsia 25 kutoka katika Wizara, Idara zinazojitegemea na Wakala za Serikali. Aidha, mwongozo wa kamati za ulinzi wa wanawake na watoto katika ngazi mbalimbali umeandaliwa.

Ushiriki wa Wanawake katika Ngazi za Uongozi na Maamuzi

- 139. Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kuhamasisha wanawake kushiriki katika ngazi mbalimbali za uongozi na maamuzi. Katika kutekeleza hilo, wizara kwa kushirikiana na shirika la TGNP

imeandaa Kanzidata inayoonesha wasifu wa wanawake kwa ajili ya kuwawezesha kushiriki katika fursa za uongozi, ngazi za maamuzi na ajira. Kanzidata hii pia itasaidia kuwatambua wanawake wajasiriamali. Katika kanzidata hii tumebainisha uwepo wa wanawake wasomi, wataalam wenye uwezo katika fani mbalimbali ikiwemo engineers, wahasibu, Madaktari, Wachumi na Wataalam wa Maendeleo wa Maendeleo na Ustawi wa Jamii. Wizara itaendelea kuhimiza waajiri na mamlaka za uteuzi kutumia kanzidata hii.

Kuimarisha haki ya Mwanamke Kunyonyesha Wakati ya Kazi

- 140. Mheshimiwa Spika,** Tanzania ni moja kati ya nchi zilizoridhia matamko na mikataba mbalimbali ya kimataifa inayohusu haki ya unyonyeshaji wa Watoto. Miongoni mwa mikataba na matamko ya kimataifa ambayo imeridhiwa na Tanzania ni pamoja na '*Innocent Declaration on the Protection, Promotion and Support of Breastfeeding na Maternity Protection Convention, 2000 (No. 183)*'. Katika mwaka 2016/17, Serikali imefanya mapitio ya Sheria ya Kazi na Mahusiano Kazini hususan kifungu cha 33(10) na kuifanyia marekebisho kupitia Kanuni zake mpya zilizotangazwa kwenye Gazeti la Serikali la Na. 47 la tarehe 24/2/2017 ambapo kwa sasa imewekwa wazi haki ya mama kunyonyesha muda wa masaa mawili katika muda wa kazi kwa kipindi cha miezi 6 baada likizo ya uzazi. Kabla ya marekebisho haya, haki ya mama kunyonyesha baada ya likizo ya uzazi haikuwa imefafanuliwa ni kwa kipindi cha muda gani. Kifungu hiki sasa kinasomeka '***Where an employee is breast-feeding a child, the employer shall allow the employee to feed the child during working hours up to a maximum of two hours per day, for a period of 6 months after maternity leave***', badala ya kusomeka '***Where an employee is breast-feeding a child, the employer shall allow the employee to feed the child during working hours up to a maximum of two hours per day.***' Marekebisho hayo yatasaidia kuimarisha upatikanaji wa haki za wanawake katika uzazi na kuhakikisha haki na maendeleo ya mtoto mchanga. Nitumie fursa hii kuwataka waajiri wa sekta binafsi na wa umma kuzingatia

matakwa haya ya kisheria. Aidha, pia ninapenda kuwahamasisha wanawake kuitumia fursa hii kwa ajili ya kuweka msingi imara wa maendeleo ya awali ya watoto wao.

Uingizaji wa Masuala ya Jinsia Katika Sera, Sheria na Mipango ya Kisekta na Taifa

- 141. *Mheshimiwa Spika***, kuhusu uingizaji wa masuala ya jinsia katika Sera na Mipango, Wizara kwa kushirikiana na wadau imeandaa Taarifa ya Hali ya Jinsia Nchini ya mwaka 2016. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Takwimu pamoja na Shirika la Umoja wa Mataifa la UN-Women imeandaa viashiria vya jinsia katika utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu hapa nchini. Uwepo wa viashiria hivi utasaidia kuhakikisha upangaji, utekelezaji na ufuatiliaji wa malengo hayo unazingatia masuala ya jinsia na uwezesaji wanawake.

MAENDELEO YA MTOTO

- 142. *Mheshimiwa Spika***, Maendeleo endelevu ya Taifa lolote, yanategemea uwekezaji katika makuzi, malezi, na maendeleo ya mtoto. Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012, **idadi ya watoto ni asilimia 51.6 ya watanzania wote**. Hali hii inaonesha umuhimu wa kulinda na kusimamia utekelezaji wa haki za msingi za mtoto ambazo ni; kuishi, kuendelezwa, kulindwa, kushiriki na kutobaguliwa.

Ukatili dhidi ya watoto

- 143. *Mheshimiwa Spika***, kumekuwa na ongezeko la taarifa za vitendo vya ukatili vinavyofanywa dhidi ya watoto. Kwa mujibu wa taarifa ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, vitendo vya ukatili dhidi ya Watoto kwa mwaka 2016 vilivyoriipotiwa ni 10,551 ikilinganisha na vitendo 9,541 mwaka 2015 sawa na ongezeko la asilimia 9.6%. Vitendo hivyo vinasababishwa kwa kiasi kikubwa na hali ya umaskini na uwepo wa mila na desturi zenye madhara. Utolewaji wa taarifa za vitendo vya ukatili ni mojawapo ya mikakati ya Kupunguza vitendo hivyo katika jamii. Hivyo, Wizara kwa

kushirikiana na wadau imeendelea kupokea taarifa juu ya vitendo husika na kuchukua hatua. Taarifa kupitia mtandao wa huduma ya simu ya kusaidia kuripoti taarifa za ukatili dhidi ya watoto kupitia namba ya simu 116 (Child Helpline) zimeongezeka kutoka 33,675 mwaka 2015/16 hadi kufikia simu 37,888 mwaka 2016/17, ongezeko hili sawa na asilimia 12.5 ya simu zilizopokelewa. Kuongezeka kwa idadi hii ya simu ni matokeo ya mwamko wa jamii katika kutoa taarifa za masuala ya vitendo vya ukatili dhidi ya watoto ikiwemo ulawiti na ubakaji. Nitumie fursa hii kutoa rai kwa jamii, wazazi, walezi na watoto kutosita kutoa taarifa kuhusu vitendo vya ukatili katika maeneo yao.

- 144. Mheshimiwa Spika,** Wizara pia imetoa mafunzo juu ya mbinu za kushirikisha wazazi na walezi kubadili mitazamo kuhusu mila na desturi zenye madhara kwa watoto na umuhimu wa kuwekeza katika malezi yenye mwelekeo wa kumlinda na kumwendeleza mtoto hasa mtoto wa kike. Mafunzo hayo yalitolewa wa kipindi cha Julai 2016 mpaka Machi 2017 kwa maafisa maendeleo ya jamii 505, walimu 40 na maafisa ustawi wa jamii 39 katika Halmashauri 72 nchini.

Mimba na ndoa za utotoni

- 145. Mheshimiwa Spika,** mimba na ndoa za utotoni bado ni kikwazo katika kufikia maendeleo endelevu ya nchi yetu. Kwa mujibu wa Utafiti wa Taasisi ya Takwimu ya Taifa kiwango cha **ndoa za utotoni nchini ni asilimia 37**. Mikoa inayoongoza kwa ndoa za utotoni ni Shinyanga (59%) Tabora (58%), Mara (34%), Dodoma (51%) na Lindi (48%). Aidha Takwimu hizo pia zinaonesha kuwa **asilimia 27 ya watoto wanaathirika na mimba za utotoni** nchini, mikoa inayoongoza ni Katavi (36.8%), Tabora (36.5%), Simiyu (32.1%), Geita (31.6%) na Shinyanga (31.2%). Katika kukabiliana na ndoa na mimba za utotoni, Wizara kwa mwaka 2016/17 ilishirikiana na wadau kufanya utafiti katika mikoa 10 na halmashauri 20 na kubaini kuwa **vyanzo vikubwa vya ndoa na mimba za utotoni ni umaskini na mila potofu**. Utafiti huu umesaidia Serikali na wadau wengine kuendesha kampeni na

programu za kupinga ndoa za utotoni ili kupunguza tatizo hili. Wizara kwa kushirikiana na wadau iliendesha Kampeni maalum ya kupinga ndoa za utotoni mkoani Shinyanga ambayo iliwafikia wananchi zaidi ya 800 na kuokoa Watoto wa kike 102 waliokuwa katika hatua za kuozeshwa.

Maendeleo ya Mtoto wa Kike

- 146. *Mheshimiwa Spika***, Katika kuhakikisha kuwa mtoto wa kike anapata fursa ya kujiendeleza, Wizara imeendelea kuhamasisha uanzishwaji wa klabu za wasichana shuleni ambazo zinawapa fursa ya kujitambua, kujua haki zao na kutoa taarifa ya ukiukwaji wa haki zao. Vilevile, klabu hizi ni sehemu ambayo watoto wanakutana na kubadilishana mawazo kuhusu maendeleo yao kielimu. Katika Mwaka 2016/17, Wizara imehamasisha na kuwezesha **kuanzishwa kwa klabu 105 za watoto wa kike na kiume shuleni** katika wilaya ya Tarime, Shinyanga vijini na Kahama.

Ushiriki wa Mtoto katika Maendeleo

- 147. *Mheshimiwa Spika***, Wizara inaendelea kusimamia upatikanaji wa haki ya ushiriki wa mtoto kupitia mabaraza ya watoto. Katika mwaka 2016/17, Wizara iliwawezesha viongozi wa Kamati Kuu ya Baraza la Watoto la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kufanya ziara ya mafunzo kwenye mabaraza yanayotekeleza majukumu yake vizuri. Mikoa iliyotembelewa ni pamoja na Mwanza, Lindi, Iringa, Mjini Magharibi, Mkoa wa kusini na Mkoa wa Kaskazini. Lengo la ziara hii ni kupata ujuzi, kuboresha mabaraza na ushiriki wa Watoto katika shughuli za maendeleo. Hadi sasa, jumla za Halmashauri zilizoanzisha Mabaraza ya Watoto Ni 108 na Mikoa yenye Mabaraza za Watoto ni 21. **(Kiambatisho Na.7)**

HUDUMA ZA USTAWI WA JAMII

- 148. *Mheshimiwa Spika***, huduma za ustawi wa jamii zinalenga kuyawezesha makundi maalum kupata huduma za msingi na kushiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo. Makundi haya ni

pamoja na watoto walio katika mazingira hatarishi, watoto walio katika mkinzano na sheria, watu wenye ulemavu na wazee. Makundi mengine ni yale ambayo yanakosa au yapo katika hatari ya kukosa fursa ya kushiriki kikamlifu katika shughuli za maendeleo mfano familia zenye migogoro, wakimbizi, waathirika wa matumizi mabaya ya pombe na madawa ya kulevyaa.

Huduma za Ustawi kwa Watoto, Watoto Walio katika mazingira Hatarishi na Walio katika Mkinzano wa Sheria

- 149. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuweka mifumo ya matunzo, malezi na ulinzi wa watoto yenye misingi ya kijamii. Mwaka 2016/17, Wizara kwa kushirikiana na wadau imehamasisha na kuzijengea uwezo Halmashauri 18 kuanzisha timu za ulinzi na usalama wa mtoto ambapo idadi ya Halmashauri zenye timu za ulinzi na usalama imeongezeka kutoka 33 mwaka 2015/16 hadi kufikia Halmashauri 51 mwaka 2016/17. Vilevile, kwa kipindi cha kuanzia Julai 2016 hadi Machi 2017 Wizara imeendelea na zoezi la kuziwezesha Halmashauri kuwatambua watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi ili kuwa na takwimu sahihi zitakazotumiwa na wadau kutoa huduma. Jumla ya watoto 131,304 (wavulana 66,965 na wasichana 64,339) walitambuliwa na kupatiwa huduma mbalimbali ikiwemo chakula, mavazi, mahitaji ya shule na msaada wa kisaikolojia.
- 150. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha mwaka 2016/17, Wizara kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI imeandaa mwongozo wa mfumo wa kushughulikia masuala ya watoto walio katika mazingira hatarishi. Mfumo huu utawezesha kushughulikia masuala ya watoto kwa wakati. Vilevile, kwa kushirikiana na wadau, wizara imewajengea uwezo watoa huduma za ustawi wa jamii na watoa huduma za kujitolea 2,974, ili waweze kutoa huduma katika ngazi za kata na vijiji/mitaa.
- 151. Mheshimiwa Spika,** Wizara pia ilitoa leseni 18 za uendeshaji wa makao ya watoto na kufanya **Makao ya Watoto** yaliosajiliwa kufikia 195. Aidha, Wizara imeendelea kutoa huduma za chakula,

malazi na huduma za afya kwa watoto 115 waliotunzwa katika Makao ya Taifa ya Watoto Kurasini.

- 152. *Mheshimiwa Spika***, Ili kuwezesha watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi kulelewa katika familia, Wizara inatekeleza mpango wa kuwatumia walezi wa kuaminiwa, walezi mbadala, huduma ya malezi ya kambo na kuasili. Kwa mwaka 2016/17, jumla ya watoto 53 (Me 19, Ke 24) waliwekwa katika malezi ya kambo na watoto 20 (Me 7, Ke 13) waliasiliwa. Katika kipindi hicho Wataalamu wa Ustawi wa Jamii 35 walijengewa uwezo kuhusu kuwatabua walezi wa kuaminika ambao watatoa huduma ya muda kwa watoto hao.

Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto

- 153. *Mheshimiwa Spika***, Malezi Changamshi ya awali kwa mtoto yameendelea kuratibiwa. Kwa mwaka 2016/17, vituo 75 vya kulelea watoto wadogo mchana vimesajiliwa na kufanya idadi ya vituo hivyo kuongezeka kutoka vituo 782 mwaka 2015/16 hadi kufikia vituo 856 mwaka 2016/17. Aidha, jumla ya walezi wa watoto 1,211 walidahiliwa katika vyuo 23 vya malezi ya watoto. Vilevile, Wizara iliwajengea uwezo wa malezi na makuzi ya mtoto wataalam wa afya na wahudumu wa afya ngazi ya jamii 401 katika Manispaa ya Tabora na Halmashauri ya Nzega na Igunga.

Huduma kwa Watoto walio katika Mkinzano na Sheria na Marekebisho ya Tabia.

- 154. *Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kutoa matunzo na maadilisho kwa watoto walio katika mkinzano na sheria katika mahabusu za watoto za Dar es Salaam, Arusha, Mbeya, Moshi na Tanga na Shule ya Maadilisho Irambo. Katika mwaka 2016/17, Wizara imetoa huduma za chakula, malazi, mavazi, huduma za matibabu na elimu kwa watoto 375 (wavulana 345, wasichana 30) walio katika mahabusu za watoto na waadiliwa (wavulana 72) katika shule ya Maadilisho Irambo. Aidha, Wizara imewachepusha watoto 882 kutoka katika mfumo wa makosa ya jinai. Kati yao,

watoto 353 wamepitia mpango wa jamii wa marekebisho ya tabia kwa watoto waliokinzana na sheria na watoto 529 waliotuhumiwa kufanya makosa ya jinai kutoka katika Vituo vya Polisi na kuunganishwa na familia zao.

- 155. Mheshimiwa Spika**, aidha, Wizara iliwajengea uwezo maafisa 228 wanaosimamia haki za Watoto. Mafunzo yalihusu utekelezaji na usimamizi wa amri za mahakama ili kuboresha upatikanaji wa haki kwa wakati. Kati ya hao, Mahakimu 46, Maafisa Ustawi wa Jamii 135 na Waendesha Mashtaka 47.

Maendeleo na Ustawi wa Familia

- 156. Mheshimiwa Spika**, familia ni kitovu cha maendeleo ya binadamu na Taifa kwa ujumla. Katika kuhakikisha utulivu na uimara wa familia ambao ni msingi wa jamii, Wizara imeendelea kutoa huduma za unasihi na usuluhishi wa migogoro ya ndoa. Katika mwaka 2016/17, jumla ya mashauri ya ndoa 6,819 yalipokelewa ambapo mashauri 2,727 yalisuluhishwa na mengine 4,092 yalipelekwa mahakamani kwa utatuzi wa kisheria.

- 157. Mheshimiwa Spika**, Wizara imewajengea uwezo wataalam wa Maendeleo ya Jamii na Ustawi wa Jamii 402 kuhusu elimu ya malezi bora katika ngazi ya familia. Mafunzo hayo yalitolewa katika Halmashauri na Kata za Temeke, Mafinga na Mufindi. Mafunzo hayo yanatarajiwa kuwawezesha wataalam hao kuwajengea uwezo wazazi na walezi kuhusu malezi bora ya watoto.

HAKI NA USTAWI WA WAZEE

- 158. Mheshimiwa Spika**, wazee ni rasilimali muhimu kwa maendeleo ya taifa kutokana na uzoefu na ujuzi walionao katika nyanja mbalimbali. Kwa mwaka 2016/17, Wizara kwa kushirikiana na wadau imeendelea kutoa elimu kwa jamii kuhusu haki na ustawi wa wazee kupitia vyombo vya habari na maadhimisho ya siku ya wazee. Elimu hii imesaidia kuongezeka kwa idadi ya wazee wanaopata huduma za afya na kupungua kwa vitendo vya ukatili.

Kwa mujibu wa Taarifa ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi mauaji ya wazee yamepungua kutoka 190 (me 66, ke 124) mwaka 2015 hadi 135 (me 44, ke 91) mwaka 2016.

- 159. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/17, Wizara kwa kushirikiana na OR - TAMISEMI imewezesha kuwatambua wazee 69,100 na kufanya idadi ya wazee waliotambuliwa kufikia 367,889. Kati yao, wazee 16,990 walipatiwa vitambulisho vya msamaha wa matibabu na kufanya idadi ya wazee wenye vitambulisho hivyo kufikia 74,590. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na wadau imewezesha kufanyika kwa ukarabati katika makazi ya wazee ya Kailima. Wizara pia imeboresha miundombinu kwa kuanza ujenzi wa bweni katika makazi ya Kolandoto (Mkoa wa Shinyanga). Vilevile, Wizara imeendelea kutoa huduma kwa wazee 456 wasiojiweza katika makazi 17 yanayoendeshwa na Serikali. Huduma hizi ni pamoja na chakula, malazi na matibabu.
- 160. Mheshimiwa Spika**, nachukua fursa hii kuwashukuru wadau mbalimbali waliochangia katika kuhakikisha huduma bora kwa wazee nchini. Kipekee napenda kumshukuru **Mke wa Rais, Mhe, Mama Janet Magufuli** kwa kuwa mstari wa mbele katika kuwasaidia wazee wanaotunzwa katika makazi ya wazee hapa nchini. Natoa wito kwa jamii kuiga mfano wa mama yetu huyu. Sote ni wazee watarajiwa tunahitaji kuwaenzi, kuwaheshimu na kuwatunza wazee wetu.

Wataalam wa Ustawi wa Jamii

- 161. Mheshimiwa Spika**, Wataalam wa Ustawi wa Jamii ni muhimu katika kuhakikisha utengamano wa familia na jamii. Katika kuhakikisha tunakua na wataalam hao katika ngazi za Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara kupitia **Taasisi ya Ustawi wa Jamii** imeendelea kuzalisha wataalam hao kupitia mafunzo katika fani za Ustawi wa Jamii na fani nyingine ikiwemo Rasilimali Watu na Mahusiano Kazini kwa ngazi ya Astashahada, Stashahada, Shahada, Stashahada ya Uzamili na Shahada ya Uzamili. Kwa kipindi cha mwaka 2016/17, jumla ya wataalamu 1,164 walihitimu.

Aidha, katika kuboresha mafunzo hayo, Taasisi imeendelea na ujenzi wa Maktaba ya kisasa.

MASHIRIKA YASIYO YA KISERIKALI

- 162. *Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kuweka mazingira wezeshi kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kushiriki kikamilifu katika kuchangia kufikiwa kwa maendeleo na ustawi wa jamii. Katika kutekeleza hilo, Wizara iliendelea kusajili, kufuatilia na kuratibu shughuli za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali nchini ambapo, katika kipindi cha 2016/17, jumla ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 264 yalisajiliwa. Kati ya hayo mashirika 26 ni ngazi ya Kimataifa, 218 ngazi ya Kitaifa, 5 ngazi ya Mkoa na 15 ni ya ngazi ya Wilaya. Usajili huo umeongeza idadi ya mashirika kutoka 8,047 mwezi Julai, 2016 hadi kufikia 8,144 mwezi Machi, 2017 (**Kiambatisho Na. 8**).
- 163. *Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha mwaka 2016/17, Wizara ilifuatilia utendaji wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Katika ufuatiliaji huo, jumla ya miradi 79 ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali iliyopo katika mikoa ya Rukwa, Katavi, Geita, Mara, Tanga na Mtwara ilitembelewa na kukaguliwa. Wizara pia ilifanya tathmini ya taarifa za utekelezaji kutoka katika mashirika 267. Matokeo ya tathmini yanaonesha kuwa mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali umezidi kuimarika hasa katika maeneo ya; afya, hifadhi ya mazingira, elimu, jinsia, utawala bora, utetezi wa haki za binadamu, hifadhi ya jamii na kilimo. Taarifa ya ufuatiliaji na tathmini pia ilibainisha kuwa, jumla ya Mashirika 100 hayakuzingatia miongozo ya kisera, sheria, kanuni na katiba ya mashirika husika na hivyo kufutiwa usajili.

UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA 2016/17 KWA TAASISI NYINGINE ZILIZO CHINI YA WIZARA

TAASISI YA CHAKULA NA LISHE (TFNC)

- 164. *Mheshimiwa Spika***, Taasisi ya Chakula na lishe ina jukumu la kuratibu, kutoa miongozo, kujenga uwezo kwa wataalamu, kufanya tafiti na kuishauri Serikali na wananchi kwa ujumla juu ya lishe bora na namna ya kuutokomeza utapiamlo. Taasisi imeendelea na jitihada za kupambana na utapiamlo kwa watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano na wanawake walioko kwenye umri wa kuzaa. Aidha, Utafiti wa Maendeleo ya Afya Nchini wa mwaka 2016 umebaini kuwa tatizo la udumavu kwa watoto chini ya miaka mitano limepungua kutoka asilimia 42 hadi 34, uzito pungufu umepungua kutoka asilimia 16 hadi 14. Mafanikio haya yametokana na utekelezaji wa afua mbalimbali. Vilevile, Taasisi ilikamilisha maandalizi ya Mpango wa Taifa wa Utekelezaji wa masuala ya lishe 2016/17 – 2020/21. Mpango huo ni mbadala wa Mpango Mkakati wa Taifa wa Lishe wa mwaka 2011/12-2015/16 ambao umekwisha muda wake.
- 165. *Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2016/17, Taasisi ilifanya mafunzo kwa wakufunzi wa Taifa wa Afya na Lishe ya watoto. Mafunzo yalikusisha wajumbe wa Timu za Uendeshaji wa Huduma za Afya za Halmashauri kwa Halmashauri zote 184 nchini. Mafunzo yalilenga kutathmini zoezi la Afya na Lishe ya watoto la mwezi Juni 2016, kuangalia changamoto zinazowakabili, ili kuwapa wajumbe wa Timu za Uendeshaji wa Huduma za Afya za Halmashauri ujuzi zaidi na mbinu za utekelezaji wa afua za Afya na Lishe ya watoto. Aidha, Taasisi imeendelea kukusanya taarifa za ufanisi wa utoaji huduma za mwezi wa Afya na Lishe ya Mtoto kwa mwezi Desemba 2016 kutoka mikoa yote nchini ili kujua idadi ya watoto waliofikiwa na huduma za matone ya vitamini A (miezi 6 – 59), utoaji wa dawa za kutibu maambukizi ya minyoo (miezi 12 – 59) na upimaji wa hali ya lishe ya watoto wenye umri wa miezi 6 - 59 pamoja na kutoa rufaa kwa watoto wenye utapiamlo.

BOHARI YA DAWA (MSD)

- 166. Mheshimiwa Spika**, Bohari ya Dawa imetekeleza majukumu yake ya msingi ya ununuzi, uhifadhi na usambazaji wa Dawa, Vifaa, Vifaa Tiba, Vitendanishi na chanjo ili kuwezesha upatikanaji endelevu katika vituo vya kutolea huduma za afya zaidi ya **vituo 5,414** nchini. Wastani wa upatikanaji wa dawa muhimu katika Bohari ya Dawa umeimarika. Hali hiyo inatokana na ongezeko la bajeti ya dawa kutoka Shilingi bilioni 31 mwaka 2015/16 hadi kiasi cha Shilingi bilioni 251.5 mwaka 2016/17. Aidha, Katika kipindi cha Julai 2015 mpaka Machi 2016, Bohari ilipokea ni **Shilingi bilioni 24** tu kwa ajili ya dawa. Kwa mwaka mzima ikilinganishwa na kipindi cha 2016/17 hadi kufikia Machi 2017 ambapo Bohari tayari imeshapokea kiasi cha **Shilingi bilioni 112.198**.
- 167. Mheshimiwa Spika**, MSD inaendelea kuimarisha mfumo wa ugavi ambapo imefunga viambato vya kielektroniki (Barcode Scanners) katika maeneo yote ya usambazaji dawa ili kuwezesha upatikanaji wa taarifa sahihi za dawa, vifaa na vifaa tiba katika maghala wakati wote. Aidha, Kwa upande wa miradi msonge, MSD imetunza na kusambaza dawa zenye thamani ya zaidi ya **Shilingi bilioni 202** katika kipindi cha kuanzia Julai 2016 hadi Machi, 2017. Hali hiyo, imewezesha kuimarika kwa upatikanaji wa dawa za Malaria, UKIMWI, Kifua Kikuu na Ukoma nchi nzima. Vilevile, MSD imenunua, kutunza na kusambaza vifaa, vifaa tiba na vitendanishi vyenye thamani ya zaidi ya **Shilingi bilioni 57** kwa ajili ya kuimarisha huduma za uchunguzi wa magonjwa ya Malaria, UKIMWI, Kifua Kikuu na Ukoma nchi nzima.
- 168. Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha upatikanaji wa dawa na vifaa tiba kwa kiwango cha kutosha nchini, Serikali kupitia mpango wa ushikirishwaji wa sekta binafsi imeanza kutekeleza mkakati wa ujenzi wa viwanda vitakavyozalisha dawa na vifaa Tiba hapa nchini ambapo MSD imetengewa eneo la Ekari 100 Mkoani Pwani. Aidha, MSD imeendelea kupanua uwezo wa maghala katika kanda zake ambapo katika kipindi cha Julai 2016 hadi Machi, 2017,

maandalizi ya ujenzi wa ghala la Kanda ya Dar es Salaam ujenzi wake unategemewa kuwa umekamilika ifikapo June 2018. Kukamilika kwa ujenzi huo kutasaidia kuondoa gharama ya **Shilingi milioni 800** zinazotumika katika ukodishaji wa maghalaya kuhifadhi dawa kutoka sekta binafsi kwa mwaka.

MFUKO WA TAIFA WA BIMA YA AFYA (NHIF)

- 169. Mheshimiwa Spika**, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) umeendelea kubuni na kutekeleza mikakati mbalimbali hususan kuongeza wigo wa wanufaika wa bima ya afya. Idadi ya wanachama wachangiaji wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya, imeongezeka kutoka wanachama **702,598** waliokuwa wameandikishwa mwaka 2015/16 hadi kufikia **wanachama 792,987** mwezi Machi 2017. Aidha, idadi ya wanufaika nayo iliongezeka kutoka **3,377,023** mwaka 2015/16 hadi kufikia **wanufaika 3,880,088** mwezi Machi 2017. Hii inaonyesha kuwa wanachama wa Mfuko wameongezeka kwa wastani wa **asilimia 15** na wanufaika wameongezeka kwa **asilimia 13** katika kipindi cha miaka mitano (**Kiambatisho Na.9**). Mafanikio hayo yameweza kupatikana kutokana na juhudi zinazofanywa na Mfuko za kuelimisha watazania pamoja na kubuni mbinu mbalimbali za kuongeza wigo wa wanachama, kama kuanzishwa kwa mpango wa **KIKOA** (unaojumuisha kundi la wajasiriamali, vikundi vya vikoba, saccos na wavuvi), **TOTO AFYA KADI** (unaojumuisha watoto chini ya miaka 18), Wanafunzi wa vyuo vya Elimu ya Juu, Wastaafu na wanachama binafsi.

MFUKO WA AFYA YA JAMII (CHF)

- 170. Mheshimiwa Spika**, Hadi kufikia Machi 2017 Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF) ulikuwa na jumla ya kaya **1,595,651** zilizojiunga ukilinganisha na kaya **1,452,855** zilizokuwa zimejiunga mwaka 2015/16. Aidha, wanufaika wameongezeka kutoka **8,717,130** mwaka 2015/16 hadi kufikia wanufaika **9,573,906** Machi 2017. (**Kiambatisho Na.10**). Katika kuchangia juhudi za wananchi wanaochangia CHF na kuboresha huduma zitolewazo, Serikali

hutoa malipo ya tele kwa tele kwenye Halmashauri kulingana na kiwango cha makusanyo ya CHF. Malipo yaliyofanyika kwa Halmashauri kwa kipindi cha kuanzia Julai 2016 hadi Machi 2017 ni **Shilingi bilioni 3.5**. na hivyo kuwezesha jumla ya **Shilingi bilioni 12.3** kulipwa kwa Halmashauri mbalimbali nchini tangu Mfuko ulipokabidhiwa jukumu hili mwezi Julai 2009. Vilevile, Mfuko umefanya mapitio ya Tiba kwa Kadi (TIKA) ili Huduma hiyo iimarike Mijini, Utaratibu wa uanzishaji wa TIKA uko katika hatua mbalimbali za utekelezaji katika Manispaa za jiji la Dar-es-salaam, Kibaha Mji na Babati Mjini. Matarajio ya Mfuko ni kuwa Halmashauri zote za Miji zitajielekeza katika kutekeleza TIKA.

MAMLAKA YA CHAKULA NA DAWA (TFDA)

- 171. Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia Mamlaka ya Chakula na Dawa imeendelea na shughuli za udhibiti wa ubora na usalama wa chakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba ambapo Mamlaka inakamilisha utekelezaji wa Mpango Mkakati wake wa miaka mitano wa 2012 – 2017. Aidha, katika kipindi cha mwaka 2016/17, Mamlaka ilipokea jumla ya maombi ya usajili wa viwanda vipya 748 (chakula 739 na vipodozi 9) na vyote vilitathminiwa na kukaguliwa ambapo viwanda 622 (chakula 613 na vipodozi 9) sawa na **asilimia 83** vilisajiliwa baada ya kukidhi vigezo. Vilevile, Mamlaka ilipokea jumla ya maombi 8,023 ya usajili wa majengo na maeneo ya biashara ambapo maeneo 7,873 sawa na **asilimia 98.4** yalikitidhi vigezo na kusajiliwa.
- 172. Mheshimiwa Spika**, Katika kujiridhisha na usalama na ubora wa bidhaa katika soko, Mamlaka ilifanya ukaguzi wa majengo 13,461 (6,743 ya chakula, 2,553 dawa, 3,957 vipodozi na 208 vifaa tiba) ambapo majengo 11,923 sawa na **asilimia 89** yalikitidhi vigezo na hivyo kuhuishiwa vibali vyao vya biashara kwa mwaka 2016/17. Aidha, kupitia mfumo wa ufuatiliaji wa ubora na usalama wa bidhaa katika soko, jumla ya sampuli 462 zilichukuliwa katika soko na kuchunguzwa katika maabara ambapo sampuli 451 sawa na **asilimia 98** zilifaulu na sampuli 11 hazikukidhi vigezo na hivyo bidhaa husika ziliondolewa katika soko. Aidha, Mamlaka ilipokea

maombi 5,802 kwa ajili ya usajili wa bidhaa za dawa, chakula, vifaa tiba na vipodozi ambapo bidhaa 4,322 sawa na **asilimia** 75 yalisajiliwa. Vilevile, Mamlaka ilifanya uchunguzi wa jumla ya sampuli 2,860. *Kati ya sampuli zilizochunguzwa, sampuli 2,396 sawa na asilimia 84 zilifaulu vigezo vya ubora na usalama na asilimia 16 hazikukidhi vigezo na hivyo bidhaa husika hazikusajiliwa na nyingine kuondolewa.*

173. Mheshimiwa Spika, Mamlaka ilisimamia uteketezaji wa jumla ya tani 631.7 za bidhaa za chakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba, zenye thamani ya takriban Shilingi 797,312,103.15 kutokana na kutofaa kwa matumizi ya binadamu. Aidha, vipodozi vyenye viambato sumu vya thamani ya takriban Shilingi milioni 616 vilikamatwa katika maghala ya kificho na viwanda bubu jijini Dar es Salaam na matenka ya kubebea mafuta mkoani Njombe ambapo vipodozi hivyo vinasubiri hatua za kisheria kukamilika kabla ya kuteketezwa. Vilevile, Mamlaka imetoa Elimu kwa Umma kwa makundi mbalimbali ya wananchi na mihadhara katika vyuo na shule za sekondari ambapo wanafunzi na walimu 51,835 katika mikoa ya Ruvuma, Lindi, Pwani, Mwanza, Shinyanga, Geita, Mbeya, Rukwa, Tanga, Simiyu na Songwe walielimishwa.

174. Mheshimiwa Spika, Ili kusogeza huduma karibu na wananchi, Mamlaka imekamilisha ujenzi wa ofisi na maabara ya Kanda ya Ziwa katika eneo la Nyakato, jijini Mwanza. Kukamilika kwa ofisi na maabara hiyo kutaongeza ufanisi wa utoaji huduma na hivyo kuimarisha udhibiti. Aidha, Mamlaka imeimarisha mfumo wa kielektroniki wa kupokea taarifa za madhara yatokanayo na matumizi ya dawa kwa njia ya simu ya kiganjani ili kurahisisha upatikanaji wa taarifa za madhara ya dawa kwa haraka. Kupitia mfumo huo jumla ya taarifa **mpya 71** sawa na asilimia 44 ya taarifa zote zimepokelewa. Vilevile, Mamlaka imeanzisha mfumo wa kuweka taarifa za bidhaa zote zilizosajiliwa nchini kwenye mtandao ambao unasaidia wananchi na wateja kwa ujumla kuona bidhaa zilizosajiliwa na tarehe za kuisha muda wa usajili.

WAKALA WA MAABARA YA MKEMIA MKUU WA SERIKALI (GCLA)

- 175. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/17, Wizara kupitia Wakala wa Mkemia Mkuu wa Serikali imenunua mtambo wa **Liquid Chromatography Mass Spectrometer** kwa kiasi cha Shilingi bilioni 1.6. Mtambo huo utatumika katika kufanya uchunguzi wa sampuli mbalimbali, zikiwemo za sumu, kilimo, uvuvi, mifugo, maji, dawa za binadamu, gesi, mafuta n.k. Aidha, mtambo utatumika kuchunguza dawa za kulevya na kutoa mchango katika juhudi za Serikali kupambana na matumizi ya dawa za kulevya. Vilevile, katika kuboresha huduma za uchunguzi wa kimaabara Wakala imenunua na kusimika mtambo wa kisasa (**ED-XRF**) katika Maabara ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Mbeya. Mtambo huo utatumika kutambua ubora na usalama wa bidhaa mbalimbali za viwandani na kilimo, kutambua uwepo wa madini ya thamani kwenye udongo na bidhaa za vito na sampuli zinazohusiana na usalama wa afya na mazingira.
- 176. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/17, Wakala ilikagua na kusajili makampuni 261 yanayojihusisha na shughuli za kemikali nchini sawa na asilimia 70 ya lengo. Aidha, Wakala ilikagua viwanda na maghala 346 ambayo ni sawa na asilimia 65 ya lengo hadi kufikia Machi, 2017. Vilevile, Wakala ilifanya uchunguzi na kutoa taarifa ya sampuli **25,632**, sawa na asilimia 194 ya lengo la kuchunguza sampuli **13,170**. Sampuli hizo ni za Vinasaba, Sumu, Dawa za Kulevya, Vyakula, Dawa asilia, Kemikali, Maji, Vilainishi vya Mitambo na sampuli za mazingira. Pia, Wakala umeendelea na ujenzi wa Maabara ya Nyanda za Juu Kusini Mbeya ambao hadi mwezi Machi jengo hilo limeshapauliwa na **Shilingi 180,000,000.00** sawa na asilimia 60 ya gharama zote zimetumika.

TAASISI YA TAIFA YA UTAFITI WA MAGONJWA YA BINADAMU (NIMR)

- 177. *Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2016/17, Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu imeendelea na utafiti wa chanjo dhidi ya virusi vya HPV vinavyosababisha Saratani ya mlango wa kizazi. Utafiti huo unalenga kubaini kama dozi moja ya chanjo hiyo inaweza kutoa kinga sawa na dozi mbili au tatu. Utafiti unashirikisha wasichana walio na umri wa miaka kati ya 9 na 14 walio katika shule za umma za kutwa za msingi na sekondari zilizopo jijini Mwanza. Utafiti huo utashirikisha wasichana 900, watakaofuatiliwa kwa miezi 36 tangu walipopata dozi ya kwanza na unategemewa kukamilika mwaka 2021.
- 178. *Mheshimiwa Spika***, Taasisi kwa kushirikiana na Taasisi kutoka nchi za Kenya, Uganda na Ghana zilishiriki katika utafiti wa awali wa chanjo dhidi ya virusi vya Ebola. Madhumuni ya utafiti huo ilikuwa ni kutathmini usalama, ubora na uwezo wa kutengeneza kinga dhidi ya virusi vya Ebola. Aidha, utafiti huo ulifanyika katika jiji la Mwanza kwa kushirikisha watu wazima 25 wasiokuwa na matatizo ya kiafya waliohiari kushiriki, wakiwemo wanaume 23 na wanawake Wawili. Matokeo ya utafiti huo yanaonesha kuwa chanjo hiyo kuwa ni salama. Uchambuzi wa takwimu unaendelea ili kuweza kubaini ubora wa chanjo hiyo katika kufanya mwili utengeneze kinga dhidi ya virusi vya Ebola. Matokeo haya yatawasilishwa pale uchambuzi wa takwimu utakapokamilika.
- 179. *Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2016/17, Taasisi ilifanya utafiti katika tiba asilia ili kubaini uwezo na usalama wa dawa za asili zinazotumiwa na jamii mbalimbali hapa nchini. Aidha, Taasisi imefanya utafiti wa dawa za asili zinazotumika kwa ajili ya tiba ya magonjwa ya malaria, UKIMWI na magonjwa nyemelezi, ugonjwa wa ini, shinikizo la damu, kisukari na kupunguza mafuta lehemu mwilini pamoja na uvimbe wa tezi dume kwa wanaume na dawa inayoongeza nguvu za kiume. Taasisi iko katika hatua za mwisho za kukamilisha usajili wa dawa asilia 11 ili ziweze kuingizwa sokoni.

MABARAZA YA KITAALUMA

- 180. Mheshimiwa Spika**, Serikali inatambua umuhimu wa taaluma mbalimbali zilizomo katika sekta ya afya. Kwa kuzingatia hilo Serikali imetunga sheria mbalimbali za kusimamia wanataaluma wa taaluma hizo. Hadi Machi 2017, Wizara imetunga sheria nane zinazosimamia taaluma za udaktari na udaktari wa meno; uuguzi na ukunga; ufamasia; wataalam wa maabara; wataalam wa afya; optometria; radiolojia na tiba asili. Aidha, Wizara inasimamia utoaji wa huduma kupitia hospitali na maabara binafsi nchini.
- 181. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/17, Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania limeendelea kusimamia ubora wa huduma zinazotolewa na wauguzi na wakunga nchini na kuhakikisha jamii inapata huduma za uuguzi na ukunga zilizo bora na salama. Aidha, awamu ya kwanza ya **Ujenzi wa Kituo cha kuwaendeleza Wauguzi na Wakunga** kitaaluma nchini katika eneo la **mjini Kibaha (Pwani)** kwa kutumia vyanzo vya mapato ya ndani **umekamilika**. Lengo la mradi huo ni kuwawezesha wauguzi na wakunga nchini kupata nafasi ya kujiendeleza kitaaluma kwa kupitia mafunzo ya masafa yatakayokuwa yakiratibiwa katika jengo hilo. Mradi huo umegharamiwa kwa mapato ya ndani ya Baraza ambapo unatarajia kukamilika kabla ya Mwezi Juni, 2017 na kiasi cha **Shilingi bilioni 2.674** kimetumika.
- 182. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/17, **Baraza la Famasi** liliendelea kushirikiana na Taasisi nyingine za Serikali kufanya kaguzi katika maduka ya jumla na rejareja ya dawa ambapo jumla ya maduka ya dawa **721** yalikaguliwa na maduka **396 asilimia 54.9** yalikutwa na makosa mbalimbali. Baadhi ya makosa yaliyobainika ni pamoja na utoaji huduma ikiwemo kuendesha biashara ya dawa pasipo usimamizi wa mfamasia na uuzaji wa dawa zisizoruhusiwa kwa maduka ya dawa muhimu. Aidha, Baraza limetoa vibali kwa famasi **190** na maduka ya dawa muhimu **1,009** katika Halmashauri mbalimbali ambapo hadi kufikia Machi 2017 jumla ya famasi **1,432** na maduka ya ADDO **11,517** **yalikuwa yamesajiliwa** nchini kote.

- 183. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/17, **Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala** kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI imewasajili waganga wa tiba asili na tiba mbadala **5,298** kutoka mikoa yote nchini na hivyo kufikisha waganga **15,960** waliosajiliwa, vituo vya kutolea huduma vilivyosajiliwa ni **45** na hivyo kufikisha jumla ya vituo **228**. Aidha, Baraza lilifanya ufuatiliaji wa huduma za tiba asili katika Mikoa ya Ruvuma, Mbeya, Iringa na Songwe na kutoa elimu kuhusu Sheria, Kanuni, Miongozo mbalimbali kwa waratibu **17** wa mikoa hiyo pamoja na baadhi ya waganga **373** wa tiba asili.
- 184. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/17, **Bodi ya Ushauri ya Hospitali Binafsi** imesajili vituo 45, makampuni 13 na kuandaa Mkataba wa Huduma kwa Wateja. Aidha, **Bodi ya Maabara Binafsi za Afya** ilifanya ukaguzi wa jumla ya bidhaa 309 zilizoingizwa nchini.

III. VIPAUMBELE VYA WIZARA NA BAJETI YA MAPATO, MATUMIZI YA KAWAIDA NA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2017/18

185. *Mheshimiwa Spika* Katika mwaka wa fedha 2017/18, Wizara kupitia fungu 52 itatekeleza vipaumbele vifuatavyo:

- i. Kuimarisha Huduma za Kinga, Tiba, na kuongeza usawa katika kutoa huduma za afya;
- ii. Kuimarisha huduma za afya ya uzazi na mtoto ili kupunguza vifo vya wanawake wajawazito na watoto;
- iii. Kuimarisha upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi katika vituo vya umma vya kutolea huduma za afya;
- iv. Kuimarisha miundombinu kwenye vyuo vya mafunzo ya afya kwa lengo la kuongeza udahili na upatikanaji wa rasilimali watu;
- v. Kuimarisha matibabu ya kibigwa nchini kwa kuendeleza ujenzi, upanuzi, ukarabati wa miundombinu na kufunga mitambo ya kisasa ya kutolea huduma za afya katika Hospitali ya Taifa Muhimbili, Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI), Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI), Hospitali ya Benjamini Mkapa - Dodoma, Taasisi ya Saratani Ocean Road, Hospitali Maalum za Mirembe na Kibong'oto; pia Hospitali za Rufaa za Kanda za Bugando, KCMC, Mbeya na Mtwara;
- vi. Kuimarisha mazingira ya ubia na ushirikiano kati ya Serikali na Sekta binafsi (PPP) katika utoaji wa huduma za afya;
- vii. Kuimarisha huduma za lishe na upatikanaji wake katika jamii na vituo vya kutolea Huduma za Afya;
- viii. Uimarishaji wa matumizi ya Teknolojia ya Habari na

Mawasiliano (TEHAMA) katika kuboresha huduma za afya;
na

ix. Kuhamasisha wananchi kwa nia ya kuongeza idadi ya wanaojiunga na Mifuko ya Bima za Afya.

186. Mheshimiwa Spika, Kwa upande wa Fungu 53 imepanga kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia maeneo ya kipaumbele yafuatayo;

- i. Kuamsha ari ya wananchi kushiriki katika shughuli za kujiletea maendeleo;
- ii. Kuwezesha utekelezaji wa Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto wa mwaka 2017/18 – 2021/22;
- iii. Kuimarisha upatikanaji wa haki na maendeleo ya Mtoto;
- iv. Kukuza usawa wa jinsia na uwezesaji wa wanawake kiuchumi;
- v. Kuimarisha huduma za ustawi wa Mtoto na Wazee;
- vi. Kuimarisha ushiriki wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika maendeleo ya jamii kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za nchi; na
- vii. Kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia katika Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru, Vyuho vya Maendeleo ya Jamii pamoja na Taasisi ya Ustawi wa Jamii

187. Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza vipaumbele vilivyoainishwa katika mwaka 2017/18, kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na;

HUDUMA ZA KINGA

188. Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha 2017/18, Wizara itaendelea kutekeleza afua mbalimbali za huduma za kinga ikiwa ni pamoja na;

- i. Kununua na kusambaza chanjo kulingana na mahitaji ya nchi ambapo **jumla ya Shilingi bilioni 33** zimetengwa;
- ii. Kununua na kusambaza **majokofu 1,710** ya kutunzia chanjo yatakayotumika katika ngazi ya wilaya na vituo vya huduma;
- iii. Kuendelea kutekeleza Kampeni ya uhamasishaji na uelimishaji umma **(Behaviour Change and Communication-BCC)** kuhusu usafi wa mazingira nchini;
- iv. Kuendelea kugawa dawa kwa ajili ya kuzuia maambukizi ya ugonjwa wa usubi na Matende, minyoo ya tumbo, kichocho na ugonjwa wa trakoma katika Halmashauri za mikoa ambayo haikupatiwa dawa hizo kwa mwaka 2016/17;
- v. Kuendela kugawa vyandarua kupitia kliniki za wajawazito na watoto (RCH) katika mikoa 9 ya Ruvuma, Lindi, Mtwara, Geita, Mwanza, Kagera, Mara, Simiyu na Kigoma na baadae kujumuisha Mikoa mingine iliyobaki hadi kukamilisha mikoa yote kwa awamu;
- vi. Kuendelea kuhakikisha upatikanaji wa vitendanishi (mRDT) kwa ajili ya kupima uwepo wa vimelea vya malaria na dawa mseto katika vituo vyote vya kutolea huduma za afya nchini;
- vii. Kuongeza wigo na kasi ya uibuaji wa wagonjwa wa kifua kikuu katika mikoa yote nchini;
- viii. Kusambaza mashine 90 za GenXpert zitakazotumika kufanyia uchunguzi wa vimelea vya Kifua kikuu nchini;
- ix. Kufanya kampeni maalum za uchunguzi na uibuaji wa wagonjwa wapya wa ukoma katika wilaya zenye viwango vikubwa vya maambukizi zikiwemo wilaya za Liwale, Kilombero, Chato, Nanyumbu, Mkinga na Muheza;
- x. Kuendelea kutoa dawa za kufubaza virusi vya UKIMWI kwa jumla ya watu **2,253,836** nchini;
- xi. Kufunga mashine mpya **80** za kupima uwingi wa virusi vya UKIMWI, TB na Utambuzi wa Virusi vya UKIMWI kwa watoto wadogo wenye umri chini ya miezi 18 katika hospitali za mikoa ambayo haijapatiwa huduma hii na hasa katika wilaya zenye idadi kubwa ya WAVIU;

- xii. Kuendelea kuhamasisha wananchi kuzingatia mfumo bora wa maisha ikiwemo kufanya mazoezi mara kwa mara, kuzingatia ulaji wa vyakula unaofaa, kupunguza unywaji wa pombe kupita kiasi, kujiepusha na matumizi ya sigara na bidhaa za tumbaku pamoja na kujenga utamaduni wa kupima afya mara kwa mara; na
- xiii. Kuanza mchakato wa kutunga sheria mpya inayoendana na *Framework of the convention on tobacco control* badala ya sheria ya Tumbaku ya mwaka 2003 inayotumika sasa.

Huduma za Afya ya Uzazi na Mtoto

- i. Kuendelea kushirikiana na wadau wa maendeleo katika kununua na kusambaza dawa na vifaa vya uzazi wa mpango nchini ambapo **Serikali imetenga jumla ya Shilingi bilioni 14;**
- ii. Kuendelea kununua, kusambaza na kutoa bila malipo dawa kwa ajili ya uzazi salama katika vituo vya umma vya kutolea huduma ikiwemo oxytocin (dawa ya kuzuia kutokwa na damu baada ya kujifungua), magnesium sulphate (kwa ajili ya kifafa cha mimba), Fefol (kwa ajili ya kuongeza damu) ambapo jumla ya **Shilingi bilioni 7 zimetengwa;**
- iii. Kuendelea kuhamasisha jamii kuhusu umuhimu wa kuhudhuria kliniki kwa akinamama wajawazito nchini na kujifungulia katika Vituo vya kutolea huduma badala ya kujifungulia nyumbani;
- iv. Kuendelea kushirikiana na wadau wa maendeleo kwa kulipia kadi za Bima ya Afya kwa wanawake wajawazito wa kipato cha chini 150,000 kupitia Mradi wa Tumaini la Mama ambapo **jumla ya Shilingi milioni 600 zimetengwa;**
- v. Kuboresha huduma za uchunguzi za uzazi salama kwa kununua **mashine 65** za ultrasound kwa ajili ya vituo vya afya ili kuwezesha kutoa huduma maalum za dharura kwa kinamama wajawazito ambapo **jumla ya Shilingi**

5,412,500,000 zimetengwa;

- vi. Kuendelea kuboresha upatikanaji wa huduma za uzazi za dharura ikiwemo upasuaji wa kumtoa mtoto tumboni kwa kuboresha vituo vya afya 150 **ambapo jumla ya Shilingi bilioni 1.8 kutoka vyanzo vya ndani zimetengwa;**
- vii. Kuendelea kuboresha upatikanaji wa damu salama kwa kuongeza vituo 5 vya benki za damu katika mikoa yenye takwimu za vifo vingi vitokanavyo na uzazi ikiwemo mikoa ya Katavi, Rukwa, Ruvuma, Njombe na Manyara **jumla ya Shilingi bilioni 2 zimetengwa;**
- viii. Kuongeza upatikanaji wa huduma za kupima na matibabu ya mabadiliko ya awali ya saratani ya mlango wa kizazi na saratani ya matiti katika Vituo vya afya na zahanati 100 nchini;
- ix. Kuhakikisha wodi za watoto wachanga (neo natal ward) zinaanzishwa katika hospitali zote za Rufaa za mikoa na wilaya nchini;
- x. Kuendelea kutoa huduma za urutubishaji wa unga, mafuta na uongezaji wa madinjoto katika chumvi kwa mikoa yote nchini; na
- xi. Kuendelea kuelimisha na kuhamasisha jamii kuhusu masuala mbalimbali ya kiafya kupitia njia zote za mawasiliano, ikiwemo machapisho, vyombo vya habari, simu za kiganjani na mitandao ya kijamii.

HUDUMA ZA TIBA

Dawa, Vifaa, Vifaa Tiba na Vitendanishi.

- 189. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha 2017/18, Wizara itaendelea kuimarisha hali ya upatikanaji wa Dawa, Vifaa, Vifaa Tiba na Vitendanishi nchini kwa kununua na kuvisambaza katika vituo vya kutolea huduma za afya. **Jumla ya Shilingi bilioni 236 zimetengwa.**

Huduma za Damu Salama

190. Mheshimiwa Spika katika mwaka 2017/18, Wizara imetenga jumla ya **Shilingi bilioni 3.5** ili kuendelea kukabiliana na tatizo la uhaba wa damu salama kwa kutekeleza yafuatayo:

- i. Kukusanya chupa za damu salama 230,000 kukidhi mahitaji ya damu salama nchini; na
- ii. Kuendesha kampeni ya ukusanyaji wa damu kutoka katika makundi mbalimbali katika jamii.

Uimarishaji wa Huduma za kibingwa

191. Mheshimiwa Spika katika mwaka 2017/18, **Wizara itaendelea** kuimarisha upatikanaji na utoaji wa huduma za kibingwa nchini. Kupitia **Hospitali ya Taifa Muhimbili** kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na:

- i. Kuanzisha huduma za kubadilisha figo (renal transplant);
- ii. Kuanzisha huduma za upandikizaji wa vifaa vya kusaidia kusikia ambapo jumla ya **Shilingi milioni 206.3** zimetengwa kwa ajili ya kununua vifaa vya kusaidia kusikia.(cochlear implant);
- iii. Kuanza ujenzi wa jengo maalum kwa wagonjwa wanaolipia (private wing) ambapo jumla ya **Shilingi bilioni 14.5** zimetengwa;
- iv. Kununua Vifaa, Vitendanishi na Vifaa Tiba kwa lengo la kuboresha huduma za kibingwa ambapo jumla ya Shilingi bilioni 4 zimetengwa;

192. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa **Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI)**, katika mwaka 2017/18, Wizara itaendelea kutekeleza kazi zifuatazo:

- i. Kuendelea kutoa matibabu kwa maradhi yote ya Mgongo, mishipa ya fahamu na mifupa;
- ii. Kuwaongezea ujuzi wataalam wa upasuaji wa kubadilisha Nyonga na Goti;

- iii. Kuanza upasuaji wa vivimbe kwenye mishipa ya damu ya ubongo;
- iv. Kuboresha utoaji wa huduma kwa kununua vifaa na vifaa tiba vya kisasa kwa ajili ya jengo la MOI awamu ya tatu ambapo jumla ya Shilingi bilioni 2 zimetengwa; na
- v. Kuendelea kurejesha Mkopo uliotumika kugharamia ujenzi wa jengo hilo ambapo jumla ya **Shilingi bilioni 1.8** zimetengwa.

193. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2017/18, **Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete** itaendelea kuboresha huduma za matibabu ya moyo kwa kutekeleza yafuatayo:

- i. Kuboresha miundombinu ya kutolea huduma ikiwa ni pamoja kununua vifaa tiba kwa ajili ya chumba cha upasuaji ambapo jumla ya **Shilingi bilioni 2** zimetengwa,
- ii. Kuendelea kuwajengea uwezo wataalam; na
- iii. Kuandaa kambi mbalimbali za upasuaji kwa kushirikiana na madaktari bigwa kutoka nje ya nchi.

194. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2017/18, **Taasisi ya Saratani Ocean Road** itaendelea kuimarisha huduma za kinga, uchunguzi, mafunzo na tiba ya saratani kwa kutekeleza kazi zifuatazo:

- i. Kununua vifaa vya kisasa vya uchunguzi na matibabu ikiwa ni pamoja na PET Scan **ambapo kiasi cha Shilingi bilioni 14.5 zimetengwa**. Hatua hii inatarajiwa kupunguza rufaa za wagonjwa nje ya nchi zaidi ya asilimia 60 na hivyo kuokoa pesa za Serikali kiasi cha **Shilingi bilioni 5** kwa mwaka zinazotumika kulipia matibabu ya wagonjwa nje ya nchi;
- ii. Kuimarisha huduma za mkoba hasa katika maeneo ambayo yanaonekana kuwa na idadi kubwa ya watu waliogundulika kuwa na saratani; na
- iii. Kuimarisha upatikanaji wa dawa kwa wagonjwa wa saratani ili kupunguza mzigo kwa wagonjwa hasa wa kipato cha chini.

195. Mheshimiwa Spika, Wizara itaendelea kuboresha upatikanaji wa huduma za afya za kibingwa katika **Hospitali ya Benjamin Mkapa**

Dodoma kwa kutekeleza yafuatayo:

- i. Kununua vifaa na vifaa tiba ili kuboresha utoaji wa huduma za kibingwa ambapo jumla ya **Shilingi bilioni 1** zimetengwa;
- ii. Kuongeza watalaam wa fani mbalimbali na kuwajengea uwezo waliopo;
- iii. Kuanzisha maabara ya kisasa (cath lab) kwa ajili ya matibabu ya moyo pamoja na maabara yenye uwezo wa kuchunguza vinasaba; na
- iv. Kuanzisha huduma ya matibabu ya magonjwa ya Figo na njia ya mkojo (Dialysis) na upandikizaji wa Figo (Renal Transplant).

196. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2017/18, Wizara kupitia **Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe** itaendelea kuboresha upatikanaji wa huduma ya tiba ya afya ya akili katika kwa kutekeleza yafuatayo:

- i. Kununua vifaa na vifaa tiba **ambapo jumla ya Shilingi bilioni 1 zimetengwa**;
- ii. Kujenga uzio kuzunguka eneo la hospitali; na
- iii. Kuendelea na ukarabati wa wodi za wagonjwa.

197. Mheshimiwa Spika, Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini Mbeya itatekeleza kazi zifuatazo:

- i. Kuboresha na kupanua wigo wa huduma zinazotolewa kwa kufanya ukarabati jengo la daraja la kwanza na kukamilisha ujenzi wa jengo la watoto hivyo kuongeza uwezo kwa hospitali kutoka **vitanda 477** vya sasa mpaka vitanda **605**; na
- ii. Kuendelea na ujenzi wa jengo la kutoa huduma za radiolojia (Radiology) **ambapo jumla ya Shilingi bilioni 2 zimetengwa**.

198. Mheshimiwa Spika, Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Ziwa Bugando itatekeleza kazi zifuatazo:

- i. Kukarabati wa miundombinu ya kutolea huduma ikiwa pamoja na kliniki za wagonjwa wa nje, jengo la Saratani;

- ii. Kukamilisha ujenzi wa kliniki ya wanachama wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya; na
- iii. Kununua mashine ya Brachytherapy kwa ajili ya matibabu bora zaidi ya saratani.

199. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2017/18 **Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Kaskazini KCMC**, sambamba na kuendelea kutoa huduma itaendelea kutekeleza kazi zifuatazo:

- i. Kutekeleza awamu ya pili ya ujenzi wa wodi na hosteli za wagonjwa wa saratani utakaogharimu **Shilingi bilioni 2**; na
- ii. Kuendelea kuimarisha utoaji wa huduma za kusafisha figo.

200. Mheshimiwa Spika, **Hospitali Maalumu ya Kibong'oto** itaendelea kutekeleza kazi zifuatazo:

- i. Kuboresha miundombinu ya kutolea huduma ikiwa ni pamoja na ukarabati wa wodi za wagonjwa na maabara. Jumla ya Shilingi bilioni 1 zitatumika kutekeleza kazi hizo; na
- ii. Kutoa elimu kwa wataalam mbalimbali kwa ajili ya kuwajengea uwezo wa kuanzisha matibabu ya kifua kikuu sungu.

201. Mheshimiwa Spika, katika kuimalisha Huduma **za uchunguzi wa magonjwa** Wizara itaendelea na ujenzi wa maabara ya Taifa ya Afya ya Jamii katika eneo la Mabibo, Dar es salaam. Mradi huo hadi kukamilika unatarajiwa kutumia kiasi cha **Shilingi 7,493,193,434.97.00**.

202. Mheshimiwa Spika, kuhusu **Tiba Asili na Tiba Mbadala** Wizara itaendelea kutoa elimu kwa umma na waganga kupitia vyombo vya habari kuhusu usajili wa dawa za asili na maeneo ya kuzalishia dawa hizo.

203. Mheshimiwa Spika, katika mwaka, 2017/18, Wizara inakusudia kuboresha utoaji wa **huduma za uuguzi na ukunga** unaozingatia maadili, utu, na heshima ya mteja “respective care”. Aidha, Wizara inapanga kuandaa mafunzo ya muda mfupi kwa ajili ya kukidhi

mahitaji ya kurahisisha upatikanaji wa huduma muhimu zitolewazo na Wauguzi na Wakunga.

- 204. Mheshimiwa Spika,** Wizara itaendelea **kuboresha mfumo wa ufuatiliaji na upatikanaji wa takwimu za afya kutoka katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini**. kwa kuimarisha mfumo wa kielektroniki wa kutoa taarifa za vituo vya afya nchini yaani (**HMIS/DHIS2**) na uboreshaji wa mtandao wa kutoa taarifa za afya kupitia anuani ya **hmisportal.moh.go.tz**
- 205. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2017/18, Wizara kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI inatarajia kuimarisha mfumo wa mawasiliano kwa kutekeleza yafuatayo:
- i. Kufunga awamu ya kwanza ya mfumo wa kielektroniki wa kuhifadhi kumbukumbu za wagonjwa katika vituo vyote vya kutolea huduma za Afya na kutoa mafunzo ya matumizi ya mfumo huo;
 - ii. Kuanza kutumia TEHAMA katika kufuatilia wagonjwa na taarifa zao katika ngazi ya jamii hususan taarifa za vifo, uzazi, magonjwa ya mlipuko na magonjwa sugu kama kifua kikuu na UKIMWI (self-assessment) kwa kutumia mfumo wa simu za kiganjani; na
 - iii. Kuanzisha mfumo wa CHF mobile app ambao utarahisisha upatikanaji wa huduma za bima ya afya katika jamii.

RASILIMALI WATU KATIKA SEKTA YA AFYA

- 206. Mheshimiwa Spika,** Wizara itaendelea kusimamia eneo la rasilimali watu katika sekta ya afya ambapo katika mwaka 2017/18 kazi zifuatazo zitatekelezwa:
- i. Kudahili wanafunzi watarajari 13,632 katika vyuo vya afya vilivyoko chini ya Wizara;
 - ii. Kuendelea kugharamia mafunzo ya uzamili na uzamivu kwa watalaam wa kada mbalimbali za afya; na
 - iii. Kuendelea kuboresha miundombinu katika Vyuo vya Afya kwa kufanya ukarabati na upanuzi wa vyuo ambapo jumla ya **Shilingi bilioni 3** zimetengwa.

207. Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza vipaumbele vilivyoainishwa katika mwaka 2017/18, kazi zitakazotekelezwa na fungu 53 ni zifuatavyo;

MAENDELEO YA JAMII

208. Mheshimiwa Spika, ili kufanikisha kufikiwa kwa malengo ya nchi ya kufikia Uchumi wa kati kupitia wataalam hawa, Wizara katika mwaka 2017/18 pamoja na mambo mengine itatekeleza yafuatayo:

- i. Kuendelea kuhamasisha Halmashauri na Mikoa kuajiri watumishi wa fani ya Maendeleo ya Jamii;
- ii. Kuendelea kuboresha utekelezaji wa shughuli za Maendeleo ya Jamii ikiwemo kuimarisha mfumo wa ufuatiliaji na tathmini wa shughuli za maendeleo na ustawi wa jamii katika ngazi za Sekretarieti za Mkoa na Mamlaka za Serikali za Mtaa. Uimarishaji wa mfumo huu utawezesha serikali kupata taarifa sahihi za ushiriki wa Jamii katika kuleta maendeleo ya nchi yetu;
- iii. Kuendelea kuwajengea uwezo Wataalam wa Maendeleo ya Jamii wa kusimamia sera na miongozo ya Wizara ili waweze kuishirikisha jamii katika kujiletea maendeleo;
- iv. Kuendelea kuwezesha vyuo kuandaa na kutoa wataalam wa maendeleo ya jamii katika Vyuo 8 na Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru katika ngazi za Astashahada, Stashahada, Shahada na Stashahada ya Uzamili;
- v. Kuboresha miundombinu ya vyuo na mazingira ya kujifunzia na kufundishia; na
- vi. Kuimarisha ubora wa wataalam wa maendeleo ya jamii wanaozalishwa na Taasisi kwa kuandaa mitaala ya NTA level 4 & 9 itakayozingatia hali halisi ya mabadiliko na mahitaji ya jamii.

MAENDELEO YA JINSIA

209. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2017/18, Wizara itaendelea kusimamia maendeleo ya jinsia kwa kutekeleza yafuatayo:-

Kuwawezesha wanawake kiuchumi

- i. Kupitia Benki ya Wanawake Tanzania kutoa Mikopo yenye thamani ya Shilingi bilioni 12 kwa wajasiriamali wanawake 9,650 katika mikoa ya Dares Salaam, Mbeya, Njombe, Iringa, Dodoma, Ruvuma, Pwani na Mwanza;
- ii. Kuwezesha Akaunti ya Malaika kufanya kazi kwa ufanisi na kuwafikia wanawake wajasiriamali walengwa;
- iii. Kuhamasisha uanzishwaji wa majukwaa ya uwezeshaji wanawake kiuchumi katika mikoa yote ya Tanzania Bara kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi pamoja na Ofisi ya Rais TAMISEMI;
- iv. Kuendelea kuhakikisha Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake unawafikia wanawake wengi. Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais – TAMISEMI katika mwaka 2017/18, itaendelea kuhamasisha Halmashauri kuchangia asilimia tano (5%) ya mapato yao ya ndani katika Mfuko;
- v. Kuboresha mfumo wa taarifa za mikopo na wanufaika wa mfuko, kazi itafanyika kwa kushirikiana na OR – TAMISEMI;
- vi. Kusambaza mwongozo wa uendeshaji wa Mfuko ulioboreshwa kwa Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri zote nchini; na
- vii. Kuzijengea uwezo Kamati za Mikopo za Mfuko katika Halmashauri 15 kuhusu uendeshaji na usimamizi wa Mfuko ili kuimarisha utendaji na usimamizi wake kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais – TAMISEMI.

Kuzuia na Kutokomeza Ukatili wa Kijinsia

- viii. Kusambaza na kuwezesha kuanza kutumika kwa Daftari la kutunza taarifa za ukatili wa kijinsia katika Mamlaka za Serikali za Mitaa na Sekretarieti za Mikoa ili kuimarisha upatikanaji na ubora wa taarifa na takwimu za ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto;
- ix. Kuimarisha Kamati 51 za Ulinzi wa Wanawake na Watoto; na
- x. Kufuatilia utekelezaji wa afua za kuzuia ukatili wa kijinsia hususan dhidi ya wanawake na watoto.

Ushiriki wa Wanawake katika Ngazi za Uongozi na Maamuzi

- i. Kuendelea kuhuisha Kanzidata inayoonesha wasifu wa wanawake kwa ajili ya kuwawezesha kushiriki katika fursa za uongozi, ngazi za maamuzi na ajira; na
- ii. Kuziwezesha taasisi mbalimbali kutumia taarifa katika kanzidata kuajiri, kufanya uteuzi na maamuzi mbalimbali ya kisera.

Uingizaji wa Masuala ya Jinsia Katika Sera, Sheria na Mipango ya Kisekta na Taifa

- i. Kukamilisha mapitio ya Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia ya mwaka 2000 pamoja na Mkakati wake. Mapitio ya Sera hiyo yatawezesha kuzingatiwa kwa masuala muhimu ikiwemo Malengo ya Maendeleo Endelevu, Agenda ya Afrika Tuitakayo 2063, Mpango wa Taifa wa Maendeleo Miaka Mitano na kukidhi mahitaji ya sasa ya kufikia usawa wa kijinsia na uwezeshaji wanawake nchini; na
- ii. Kupitia Mwongozo wa uingizaji wa masuala ya jinsia katika Sekta zote pamoja na kuandaa Kanzidata kwa ajili ya kuhifadhi taarifa za hali ya jinsia nchini.

MAENDELEO YA MTOTO

Ukatili dhidi ya watoto

210. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2017/18, kupitia Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto, Wizara pamoja na mambo mengine itatekeleza yafuatayo:

- i. Kuimarisha utendaji wa kamati za ulinzi wa mtoto katika Mamlaka za Serikali ya Mitaa kuanzia ngazi ya Vijiji, Kata na Halmashauri za Wilaya;
- ii. Kuendelea kutoa mafunzo kuhusu malezi chanya na athari za ukatili dhidi ya watoto katika Halmashauri 12 za Mikoa ya Lindi na Mtwara;
- iii. Kuhamasisha kuanzishwa kwa mfumo wa ulinzi wa mtoto katika shule za msingi kwa ajili ya kukabiliana na vitendo vya ukatili dhidi ya mtoto katika mazingira ya shule;
- iv. Kuendelea kuelimisha wazazi, walezi na jamii kutokomeza mila na desturi zinazoathiri afya na maendeleo ya mtoto wa

kike na kumnyima haki kuendelea na masomo na hivyo kufifisha ndoto zake;

- v. Kuendelea kuhamasisha uanzishwaji wa klabu katika shule za msingi na sekondari; na
- vi. Kuendelea kusimamia upatikanaji wa haki ya ushiriki wa mtoto kupitia mabaraza ya watoto. Kwa mwaka 2017/18, Wizara itaendelea kuhamasisha Halmashauri kuanzisha mabaraza ya Watoto ili kuongeza idadi kutoka 108 iliyopo sasa hadi kufikia 140 na kuyawezesha kutekeleza wajibu wake ipasavyo.

HUDUMA ZA USTAWI WA JAMII

211. Mheshimiwa Spika Wizara imeendelea kuweka mifumo ya matunzo, malezi na ulinzi wa watoto yenye misingi ya kijamii. Kwa mwaka 2017/18, pamoja na mambo mengine itafanya yafuatayo:

- i. Kuendelea kuzijengea uwezo Halmashauri na wadau wengine kuweka mifumo imara ya matunzo na ulinzi kwa watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi;
- ii. Kuhamasisha na kuelimisha waajiri kuzingatia marekebisho ya Sheria ya Kazi na Mahusiano Kazini hususan kifungu cha 33(10) na kuzifanyia marekebisho kupitia Kanuni zake mpya kwa kutoa fursa kwa waajiriwa wanawake kupata haki ya kunyonyesha watoto wao;
- iii. Kuendelea kuratibu na kusimamia uanzishwaji na uendeshaji wa vituo vya malezi ya watoto pamoja na kuwajengea uwezo watoa huduma za malezi na makuzi ya awali ya Watoto;
- iv. Kuendelea kuwajengea uwezo watoa huduma kwa watoto wanaokinzana na sheria ili kuimarisha upatikanaji wa haki kwa wakati;
- v. Kuendelea kuwezesha utoaji wa huduma za usuluhishi na ushauri nasaha ili kuleta utulivu na uimara katika ndoa kwa maendeleo na ustawi wa taifa;
- vi. Kuendelea kuwajengea uwezo wataalam wa Maendeleo ya Jamii na Ustawi wa Jamii katika Halmashauri ili kuboresha makuzi na malezi katika familia kwa lengo la kupunguza vitendo vya ukatili wa watoto kwenye jamii;
- vii. Kuendelea kuongeza idadi ya wanafunzi wanaodahiliwa

- katika fani mbalimbali; na
- viii. kuboresha miundombinu ya kufundishia na kujifunzia na kuanzisha kituo cha utafiti na ubunifu katika fani ya ustawi wa jamii ili kuongeza ufanisi katika kufundisha.

HAKI NA USTAWI WA WAZEE

- 212. *Mheshimiwa Spika***, wazee ni rasilimali muhimu kwa maendeleo ya taifa kutokana na uzoefu na ujuzi walionao katika nyanja mbalimbali. Katika mwaka 2017/18, Wizara itaendelea kuboresha huduma, makazi ya wazee na kuimarisha upatikanaji wa haki kwa wazee kote nchini na kutokomeza mauaji ya wazee.

MASHIRIKA YASIYO YA KISERIKALI

- 213. *Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kuweka mazingira wezeshi kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kushiriki kikamilifu katika kuchangia kufikiwa kwa maendeleo na ustawi wa jamii. Kwa mwaka 2017/18, Wizara itaendelea kusajili na kuratibu utendaji wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu zilizopo. Aidha, Wizara itaendelea kufuatilia utendaji wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na kuhakikisha yanatoa mchango unaotarajiwa kwa maendeleo na ustawi wa jamii.
- 214. *Mheshimiwa Spika***, aidha Taasisi zilizo chini ya Wizara zitaendelea kuboresha upatikanaji wa huduma kwa kutekeleza na Mipango ya Maendeleo ikiwa ni pamoja na:
- i. Kupanua maghala ya MSD katika Kanda ya Dar es Salaam;
 - ii. Kufanya upanuzi wa maabara ya Makao Makuu ya Mamlaka ya Chakula na Dawa ili kuongeza ufanisi katika uchunguzi wa bidhaa;
 - iii. Kuanza udhibiti wa vitendanishi na vifaa vya maabara, kukamilisha ununuzi wa vifaa vya maabara ya kisasa ya TFDA Kanda ya Ziwa, Mwanza;
 - iv. Kuanza ujenzi wa jengo la Maabara na ofisi za TFDA kwa ajili ya kanda ya Kati – Dodoma;
 - v. Kununua mitambo na vifaa mbalimbali vya maabara ya Wakala wa Mkemia Mkuu wa Serikali ambapo jumla ya Shilingi **bilioni 10 zimetengwa**;

- vi. Kukamilisha ujenzi wa Maabara ya Mkemia Mkuu na Ofisi ya Kanda ya Kaskazini – Arusha;
- vii. Kukarabati maabara ya Vinasaba vya Binadamu ya Mkemia Mkuu wa Serikali iliyopo Dar es Salaam; na
- viii. Kuboresha utafiti na uzalishaji wa dawa za asili katika Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR) kwa kununua mashine za kisasa kwa ajili ya kiwanda cha kuzalisha dawa za asili Mabibo. Jumla ya **Shilingi milioni 800 zimetengwa.**

Taasisi za Mafunzo ya Maendeleo ya Jamii

- 215. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/18, Wizara kupitia **Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru** itaendelea kuongeza udahili wa wanafunzi katika fani mbalimbali. Aidha, Wizara itaboresha miundombinu ya vyuo; na mazingira ya kujifunzia na kufundishia. Vilevile, itaimarisha ubora wa wataalam wa maendeleo ya jamii wanaozalishwa na Taasisi kwa kuandaa mitaala ya NTA level 4 & 9 itakayozingatia hali halisi ya mabadiliko na mahitaji ya jamii.

Aidha, Wizara itaendelea kuratibu utoaji wa mafunzo ya maendeleo ya jamii kupitia **Vyuo (8) vya Maendeleo ya Jamii** pamoja na kuimarisha mazingira ya kufundishia na kujifunzia. Lengo ni kuongeza idadi ya wanafunzi wanaoijiunga na mafunzo katika vyuo hivyo ikiwa ni pamoja na kudurusu Mtaala wa Mafunzo kwa Vyuo vya Maendeleo ya Jamii ili kuendana na mahitaji ya soko la ajira na kuwawezesha wahitimu kujijaji.

Taasisi ya Ustawi wa Jamii

- 216. Mheshimiwa Spika**, Katika kuhakikisha tunakua na wataalam wa Ustawi wa Jamii katika ngazi za Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara kupitia Taasisi ya Ustawi wa Jamii imeendelea kuzalisha wataalam hao kupitia mafunzo katika fani za Ustawi wa Jamii na fani nyingine ikiwemo Rasilimali Watu na Mahusiano Kazini kwa ngazi ya Astashahada, Stashahada, Shahada, Stashahada ya Uzamili na Shahada ya Uzamili. Katika mwaka 2017/18, Taasisi

itaendelea kuongeza idadi ya wanafunzi wanaodahiliwa katika fani mbalimbali, kuboresha miundombinu ya kufundishia na kujifunzia na kuanzisha kituo cha utafiti na ubunifu katika fani ya ustawi wa jamii ili kuongeza ufanisi katika kufundisha. Aidha, Taasisi inatarajia kukamilisha mchakato wa kuanzisha shahada ya uzamili katika fani ya rasilimali watu na shahada ya maendeleo ya jamii.

MABARAZA YA KITAALUMA

- 217. *Mheshimiwa Spika***, Serikali itaendelea kutambua umuhimu wa taaluma mbalimbali zilizomo katika sekta ya afya; kwa kuzingatia hilo, Serikali itasimamia sheria mbalimbali za wanataaluma wa taaluma hizo. Aidha, Wizara itaendelea kusimamia utoaji wa huduma kupitia hospitali na maabara binafsi nchini.

USHIRIKIANO WA NDANI NA NJE YA NCHI

- 218. *Mheshimiwa Spika***, Wizara iliendelea kushirikiana na nchi rafiki katika kuimarisha Sekta ya Afya nchini. Aidha, Wizara iliratibu na kushiriki kwenye mikutano ya jumuiya za kikanda za SADC, EAC, ECSA-HC na mashirika mengine ya kitaifa na kimataifa na katika kutekeleza maamuzi ya pamoja yenye manufaa kwa taifa. Katika mwaka 2017/18, Wizara itaimarisha ushirikiano na nchi rafiki na Mashirika ya Kimataifa yanayosaidia Wizara yangu. Aidha, itaimarisha ushirikiano na sekta nyingine ambazo zinachangia katika kutoa huduma za afya na ustawi wa jamii nchini. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na mikoa na wadau wa sekta itaendelea kuadhimisha siku mbalimbali za afya za kitaifa na kimataifa kwa lengo la kuhamasisha na kufikisha ujumbe kwa umma. Baadhi ya siku hizo ni za Afya, Malaria Afrika, UKIMWI, Kifua Kikuu, Ukoma, Wazee, Kutotumia Tumbaku, Tiba Asili ya Mwafrika, Wachangia Damu, Utepe Mweupe, Siku ya Wauguzi na Fimbo Nyeupe na Siku ya Mtoto Njiti duniani.

IV: SHUKRANI

219. *Mheshimiwa Spika*, napenda kuchukua nafasi hii ya kipekee kuzishukuru nchi za Denmark (DANIDA), Uswisi (SDC), na Ireland (Irish Aid), Canada (DFATD) na Mashirika ya Kimataifa yakiwemo Benki ya Dunia, UNICEF, na UNFPA kwa kutoa misaada katika Mfuko wa Pamoja wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ambao umesaidia kwa kiasi kikubwa kuboresha huduma za afya nchini. Aidha, naishukuru na kuipongeza Korea Kusini kupitia shirika lake la Maendeleo (KOICA) kwa kuamua kujiunga na nchi zinazochangia fedha katika Mfuko wa pamoja kwa ajili ya huduma za afya kuanzia mwaka 2016/17. Pia, napenda kuzishukuru nchi za Canada, China, Cuba, Hispania, India, Italia, Japan, Marekani, Misri, Sweden, Uingereza, Ujerumani na Ufaransa na ambazo zimeendelea kuisaidia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa njia mbalimbali.

220. *Mheshimiwa Spika*, vilevile nayashukuru mashirika mengine ya Kimataifa kwa ushirikiano wao waliotoa kwa Wizara. Mashirika haya yanajumuisha Mfuko wa Dunia Kupambana na UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria (*GFATM*), Benki ya Maendeleo ya Afrika (*AfDB*), Benki ya Nchi za Kiarabu kwa ajili ya Maendeleo ya Uchumi ya Nchi za Afrika (*BADEA*), Jumuiya ya Nchi za Ulaya (EU), Global Alliance on Vaccine (*GAVI*), Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki (*IAEA*), Shirika la Umoja wa Mataifa la Kudhibiti UKIMWI (*UNAIDS*), Shirika la Umoja wa Kimataifa la Maendeleo (*UNDP*), *UNFPA*, *UN-Women*, Shirika la Afya Duniani (*WHO*) na Benki ya Dunia (*WB*). Wengine ni *Abbott Fund*, *BASIC NEED (UK)*, *ACF – Canada*, *Baylor College of Medicine* ya Marekani, *Canadian Bar Association*, *CDC*, *CORDAID (Netherlands)*, *CUAMM*, *DANIDA*, *DFID*, *Engender Health (USA)*, *EED*, *Elizabeth Glaser Paediatric Aids Foundation (EGPAF)*, *Family Health International (FHI360)*, *FINIDA*, *GIZ*, *Good Samaritan Foundation (GSF)*, *German TB and Leprosy Relief Association (GLRA)*,

HelpAge International, ILO, Jane Adams School of Social Work ya Chuo Kikuu cha Illinois Marekani, John Snow Incorporation (JSI), JICA, KOICA, KfW, Global Partnership for Education (GPE), Madaktari Afrika na Madaktari Wasio na Mipaka (Medicins Sans Frontieres – MSF), MSERIOR, ORIO, P4H, SAREC, SDC, SIDA (Sweden), Shirika la Upasuaji la Spain, SIGN la Marekani, na Shirika la Human Resource Capacity Project, Touch Foundation, USAID na, Children Investment Foundation Fund (CIFF), World Lung Foundation.

- 221. *Mheshimiwa Spika***, ninawashukuru pia Wadau wa Maendeleo ambao ni African Programme for Orchorceriasis Control, *Africare*, *Axios International*, *Aids Relief Consortium*, *AIHA*, *ASCP*, *ASM*, *APHL*, *Balm and Gillead Foundation*, *Bill and Melinda Gates Foundation*, *Clinton Health Access Initiative*, *CLSI*, *CMB*, *Christoffel Blinden Mission (CBM)*, *Christian Relief Services (CRS)*, *Citi Bank*, *Department of Defence ya Marekani*, *Community of Saint Egidio (DREAM)*, *Duke University*, *ECSA*, *Futures Group*, *Glaxo Smith Kline (GSK)*, *General Electric (GE – USA)*, *Havard University na University of Maryland*, *Helen Keller International*, *Henry Jackson Foundation*, *IMA*, *ICAP*, *International Trachoma Initiative*, *Intrahealth*, *International Eye Foundation*, *I-TECH*, *Jhpiego*, *Johns Hopkins University*, *Labiofarm Industry*, *London School of Hygiene and Tropical Medicine*, *Management Science for Health (MSH)*, *MEDA*, *Merck & Company*, *Malaria No More*, *Military Advancement for Medical Research*, *NOVARTIS*, *Pathfinder*, *PATH*, *President’s Emergency Plan for AIDS Relief (PEPFAR)*, *Pharm Access International*, *PactWorld*, *Plan International*, *Pfizer*, *Qiagen*, *Research Triangle Institute (RTI)*, *Regional Psychosocial Support Initiatives (REPSSI)*, *Saint Thomas Hospital- London*, *Save the Children*, *SightSavers International*, *Supply Chain Management Systems (SCMS) na University of Columbia*, *URC*, *USA-Presidential Malaria Initiative (PMI)*, *World Vision*, *FXB*, *Walter REED Army Institute of Research (WRAIR) na World Education Inc.*

- 222. Mheshimiwa Spika**, ninawashukuru watu binafsi, vyama vya hiari na mashirika yasiyo ya kiserikali ya ndani ya nchi kwa kuwa mstari wa mbele katika kuchangia uimarishaji wa huduma za afya. Mashirika hayo ni pamoja na AGOTA, Aga Khan Foundation, APHFTA, AMREF, AGPAHI, APT, BAKWATA, Benjamin William Mkapa HIV/AIDS Foundation, CCBRT, CSSC, CCT, Counsenuth, ELCT, Ifakara Health Institute, Lions Club, MAT, AFRICARE, Msalaba Mwekundu, MEHATA, MEWATA, MUKIKUTE, FAWETA, TAMWA, TAWLA, TGNP, MDH, MeLSAT, PASADA, PAT, PSI, PRINMAT, Rotary Club International, SIKIKA, Shree Hindu Mandal, TANNA, TPHA, TPRI, Tanzania Surgical Association (TSA), Tanzania Society of Anaesthesiologist of Tanzania (SATA), Association of Gynaecologists and Obstetricians of Tanzania (AGOTA), Association of Paedricians of Tanzania (PAT), Tanzania Diabetic Association, TANESA, THPS, TUNAJALI, Tanzania Midwife Association, TDA, TAYOA, TISS, TEC, UMATI, USADEFU, White Ribbon Alliance, Mabaraza yote ya Kitaaluma, Mashirika, hospitali na vituo vya kutolea huduma za afya na ustawi wa jamii nchini pamoja na vyama vyote vya kitaaluma vya sekta ya afya.
- 223. Mheshimiwa Spika**, navishukuru Vyuo Vikuu vya Dar es Salaam, Muhimbili, Sokoine, Ardhi, Mzumbe, Dodoma, Chuo Kikuu Huria, Kumbukumbu ya Hurbert Kairuki, IMTU, Tumaini, St. Agustino, CUHAS, Sebastian Kolowa, St. John, Aga Khan, Morogoro Muslim, Taasisi ya Teknolojia ya Nelson Mandela, Arusha pamoja na Vyuo vyote vilivyo chini ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa kuwa mstari wa mbele katika kuchangia uimarishaji wa huduma za afya na maendeleo ya jamii. Aidha, nawashukuru wadau wengine waliotoa huduma ya elimu kwa njia za redio, televisheni, magazeti na mitandao ya kijamii katika masuala ya afya na maendeleo ya jamii.
- 224. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi hiki cha utendaji wangu wa kazi nikiwa Waziri, nimepata ushirikiano mkubwa kutoka kwa viongozi na wafanyakazi wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Napenda kumshukuru **Mheshimiwa Dkt.**

Hamisi Andrea Kigwangalla (Mb.), Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa ushirikiano anaonipa katika kutekeleza majukumu yangu. Aidha naomba kuwashukuru **Dkt. Mpoki M. Ulisubisya** Katibu Mkuu (Afya) na **Bibi Sihaba Nkinga** Katibu Mkuu (Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto) kwa mchango wao katika kuwezesha utekelezaji wa majukumu yangu. Vilevile, nawashukuru **Prof. Muhammad Bakari Kambi**, Mganga Mkuu wa Serikali Makamishna, Wakurugenzi na Wakuu wa Vitengo vya Wizara yangu. Nawashukuru pia Wakurugenzi wa Hospitali ya Taifa Muhimbili, MOI, JKCI, ORCI, BMH, Mirembe, Kibongoto na Wakurugenzi wa Hospitali za Rufaa za Kanda za Mbeya, Bugando, na KCMC na Taasisi zilizo chini ya Wizara, Waganga Wakuu wa Mkoa na Wilaya, Waganga Wafawidhi wa Hospitali, Vituo vya Afya na Zahanati, Wakuu wa Taasisi, Wakuu wa Vyuo vya Mafunzo vilivyo chini ya Wizara na watumishi wote wa wizara, Mashirika ya Dini, Mashirika ya Kujitolea na Mashirika Binafsi. Natoa shukrani kwa sekta zote ambazo tunashirikiana nazo katika kutoa huduma za afya na ustawi wa jamii pamoja na wananchi wote kwa ushirikiano wao. Kwa namna ya pekee napenda kuwashukuru watumishi wote wa sekta ya afya, maendeleo na ustawi wa jamii wakiwemo madaktari, wauguzi na wakunga kwa kuendelea kutoa huduma kwa wananchi. Naomba waendeleo kuzingatia misingi ya kutoa huduma bora, maadili ya kazi na kufanya kazi kwa bidii kwa manufaa ya taifa letu

225. Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii pia kuishukuru familia yangu, kwa uvumilivu wao na pia kwa kunitia moyo katika kutekeleza majukumu yangu ya Kitaifa. Kwa Viongozi na Wananchi hasa wanawake wa Mkoa wa Tanga ninawashukuru kwa ushirikiano wanaoendelea kunipatia katika utekelezaji wa majukumu yangu. Naahidi kuwa nitaendelea kuwaenzi na kuwatumikia kwa nguvu zangu zote ili kuleta mabadiliko ya haraka ya kimaendeleo katika Mkoa wetu.

V: MAOMBI YA FEDHA KWA KAZI ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA KATIKA MWAKA WA FEDHA 2017/18

Fungu 52 - Afya

Mapato

226. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2017/18 Wizara imekadiria kukusanya mapato ya **Shilingi 225,038,495,525.00** Kati ya fedha hizo **Shilingi 207,472,729,612.00** zitakusanywa katika mashirika na Taasisi zilizo chini ya Wizara na **Shilingi 17,565,765,913.00** ni kutoka katika vyanzo vya makao makuu. Vyanzo hivyo vinatokana na makusanyo ya uchangiaji wa huduma za afya, tozo na ada mbalimbali, usajili wa vituo binafsi vya kutolea huduma, maabara binafsi na Mabaraza ya Kitaaluma.

Matumizi ya Kawaida

227. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2017/18, Wizara inakadiria kutumia kiasi cha **Shilingi 291,895,940,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 64,063,937,000.00** zitatumika kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na **Shilingi 227,832,003,000.00** zitatumika kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi. Kati ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya Mishahara **Shilingi 49,036,786,000.00** ni kwa ajili ya watumishi wa Wizara, Makao Makuu na **Shilingi 178,795,217,000.00** ni kwa ajili ya watumishi wa Taasisi, Mashirika na Wakala zilizo chini ya Wizara.

Miradi ya Maendeleo

228. *Mheshimiwa Spika*, kwa upande wa shughuli za maendeleo, Wizara inakadiria kutumia **Shilingi 785,805,952,000.00** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya hizo, fedha za ndani ni **Shilingi 336,300,000,000.00** na fedha za nje ni **Shilingi 449,505,952,278.00**.

Jumla ya Makadirio ya Bajeti kwa 2017/18 kwa Fungu 52 ni **Shilingi 1,077,701,892,000.00**

Fungu 53 – Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto

- 229. Mheshimiwa Spika**, Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli na Matumizi kwa Mwaka 2017/18 kwa Fungu – 53 ni kama ifuatavyo:

Makusanyo ya Maduhuli

Wizara inataraji kukusanya Maduhuli yenye jumla ya **Shilingi 2,101,874,000.00** ambazo ni kutokana na ada za wanafunzi kutoka Vyuo 8 vya Maendeleo ya Jamii, ada za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na mauzo ya vitabu vya zabuni.

Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo

Makadirio ya Matumizi ya Kawaida kwa mwaka 2017/18, ni **Shilingi 35,300,602,090.00** ambapo Mishahara ni **Shilingi 19,142,252,240.00** na **Shilingi 16,158,349,850.00** ni Matumizi Mengineyo. Aidha, Miradi ya Maendeleo inakadiriwa kutumia kiasi cha **Shilingi 2,606,278,000**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 2,000,000,000.00** ni fedha za ndani na **Shilingi 606,278,000** ni fedha za nje.

Jumla ya Makadirio ya Bajeti kwa 2017/18 kwa Fungu 53 ni **Shilingi 37,906,880,090**

- 230. Mheshimiwa Spika**, Jumla kuu ya fedha zote zinazoombwa ni **Shilingi 1,115,608,772,090.00**
- 231. Mheshimiwa Spika**, Hotuba hii inapatikana pia katika tovuti za Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto www.moh.go.tz. na www.mcdgc.go.tz.
- 232. Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja

Kiambatisho Na. 1.**Halmashauri zilizopata pikipiki**

Mkoa	Halmashauri	Idadi ya Pikipiki
Arusha	Meru	1
	Loliondo	1
	Ngorongoro	1
	Karatu	1
	Monduli	1
Dodoma	Kondoa	1
	Chemba	1
	Mpwapwa	1
Geita	Mbogwe	1
	Chato	1
	Nyang'hwale	1
	Bukombe	1
Iringa	Iringa	1
	Kilolo	1
Kagera	Biharamulo	1
	Ngara	1
	Muleba	1
	Kyerwa	1
	Karagwe	1
Katavi	Mlele	1
	Mpanda Manispaa	1

Mkoa	Halmashauri	Idadi ya Pikipiki
	Mpanda	1
	Nsimbo	1
Kigoma	Uvinza	1
	Kigoma	1
	Kasulu	1
	Buhigwe	1
	Kakonko	1
Kilimanjaro	Rombo	1
	Same	1
	Mwanga	1
Lindi	Liwale	1
	Kilwa	1
	Nachingwea	1
	Lindi	1
	Ruangwa	1
Manyara	Hanang	1
	Simanjiro	1
	Kiteto	1
Mara	Musoma	1
	Butiama	1
	Rolya	1
	Serengeti	1
Mbeya	Mbarali	1

Mkoa	Halmashauri	Idadi ya Pikipiki
	Kyela	1
	Chunya	1
	Busokelo	1
Songwe	Ileje	1
	Momba	1
	Songwe	1
Morogoro	Gairo	1
	Kilosa	1
	Mvomero	1
	Ulanga	1
Mtwara	Tandahimba	1
	Newala	1
	Nanyumbu	1
	Masasi	1
Mwanza	Ukerewe	1
	Magu	1
	Sengerema	1
	Kwimba	1
Njombe	Ludewa	1
	Makete	1
	Wanging'ombe	1
Pwani	Bagamoyo	1
	Kibaha	1

Mkoa	Halmashauri	Idadi ya Pikipiki
	Mafia dc	1
	Rufiji	1
Rukwa	Sumbawanga dc	1
	Nkasi	1
	Kalambo	1
Ruvuma	Nyasa dc	1
	Namtumbo	1
	Mbinga	1
	Tunduru	1
Shinyanga	Shinyanga dc	1
	Kishapu	1
	Msalala	1
	Ushetu	1
Simiyu	Meatu	1
	Busega	1
	Itilima	1
	Bariadi dc	1
	Maswa	1
Singida	Mkalama	1
	Iramba	1
	Ikungi dc	1
	Singida dc	1
Tabora	Igunga	1

Mkoa	Halmashauri	Idadi ya Pikipiki
	Sikonge	1
	Kaliua	1
	Uyui	1
	Nzega	1
Tanga	Kilindi	1
	Handeni	1
	Mkinga	1
	Bumbuli	1
	Korogwe dc	1
	Muheza	1



Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Mhe. Umyy Mwalimu akipanda viazi katika eneo la kituo na kiwanda cha kuongeza thamani mazao ya nafaka cha Ititi kinachomilikiwa na vikundi vya akina mama VICOBA wa wilaya ya Singida, kulia kwake ni Mhe. Mbunge, Aishrose Matembe (Singida) na kushoto kwake ni Mkurugenzi Mkazi wa shirika la UN women Tanzania Maria Karadenizli, na wa kwanza kushoto ni Mkuu wa Mkoa wa Singida Dkt. Rehema Nchimbi.



Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Mhe. Dkt. Hamis Kigwangalla akifanya ukaguzi wa utolewaji wa huduma za Afya katika chumba cha upasuaji cha Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Kigoma.



Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan wa pili kulia akiwa katika matembezi ya pamoja na baadhi ya viongozi wa kitaifa wakati wa uzinduzi wa kampeni ya kufanya mazoezi iliyofanyika katika viwanja vya leaders jijini Dar es salaam hivi karibuni, wa kwanza kulia ni Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Mhe. Ummu Mwalimu, katikati ni Rais Mstaafu wa Awamu ya Pili Mhe. Al Haji Ali Hassan Mwinyi, wa kwanza kushoto ni Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia , Wazee na Watoto Mhe. Dkt. Hamis Kigwangalla na wa pili kushoto ni Mkuu wa Mkoa wa Dar es salaam Mhe. Paul Makonda.



Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Mhe. Ummu Mwalimu wa kwanza kulia alipotembelea wodi ya wazazi katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Iringa.